World Vision

# Kijitabu cha Ujumuishaji wa USAWA WA KIJINSIA NA UHUSISHAJI WA KIJAMII

## katika Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini



June 2023

## SHUKRANI

Kijitabu hiki kisingeweza kuandikwa bila mchango na jitihada za watu na timu mbalimbali:

**Waandishi**

Godfrey Senkaba, Meneja wa Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini, World Vision U.S.
Dr. Jacqueline Ogega, Mkurugenzi Mkuu wa Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii, World Vision U.S.
Leticia Nkonya, PhD, Mtaalamu Mshauri Mkuu wa Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii, World Vision U.S.
Edward Winter, Mtaalamu Mshauri Mkuu wa Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii, World Vision U.S.
Zayid Douglas, Mtaalamu Mshauri Mkuu wa Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii, World Vision U.S.

**Wachangiagji**

Sarah Shteir, Mtaalamu Mshauri Mkuuwa Usawa wa Kijinsia, World Vision Australia (*wa zamani*)
Albana Dino-Spiro, Mkurugenzi Mkuu wa Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini, World Vision International
Whitney King, Kujifunza na Ufanisi wa Programu, World Vision International
Natalia Cipolla, Meneja Maendeleo ya Biashara wa Sekta ya Afya, World Vision U.S.
Wawakilishi wa GESI wa World Vision U.S.
Includovate Pty Ltd
Stephanie Pierce-Conway, Pierce Conway Design, Graphic Design

**Upitiaji na Utafiti wa Jaribio**

Timu ya World Vision Honduras
Timu ya World Vision Kenya
Timu ya World Vision Malawi
Timu ya World Vision Zambia

Shukrani za pekee kwa Dr. Leticia Nkonya na Aloisia Shemdoe kwa kufasili kijitabu hiki.


*World Vision ni shirika la kidini la kusaidia watu lililojitoa kwa ajili ya kufanya kazi na watoto, familia, na jamii zao duniani kote ili kuwawezesha kufikia uwezo wao kikamilifu kwa kupambana na vyanzo vya umaskini na ukosefu wa haki.*

© World Vision | June 2023

# YALIYOMO


**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **II**

**ORODHA YA VIELELEZO** ........ **II**

**KUHUSU KIJITABU** ........ **2**

**SEHEMU 1 KUTAMBULISHA LENZI YA GESI** ........ **4**

ZANA 1.1 Jinsi ya Kutumia Lenzi ya GESI ........ 4

ZANA 1.2 Viwango vya Chini vya GESI ........ 8

ZANA 1.3 Tafakuri ya Mtu Mmoja Mmoja ........ 12

**SEHEMU 2 JINSI YA KUFANYA UCHANGANUZI WA GESI** ........ **18**

ZANA 2.1 Uchanganuzi wa GESI ........ 18

Hatua 1: Tafakuri ya Pamoja ........ 20

Hatua 2: Mapitio ya Maandiko na Ukusanyaji wa Data za Upili wenye Muitikio wa GESI ........ 23

Hatua 3: Ukusanyaji wa Data za Msingi wenye Muitikio wa GESI ........ 33

Hatua 4: Uchanganuzi wa Data na Uandishi wa Ripoti wenye Muitikio wa GESI ........ 34

MVL1: Kuelewa Mazingira Hatarishi ........ 35

MVL2: Ramani ya Kijamii ........ 38

MVL3: Uchanganuzi wa Majukumu na Wingi wa Kazi ........ 42

MVL4: Tathmini ya Desturi za Kijinsia na Kijamii ........ 45

**SEHEMU 3 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE USANIFU WA PROGRAMU** ........ **56**

ZANA 3.1 Mwongozo wa Kuandika Pendekezo la Mradi ........ 56

ZANA 3.2 Ujumuishaji wa GESI kwenye Usanifu wa Programu ........ 59

ZANA 3.3 Viashiria vya GESI ........ 66

ZANA 3.4 Mpango Kazi wa Ujumuishaji wa GESI ........ 70

ZANA 3.5 Uandaaji wa Bajeti yenye Muitikio wa GESI ........ 73

**SEHEMU 4 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA PROGRAMU** ........ **78**

ZANA 4.1 Ujumuishaji wa GESI kwenye Ufuatiliaji wa Programu ........ 79

ZANA 4.2 Tathmini ya Programu yenye Muitikio wa GESI ........ 81

ZANA 4.3 Kuchanganua na Kuripoti Data kwa Muitikio wa GESI ........ 84

Uchanganuzi wa GESI wa Data za Kitakwimu ........ 85

Uchanganuzi wa GESI wa data za Kitaamuli ........ 90

Kuwasilisha na Kuripoti Matokeo ya GESI ........ 92

KIAMBATANISHO 1 **Faharasa ya Dhana za GESI** ........ **94**

KIAMBATANISHO 2 **Vielelezo vya Viashiria vya GESI** ........ **96**

KIAMBATANISHO 3 **Mfano wa Zana ya Uhakiki wa Ubora wa Miundo Inayofaa Watu Wote Katika Utoaji Huduma** **105**

**MAREJELEO** ........ **108**

## MAJEDWALI


Jedwali 1 Orodha ya Ujumuishaji wa GESI . . . 9
Jedwali 2 Orodha ya Tathmini ya Mtu Mmoja Mmoja yenye Muitikio wa GESI . . . 13
Jedwali 3 Mfano wa Zana ya Uchanganuzi wa Kitakwimu wa Tathmini ya Tafakuri . . . 15
Jedwali 4 Tafakuri ya Pamoja . . . 22
Jedwali 5 Mapitio ya Maandiko ya Data za GESI . . . 23
Jedwali 6 Zana ya Matriki Sanisi . . . 26
Jedwali 7 Maelezo Mafupi Kuhusu Nchi . . . 28
Jedwali 8 Maswali ya Mwongozo ya Ukusanyaji wa Data za Upili . . . 30
Jedwali 9 Data za Upili Kuhusu Ustawi . . . 31
Jedwali 10 Muhtasari wa Data Zilizopo Kuhusu Desturi za Kijinsia na Jamii Kutoka kwenye Tafiti Kubwa za Kaya . . . 32
Jedwali 11 Mipango ya Ukusanyaji wa Data zenye Muitikio wa GESI . . . 33
Jedwali 12 Viwango vya Mazingira Hatarishi . . . 37
Jedwali 13 Ramani ya Kijamii . . . 41
Jedwali 14 Chati ya Shughuli za Kila Siku . . . 44
Jedwali 15A Tathmini ya Desturi za Kijinsia na Kijamii . . . 46
Jedwali 15B Mifano ya Maswali Kusaidia Uelewa wa Vikwazo Vinavyohusiana na Desturi za Kijamii . . . 48
Jedwali 16 Tafiti za Kaya Kuhusu Ufanyaji Maamuzi . . . 51
Jedwali 17 Tafiti za Kaya Kuhusu Ushiriki . . . 53
Jedwali 18 Tafiti za Kaya Kuhusu Ustawi . . . 54
Jedwali 19 Orodha ya Mapitio ya GESI Kuhusu Ubora wa Pendekezo la Mradi . . . 56
Jedwali 20 Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Madhumuni, Malengo, na Matokeo ya Programu . . . 61
Jedwali 21 Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Shughuli . . . 63
Jedwali 22 Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Mkakati wa Kudhibiti Athari . . . 64
Jedwali 23 Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini . . . 65
Jedwali 24 Viashiria vya GESI vya Shirika la World Vision kwa Sekta ya Programu, Kikoa cha GESI, na Kiwango cha Matokeo . . . 69
Jedwali 25 Mpango Kazi wa Ujumuishaji wa GESI . . . 73
Jedwali 26 Kutengeneza Bajeti yenye Muitiko wa GESI . . . 74
Jedwali 27 Uandaaji wa Hadidu za Rejea na Kusanifu Tathmini . . . 82
Jedwali 28 Uandaaji wa Ripoti za Tathmini za Programu wenye Muitikio wa GESI . . . 83
Jedwali 29 Mfano wa Jedwali la Mzunguko la GESI . . . 86
Jedwali 30 Mfano wa Kuelezea Matokeo yenye Kuonyesha GESI . . . 87
Jedwali 31 Mfano wa Jedwali la GESI Linaloonyesha Mzunguko wa Data Zilizokusanywa kwa Mfululizo wa Muda . . . 87
Jedwali 32 Mfano wa Matokeo ya GESI ya Jaribio la T . . . 89
Jedwali 33 Mfano wa Data Zilizosimbwa . . . 91
Jedwali 34 Orodha ya Kuwasilisha na Kuripoti Matokeo ya GESI . . . 92
Jedwali 35 Viashiria Vinavyotumika Sehemu Nyingi/Mtambuka kwa Sekta Zote . . . 96
Jedwali 36 Viashiria vya Afya . . . 97
Jedwali 37 Viashiria vya Usalama wa Chakula na Shughuli za Kujipatia Riziki . . . 98
Jedwali 38 Viashiria vya Ulinzi wa Mtoto na Elimu . . . 100
Jedwali 39 Viashiria vya Msaada wa Kibinadamu na Dharura . . . 101
Jedwali 40 Viashiria vya Maji, Usafi wa Kimwili na Usafi wa Mazingira . . . 102
Jedwali 41 Viashiria vya Uwezeshaji Kiuchumi . . . 103


## VIELELEZO


Kielelezo 1 Muundo wa Kijitabu cha GESI cha Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini . . . 3
Kielelezo 2 Hatua za Kutumia Lenzi ya GESI . . . 5
Kielelezo 3 Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya Shirika la World Vision . . . 6
Kielelezo 4 Vikoa Vitano vya GESI vya Shirika la World Vision . . . 7
Kielelezo 5 Athari Zinazoweza Kusababishwa na Shughuli za Programu . . . 63
Kielelezo 6 Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Kuchagua Viashiria . . . 67
Kielelezo 7 Hatua za Uchanganuzi wa GESI kwenye Data za Kitakwimu . . . 85
Kielelezo 8 Mfano wa Grafu ya Mhimili wa GESI . . . 86
Kielelezo 9 Hatua za Uchanganuzi wa GESI kwenye Data za Kitaamuli . . . 90



## KUHUSU KIJITABU

Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii (kwa lugha ya kiingereza ni *Gender Equality and Social Inclusion* au kwa kifupi "GESI") ni muhimu katika kufikia malengo makuu endelevu ya kidunia na mkakati wa shirika la World Vision wenye malengo ya kuboresha ustawi wa mtoto.[1] GESI inaendeleza kanuni za muhimu za mabadiliko ya mwanadamu kwa kuwafikia watoto na watu wazima walio katika mazingira hatarishi zaidi na kuhoji sababu za kina zinazowafanya wawe katika mazingira hatarishi ambazo zinachochea kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kama vile desturi kandamizi za kijamii na kitamaduni, mahusiano ya kimamlaka yasiyo na usawa na mifumo kandamizi. Kuhimiza GESI ni jambo la muhimu katika kutimiza maagizo ya wafadhili ya kushughulikia mahitaji ya watoto na watu wazima walio katika mazingira hatarishi zaidi na kutimiza ahadi na mkakati wa kutengeneza mabadiliko endelevu.

Shirika la World Vision lina wajibu wa kukusanya na kuwasilisha tarifa za ufanisi wa kazi yetu ya kuendeleza ustawi wa watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi, familia zao, na jamii kama ilivyoagizwa kwenye vipaumbele vya taasisi. Mchakato wa kukusanya tarifa za mchango unaohusiana na GESI si kitu rahisi, maana unahitaji zana na ujuzi maalumu ili kuelewa uchangamani wa mikabala ya maendeleo ya mabadiliko.

### MADHUMUNI YA KIJITABU

Kijitabu hiki kimesanifiwa ili kutoa mwongozo na zana za kuwasaidia wafanyakazi kujumuisha mitazamo ya GESI kwenye hatua zote za usanifu,ufuatiliaji na tathmini ya mradi. Lengo ni kuboresha ufanisi, matokeo na uendelevu wa kazi ya shirika la World Vision kwa mtazamo wa GESI. Kijitabu hiki kina mwongozo halisi ili kuwasaidia wafanyakazi kwenda sambamba na programu za misaada na maendeleo kwa ujumuishaji wa viwango vya kimataifa vya GESI na mienendo mizuri. Kijitabu kimejikita katika mapitio ya zana na mikabala ya usanifu, ufuatiliaji na tathmini iliyopo kwa sasa. Zana zilizowekwa humu si zote, na watumiaji wanahimizwa kutafuta vyanzo vingine vya zana, baadhi ya vyanzo hivyo vyaweza kukamilisha matumizi ya zana zilizowasilishwa kwenye kijitabu hiki.

### NANI ANAWEZA KUTUMIA KIJITABU HIKI

Kijitabu hiki kinafaa kutumiwa na watumiaji wa aina mbalimbali kwenye nyanja za maendeleo ya kimataifa. Hususani, zana zimeundwa kwa ajili ya timu za miradi zilizoko kwenye sekta mbalimbali ikiwemo uandishi wa mapendekezo/biashara, ufuatiliaji, tathmini na utafiti; menejimenti ya programu na GESI. Kijitabu hiki kinaweza kuwa rasilimali muhimu kwa ajili ya wabia wa utekelezaji na wabia wa serikali, wakiwa wanashirikiana kwenye malengo ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Mtu mmojammoja na mashirika wote wanaweza kutumia kijitabu hiki kwa ajili ya kutumia lenzi ya GESI kwenye hatua zote za usanifu, ufuatiliaji na tathmini ya mradi.

### MUUNDO WA KIJITABU

Kijitabu kimegawanywa kwenye sehemu nne na kinahusisha kiambatanisho chenye faharasa ya dhana za GESI, na Vielelezo vya viashiria kwa ajili ya sekta mbalimbali. Pia, kinajumuisha marejeleo. Sehemu hizo nne ni pamoja na zana zilizorodheshwa kwenye Kielelezo 1.



1 Global Child Well-being Framework and Strategic Initiatives on Utilizing Evidence of Impact

**Kielelezo 1 | Muundo wa Kijitabu cha GESI cha Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini**

# Muundo wa Kijitabu cha GESI cha Usanifu, Ufuatiliaji na Tathmini

## Sehemu 1 KUTAMBULISHA LENZI YA GESI

| | |
|---|---|
| **ZANA 1.1** | Jinsi ya Kutumia Lenzi ya GESI |
| **ZANA 1.2** | Viwango vya Chini vya GESI |
| **ZANA 1.3** | Orodha ya Tafakuri |

## Sehemu 2 JINSI YA KUFANYA UCHANGANUZI WA GESI

| | |
|---|---|
| **ZANA 2.1** | Uchanganuzi wa GESI |
| | Hatua 1 Tafakuri ya Pamoja |
| | Hatua 2 Mapitio ya Maandiko na Ukusanyaji wa Data za Upili wenye Muitikio wa GESI |
| | Hatua 3 Ukusanyaji wa Data za Msingi wenye Muitikio wa GESI |
| | Hatua 4 Uchanganuzi wa Data na Uandishi wa Ripoti wenye Muitikio wa GESI |

## Sehemu 3 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE USANIFU WA PROGRAMU

| | |
|---|---|
| **ZANA 3.1** | Mwongozo wa Kuandika Pendekezo la Mradi |
| **ZANA 3.2** | Ujumuishaji wa GESI kwenye Usanifu wa Programu |
| **ZANA 3.3** | Viashiria vya GESI |
| **ZANA 3.4** | Mpango Kazi wa Ujumuishaji wa GESI |
| **ZANA 3.5** | Uandaaji wa Bajeti yenye Muitikio wa GESI |

## Sehemu 4 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA PROGRAMU

| | |
|---|---|
| **ZANA 4.1** | Ujumuishaji wa GESI kwenye Ufuatiliaji wa Programu |
| **ZANA 4.2** | Tathmini ya Programu yenye Muitikio wa GESI |
| **ZANA 4.3** | Kuchanganua na Kuripoti Data kwa Muitikio wa GESI |

# Sehemu 1
# Kutambulisha Lenzi ya GESI

Sehemu hii inaelezea dhana ya Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii na inaitambulisha lenzi ambayo unaweza kuitumia wakati wote wa kipindi cha mradi. Dehemu hii ina zana tatu:

| | |
|---|---|
| **ZANA 1.1** | Jinsi ya Kutumia Lenzi ya GESI |
| **ZANA 1.2** | Viwango vya Chini vya GESI |
| **ZANA 1.3** | Orodha ya Tafakuri |

## ZANA 1.1 JINSI YA KUTUMIA LENZI YA GESI

Zana hii inafasili GESI na inaelezea zana nne muhimu katika kutumia lenzi ya GESI kwenye mchakato wa usanifu,ufuatliaji na tathmini ya mradi.

### KUFASILI GESI

**Usawa wa Kijinsia** ni hali inayowawezesha wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, kufurahia kwa usawa haki za kibinadamu, mambo yanayothaminiwa na jamii, fursa, na rasilimali. Hii inajumuisha kuongeza uhuru na kuwa na sauti, kuboresha mienendo ya mamlaka na mahusiano, kubadilisha majukumu ya kijinsia na kuimarisha kiwango cha maisha kwa ujumla ili wanaume na wanawake waweze kutumia uwezo walionao kufanikisha malengo yao.[2]

**Ushirikishaji wa Kijamii** hushughulikia ukosefu wa usawa na/au uhusishaji kwa watu walio katika mazingira hatarishi kwa kutengeneza mazingira ya ushiriki katika jamii kwa kuboresha fursa, upataji na ufikiaji wa rasilimali, kuwa na sauti na kuheshimu haki za binadamu. Inakusudia kuhimiza uwezeshaji na kuendeleza jamii na taasisi zenye amani.[3]

Shirika la World Vision linafasili GESI kama mchakato changamani wa mabadiliko[4] ambao:

- Huhimiza usawa katika upataji na ufikiaji , ufanyaji maamuzi, ushiriki na ustawi wa watu walioko katika mazingira hatarishi zaidi
- Hubadilisha mifumo, desturi za kijamii, na mahusiano ili kuwawezesha watu walio katika mazingira hatarishi zaidi kushiriki na kufaidika kwa usawa katika afua za maendeleo
- Hujenga uwezo wa kufanya mambo kwa mtu mmojammoja na kwa watu pamoja, uthabiti na matendo
- Huhimiza uwezeshaji na ustawi wa watoto walio katika mazingira hatarishi, familia na jamii zao

**Lengo letu ni kufikia maendeleo endelevu kwenye ngazi ya mtu mmoja mmoja, kaya, jamii na jumuiya ili watu wote wafurahie maisha kwenye ukamilifu wake.**

GESI inafanikisha misingi ya World Vision ya kuhamasisha mabadiliko katika maisha ya watu kwa kuwafikia watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi na kuhoji sababu za kina zinazosababisha mazingira hatarishi ambazo zinaendeleza ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.

2 See UN Women; USAID Gender Equality and Female Empowerment Policy; and Kabeer (2005) on empowerment.
3 Adapted from United Nations Sustainable Development Goals (SDGs), particularly SDG# 5, 8, 10, 11 and 16 which emphasize equality and inclusion.
4 See World Vision GESI approach and TOC; adapted form United Nations Sustainable Development Goals (SDGs).

## HATUA NNE ZA KUTUMIA LENZI YA GESI

Kuna hatua nne za kutumia lenzi ya GESI kama zinavyoelezewa kwenye Kielelezo 2 hapa chini, kila hatua ina swali muhimu unalotakiwa kulijibu:

**Kielelezo 2 | Hatua za Kutumia Lenzi ya GESI**

| Hatua ya 1 | Hatua ya 2 | Hatua ya 3 | Hatua ya 4 |
|---|---|---|---|
| **Malengo ya GESI** | **Kulenga GESI** | **Nadharia ya Mabadiliko ya GESI** | **Viashiria vya GESI** |
| Je, mradi wako unabainishaje malengo ya GESI na malengo ya mkakati wa shirika? | Je, mradi wako unabainishaje na kuwalenga watu walio katika mazingira hatarishi? | Je, mradi wako unajumuishaje Nadharia ya Mabadiliko ya shirika la World Vision? | Je, mradi wako ulibainisha viashiria gani vya GESI ili kushughulikia vikoa vitano vya GESI? |

## Hatua ya 1 | Jumuisha malengo yanayohusiana na GESI kwenye mradi

Kama inavyoelezewa kwenye ZANA 1.1 hapo juu. Usawa wa Kijinsia na Uhusishaji wa Kijamii (GESI) ni muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya mabadiliko kama shirika. Wafanyakazi wa shirika la World Vision wanapaswa kubainisha namna ambavyo kila mradi unaweza kufanikisha malengo ya shirika yanayohusiana na GESI ambayo yamewekwa kwenye mkakati mkuu na malengo ya kuboresha ustawi wa mtoto.[5]

### Ni kwa namna gani mradi wako umejumuisha malengo yanayohusiana na GESI?

## Hatua ya 2 | Lenga walio katika mazingira hatarishi

Ni muhimu kutumia lenzi ya GESI kufasili watu walio katika mazingira hatarishi zaidi katika muktadha wa mradi na kubaini taasisi au michakato ambayo inasababisha na kuunga mkono kukosekana kwa usawa na uhusishaji.Ushahidi unaonyesha kwamba kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji katika jamii kuna athari za viwango tofauti tofauti kwa watoto - wasichana na wavulana, wanawake, watu wenye ulemavu, vijana, na watu wanaoishi katika umasikini. Sababu zingine za kuwa katika mazingira hatarishi au kutengwa ni pamoja na hadhi ya uhamiaji, kabila, dini, umri, lugha na hali ya kiafya. Watu wana udhaifu unaoingiliana na unaohusiana - unaojulikana kama uchangamani. Kwa mfano, wanawake wenye ulemavu wanaweza kukabiliwa na ukandamizaji mara mbili kwa sababu ya desturi za kijinsia, mawazo yaliyojengeka kuhusu jambo na unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu.Wavulana/vijana wadogo wa rika balehe wanaoishi katika umasikini uliokithiri wanaweza kuathiriwa na hatari kubwa za ukatili ndani ya jamii kwa sababu ya umri na hali ya kijamii na kiuchumi.

5 Refer to World Vision's Global Impact Framework and Strategic Initiative 2.2 on utilizing evidence of impact.




Kwa mfano shirika la World Vision linawatambua watoto walio katika mazingira hatarishi kuwa ni wale walio chini ya umri wa miaka 18 ambao wanaoishi na mambo mawili au zaidi kati ya haya yafuatayon[6]

- Wako katika mahusiano ya kunyanyaswa, ukatili au unyonyaji
- Wanaishi katika umaskini uliokithiri na ufukara
- Wanakabiliwa na ubaguzi mkubwa ambao unawazuia kupata na kufikia huduma na fursa
- Wako kwenye hatari kubwa ya kukabiliwa na athari hasi za maafa au majanga
- Wana ulemavu au ugonjwa unaohatarisha maisha yao (kama HIV/AIDS)
- Ukosefu wa huduma na ulinzi/usalama

## Ni kwa namna gani mradi wako unawabaini na kuwalenga watu walio katika mazingira hatarishi zaidi na kushughulikia muingiliano wa sababu za kuwa katika mazingira hatarishi?

## Hatua 3 | Jumuisha Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya Shirika la World Vision

Madhumuni ya Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision ni kujenga uelewa wa pamoja wa mabadiliko yanayotakiwa kufanyika ili kufikia usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii na kuhamasishana kuongoza ujumuishaji wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii wenye mpangilio mzuri ndani na kati ya sekta za programu. Hivyo basi, ni muhimu Nadharia ya Mabadiliko kama ilivyoelezewa kwenye Kielelezo 3 kujumuishwa kwenye afua za mradi na nadharia za mabadiliko.

**KIELELEZO 3 | Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya Shirika la World Vision**




6 World Vision Global Guidance on estimating the number of vulnerable children; WVUS GESI Approach and TOC, 2020.

Mkabala na Nadharia yetu ya Mabadiliko ya GESI inaonyesha vikoa vitano vya mabadiliko ya GESI ambavyo vinatakiwa viwe na ufanisi katika ngazi zote kuanzia ngazi ya mtu mmoja mmoja hadi ngazi ya jumuiya. Vikoa hivi vinafasiliwa zaidi kwenye Kielelezo 4.

Ili kujumuisha nadharia ya mabadiliko kwenye programu yako unatakiwa utumie vikoa vitano kuuliza:

1. Je, umeelewa vikwazo vinavyoyapata makundi yaliyo katika mazingira hatarishi katika kila kikoa, na kila ngazi ambayo wanakumbana na vikwazo? Vikwazo vyaweza kuwa kwenye sekta mbalimbali (afya, elimu, ulinzi wa mtoto, maji na usafi, usalama wa chakula na riziki, na huduma ya dharura).
2. Je, umebaini hatua muhimu zinazohusiana na vikoa vya GESI ili kubadili hali iliyopo? na je, hatua hizo zinatakiwa kuchukuliwa kwa kiwango gani?

**KIELELEZO 4 | Vikoa Vitano vya GESI vya Shirika la World Vision**

UPATAJI NA UFIKIAJI

Uwezo wa kupata na kufikia, kutumia, kudhibiti, na/au kumiliki mali, rasilimali, fursa, huduma, faida na miundombinu.




UFANYAJI MAAMUZI

Uwezo wa kufanya maamuzi kwa hiari kwenye ngazi ya mtu mmojammoja, familia, jamii na jumuiya. Hii inajumuisha uwezo wa kufanya maamuzi juu ya mali na maamuzi kwenye uongozi.

USHIRIKI

Uwezo wa kushiriki na kujihusisha kwenye masuala ya jumuiya na mifumo ya mamlaka ambayo yanashawishi na kuamua kuhusu maendeleo, shughuli za maisha na matokeo.

MIFUMO

Uwepo wa mifumo yenye usawa na jumuishi ambayo inahimiza uwiano, inayoshughulikia mahitaji mbalimbali ya makundi ya watu walio kwenye mazingira hatarishi na kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya uhusishwaji wao.

USTAWI

Hali ya kuwa na thamani, uwezo, kujiamini, heshima, usalama, afya, na ustawi wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, na kiroho kwa ujumla. Hii ni pamoja na kuishi bila ukatili wa kijinsia, na aina zote za unyanyapaa na ubaguzi.

## Ni kwa namna gani mradi wako unajumuisha Nadharia ya Mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision?

## Hatua 4 | Bainisha viashiria kulingana na vikoa vitano vya GESI

Vikoa vitano vya mabadiliko ya GESI ni muhimu katika kufikia kwa viwango vya juu usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kwenye kazi zetu. Maswali yafuatayo yanaweza kukusaidia kuangalia viashiria vyenye muitikio wa GESI ambavyo vinaendana na nadharia ya mabadiliko ya GESI ya shirika la World Vision's GESI na vikoa vyake vitano.

- Je, viashiria vyako ni rahisi? vinapimika? vinafikika? ni halisi? na vinazingatia muda?
- Je, ni kwa namna gani afua zako, shughuli, na muda uliojipangia kumaliza shughuli unatatua changamoto zozote zilizobainishwa kwenye vikoa vitano vya GESI?
- Je, ni kwa namna gani utatathmini kama mradi wako umefanikiwa kumetimiza kile ambacho ulisema utafanya?

Ni muhimu kuonyesha namna ambavyo mradi wako utashughulikia vikoa vyote vya GESI ili kuhakikisha kuwa programu zetu zina muitikio wa GESI. Muitikio wa GESI unamaanisha kuelewa na kuzingatia tofauti za mahitaji, fursa na uzoefu wa wanawake,wanaume,wasichana,wavulana,watu wenye ulemavu, wahamiaji wa ndani na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi na kurekebisha malengo, shughuli, mikakati na mienendo kwa namna inayowezesha kujumuisha mahitaji hayo,fursa na uzoefu kwenye programu zetu.Lengo ni kufikia mabadiliko endelevu ndani ya mfumo wa kiikolojia kwa kuzingatia vikwazo vya kijinsia na uhusishaji wa kijamii na/au fursa za mfumo wa kiikolojia kwenye ngazi za mtu binafsi,kaya, jamii na jumuiya.

Mwongozo zaidi kuhusu viashiria vya GESI unaweza kupatikana kwenye ZANA 3.3 na maelezo ya viashiria maalumu vya GESI vimeorodheshwa kwenye Kiambatanisho 2.

**Je, mradi wako umebainisha viashiria vipi ili kutathmini maendeleo kwenye vikoa 5 vya GESI?**

## ZANA 1.2 VIWANGO VYA CHINI VYA GESI

Zana hii inatoa orodha kwa taasisi kuweza kutathmini namna zinavyo kushughulikia masuala ya GESI ndani ya programu zao na taasisi kwa ujumla. Kushughulikia masuala ya GESI kupitia programu peke yake haitoshi. Zana hii inasaidia taasisi kutathimini maeneo tisa ambayo ni viwango vya chini kabisa kwa ajili ya kufanikisha maendeleo na misaada yenye usawa na uhusishaji. Orodha inazungumzia masuala ya sera, uwezo na mila, ushiriki na ushirikiano, bajeti, uchanganuzi, ukusanyaji data, viashiria, "usidhuru" na uwajibikaji. Kila suala lina maelezo ambayo ndio kiwango cha chini .[7] Orodha iliyoandikwa kwenye Jedwali 1 inaweza kutumika kama zana ya ufuatiliaji kwa ajili ya kutathmini maendeleo ya shirika. Wafanyakazi wa World Vision wanaweza kutumia orodha hii kuamua kama kiwango kimefikiwa kikamilifu, kwa kiasi fulani, au hakijafikiwa kabisa kama inavyoonyeshwa kwenye safu wima ya mafanikio na mapendekezo.

7 The nine categories of minimum standards have been adapted from a document created by the Gender Practitioners' Collaborative (2017), to include broader social inclusion standards

**Jedwali 1 | Orodha ya Ujumuishaji wa GESI**

| VIWANGO NA SIFA | 1= Ndiyo<br>2= Kwa kiasi fulani<br>3= Hapana | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Kiwango 1: Pitisha sera za GESI mahali pa kazi kwa njia husishi** | | |
| 1.1 Sera ya kimataifa ya GESI ( kwa maandishi na muundo utakaowafikia wengi) zimetengenezwa, zimesambazwa, na kutumiwa katika ofisi zote za makao makuu, nchi, na kanda. | | |
| 1.2 Sera na taratibu zinahakikisha mazingira ya kazi yana usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, pamoja na sera za kupinga unyanyasaji na ubaguzi, likizo ya uzazi kwa wanawake na wanaume, mazingira mazuri ya kufanyia kazi, utoaji wa mahitaji ya muhimu na sehemu za kunyonyeshea watoto. | | |
| 1.3 Sera za rasilimali watu kwa ajili ya shughuli za kuajiri zinajumuisha será zisizobagua na zinazozingatia kuwepo kwa watu wa aina mbalimbali. | | |
| 1.4 Sera imewekwa ili kulinda walengwa wa programu dhidi ya unyonyaji wa kijinsia na unyanyasaji unaofanywa na wafanyakazi na wenzi. | | |
| 1.5 Wafanyakazi wa shirika la World Vision wanajulishwa juu ya sera za GESI za shirika la World Vision na sera zinazohusiana na rasilimali watu wakati wa mafunzo ya wafanyakazi wapya. | | |
| **Kiwango 2: Jenga utamaduni wa shirika na uwezo wa GESI** | | |
| 2.1. Uongozi wa ngazi ya juu unachukua jukumu la kuongoza na kutekeleza sera za programu na GESI, inadhihirika katika mikutano ya wafanyakazi, mafunzo ya wafanyakazi wapya, ufuataji sera za utumishi, na kuunga mkono taratibu za GESI za usanifu, ufuatiliaji na tathmini kwenye mzunguko wa programu. | | |
| 2.2. Wafanyakazi wa shirika la World Vision wameshiriki angalau mara moja katika mafunzo ya GESI yaliyoandaliwa au kuongozwa na Washauri wa Jinsia wa shirika la World Vision na/au Washauri wa Ujusishaji wa Kijamii kila baada ya miaka 2. | | |
| 2.3. Shughuli na majukumu yanayohusiana na GESI zimebainishwa kwenye majukumu ya kazi, uendelezaji wa taaluma, na tathmini ya utendaji kazi. | | |
| 2.4. Wafanyakazi wa shirika la World Vision wanawajua wawakilishi wa GESI katika sekta mbalimbali, mtaalamu, au mshauri ambaye wanaweza kumuomba msaada wa kitaalamu. | | |
| 2.5. Wafanyakazi wa mradi wana uzoefu na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya programu inayojumuisha masuala ya kijinsia na uhusishaji. | | |
| 2.6. Kuna uwiano unaofaa miongoni mwa wafanyakazi wa mradi kwa kigezo cha jinsia katika ngazi zote, hasa kwa wafanyakazi wenza wa shirika la World Vision walio kwenye maeneo ya mradi. | | |
| 2.7. Watu wenye ulemavu, na wale walio kwenye makundi yanayokandamizwa hufanya kazi kwenye shirika la World Vision na wabia wake. | | |
| **Kiwango 3: Hakikisha ushiriki na ubia wenye muitikio wa GESI** | | |
| 3.1. Wabia na wadau wa programu wanaohusika wanajua, na wanaufahamu wa kutosha juu ya sera za GESI za shirika la World Vision. | | |
| 3.2. Wabia wa programu huchaguliwa na kuchunguzwa kwa kuzingatia sera zao za GESI na utofauti wa wafanyakazi wao na uwezo wao kuendesha mradi na makundi yote. | | |
| 3.3. Washiriki wa programu wanahusishwa katika muundo na shughuli za programu kulingana na mahitaji yao maalumu, mahitaji ya usalama, na tofauti za kitamaduni. | | |
| 3.4. Washiriki wa programu wana usawa katika fursa, kupata na kufikia mafunzo, shughuli, na fursa zingine ambazo shirika la World Vision hutoa, bila kujali jinsia yao, hali ya ulemavu, umri au sifa nyingine za kijamii. | | |

| VIWANGO NA SIFA | 1= Ndiyo<br>2= Kwa kiasi fulani<br>3= Hapana | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Kiwango 4: Tenga rasilimali kwa ajili ya GESI** | | |
| 4.1 Shughuli za upangaji mkakati wa mwaka na michakato ya bajeti zinazingatia gharama za GESI katika kila mwaka wa fedha na mzunguko wa programu. | | |
| 4.2 Bajeti ya pendekezo la mradi inajumuisha bajeti ya kufanikisha matokeo yanayohusiana na GESI kwenye programu na mfuko wa uhusishaji ili kulipia gharama za ujumuishaji ikiwa ni pamoja na lugha ya ishara, mawasiliano kwa wote, usafiri kwa kila mlemavu, utoaji wa vifaa kwa walemavu, n.k. | | |
| 4.3. Mambo yanayohusiana na bajeti ya GESI ni pamoja na wafanyakazi wa GESI, kujenga uwezo/mafunzo, tathmini za GESI, na gharama za ziada kuhakikisha usalama na kujali tofauti za kitamaduni za watu na makundi mbalimbali. | | |
| **Kiwango 5: Fanya na tumia tathmini za GESI** | | |
| 5.1 Tathmini ya GESI inafanywa wakati wa usanifu na kujumuishwa katika pendekezo la mradi. | | |
| 5.2 Tathmini ya GESI inaruhusu kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali, pamoja na washiriki muhimu wa programu (makundi yote ya kjinsia na kijamii yanawakilishwa), viongozi wa jamii, na wawakilishi wa serikali za mitaa (kama vile muda na eneo la mahojiano/majadiliano ya kikundi ni rahisi kufika na salama kwa wote, hasa ikiwa mada inayozungumziwa ni nyeti). | | |
| 5.3 Tathmini ya GESI hutumia mbinu shirikishi, zinazoruhusu watu binafsi na vikundi kuchangia kwa kina. | | |
| 5.4 Matokeo ya tathmini za GESI hutumiwa kuandaa mipango kazi ya programu, shughuli, bajeti, na michakato ya ufuatiliaji na tathmini. | | |
| 5.5 Tathmini inapima mambo yafuatayo: | | |
| a. Wajibu na majukumu kwenye kaya na jamii, pamoja na kazi za uzalishaji, majukumu ya uzazi na uhuru wa kutembea. | | |
| b. Upataji na ufikiaji na uwezo wa kudhibiti mali, rasilimali na fursa, na vikwazo katika kutafuta huduma. | | |
| c. Ufanyaji maamuzi na uhusiano wa kimamlaka katika ngazi ya kaya, jamii, mkoa na/au taifa. | | |
| d. Mahitaji, vipaumbele, na mitazamo, pamoja na mahitaji halisi na maslahi ya kimkakati ya makundi mbalimbali na maoni yao juu ya njia sahihi na endelevu za kushughulikia mahitaji. | | |
| e. Ushiriki na uongozi katika shughuli za kijamii na ushirika, maoni ya viongozi juu ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii, njia za mawasiliano zinazopendelewa na vizuizi kwa uongozi wa wanawake. | | |
| f. Maarifa, imani za kitamaduni na mitazamo ikiwa ni pamoja na upataji na ufikiaji wa maarifa na mitazamo ya kijamii, kidini na kitamaduni na desturi ambazo zinaathiri wanawake, wanaume, wavulana na wasichana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyotengwa kwa namna tofauti. | | |
| g. Mfumo wa kisheria, sheria au vizuizi vingine vinavyozuia wanawake na wanaume, wavulana na wasichana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyotengwa kuwa na fursa sawa. | | |

| VIWANGO NA SIFA | 1= Ndiyo<br>2= Kwa kiasi fulani<br>3= Hapana | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Kiwango 6: Kusanya na changanua data ziliyogawanywa kulingana na jinsi, ulemavu na sifa nyingine za kijamii** | | |
| 6.1 Tathmini ya GESI hukusanya data iliyogawanywa kwa sifa za jinsi, umri, na sifa zingine muhimu za kijamii (hali ya ulemavu, hali ya uchumi, ushirika wa kidini, kabila, rangi, n.k) kutathmini tofauti na vikwazo vya makundi mbalimbali. | | |
| 6.2 Tahmini ya msingi, kati, na ya mwisho, au tathmini za programu hukusanya data iliyogawanywa kwa jinsi, umri, na sifa nyingine muhimu za kijamii (umri, ulemavu, hali ya uchumi, ushirika wa kidini, kabila, rangi, n.k.). | | |
| 6.3 Mbinu na michakato ya ukusanyaji wa data inachukua hatua kuhakikisha usalama, ulinzi, upatikanaji na tofauti za kitamaduni za makundi mbalimbali ya kijamii. | | |
| 6.4 Tathmini na ripoti za programu zinaonyesha faida au athari za programu kwenye makundi mbalimbali ya kijamii. | | |
| **Kiwango 7: Tumia viashiria vya GESI** | | |
| 7.1. Matokeo ya tathmini ya GESI yanasaidia katika uchaguzi wa vielelezo mtambuka na maalumu kwa sekta husika. | | |
| 7.2. Viashiria vya GESI vilivyochaguliwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa programu na michakato ya tathmini vimegawanywa kwa mujibu wa vikoa vitano vya GESI vya shirika la World Vision: upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, mifumo, na ustawi (yaani kuna angalau kikoa kimoja, pale inapowezekana). | | |
| 7.3. Viashiria maalumu vya GESI kwenye sekta hupimwa katika programu zote. | | |
| 7.4. Viashiria vya kitakwimu na kitaamuli vinatumika kukusanya uzoefu mbalimbali, imani, maoni na ukweli. | | |
| **Kiwango 8: Usidhuru** | | |
| 8.1 Tathmini ya athari hufanywa kabla na wakati wa programu ili kuelewa na kushughulikia athari zozote ambazo programu inaweza kusababisha kwa baadhi ya makundi ya kijamii. | | |
| 8.2 Mpango au mkakati wa upunguzaji, ufuatiliaji na kukabiliana na athari uliobainishwa na madhara mengine yasiyokusudiwa hubainishwa na kushughulikiwa mara kwa mara katika mzunguko wote wa programu. (kama vile muitikio hasi kwa wafanyakazi wa programu au kutengwa kiuchumi) | | |
| 8.3. Mifumo imewekwa kwa wafanyakazi na wanajamii kuweza kuwasilisha kwa usalama hali ya hatari au madhara, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia, na changamoto zinazohusiana na ulemavu. | | |
| **Kiwango 9: Uwajibikaji** | | |
| 9.1 Ofisi za makao makuu na ofisi za nchi zimekamilisha ukaguzi wa mahesabu ya GESI au tathmini ya shirika ili kupima uwezo wa ndani na maendeleo kuelekea kwenye matokeo ya GESI. | | |
| 9.2 Matokeo ya tathmini ya GESI yanasambazwa kwa wafanyakazi wa programu, wabia, na wadau wa kijamii. | | |
| 9.3. Shirika la World Vision lilianzisha utaratibu wa uwajibikaji ili kufuatilia hali ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii katika shuguli za shirika na programu. | | |

# ZANA 1.3 TAFAKURI YA MTU MMOJA MMOJA

Kushughulikia kwa ufanisi masuala ya kukosekana kwa usawa na uhusishaji wa kijamii kwenye programu kunahitaji imani binafsi za wafanyakazi na utamaduni wa shirika la World Vision kupinga ubaguzi. Kuongeza uelewa wa mtu mmoja mmoja na wa taasisi kuhusu GESI ni hatua muhimu katika kujumuisha GESI katika usanifu,ufuatiliaji na tathmini.

Zana ya tafakuri ya mtu mmoja mmoja inaweza kuwasaidia wafanyakazi wa shirika la World Vision kufikiria miegemeo yao, upendeleo na vikwazo vya kufikia GESI. Zana hii ni kwa ajili ya mtu mmoja mmoja kujitathimini uwezo wake wa kushughulikia ukosefu wa usawa na uhusishaji wa kijamii.[8]

## LENGO

Zana hii imeundwa ili kuchochea mjadala baina ya timu ya wafanyakazi na ofisi wanapokuwa wanajishughulisha na kazi zinazohusiana na GESI kwenye usanifu,ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza ufahamu kuhusu malengo ya GESI ya shirika la World Vision, na kusaidia kubaini mambo yanayoweza kuhitajika kwa ajili ya kuendeleza juhudi za GESI ambazo zitazungumziwa kwenye sehemu iliyobaki ya kijitabu hiki. Zana ya Tafakuri ya Mtu Mmoja Mmoja inaweza kutumika pamoja na ZANA 1.2. Zana ya Viwango vya Chini vya GESI .

Zana ya Viwango vya Chini vya GESI inaweza kutumika kama zana ya tafakuri ya taasisi. Orodha ya Tafakuri ya Mtu Mmoja Mmoja na Viwango vya Chini vya GESI (vinapotumika kama orodha muhimu kwenye taasisi) vinatumika:

- Kuwawezesha wafanyakazi wa shirika la World Vision kufanya tathmini ya uwezo wao binafsi na uwezo wa taasisi kushughulikia GESI
- Kutathmini uwezo na utendaji wa shirika la World Vision katika kuhimiza GESI
- Kupitia mifumo ya ndani ya shirika la World Vision katika kushughulikia GESI
- Kutengeneza mpango wa ujifunzaji na mpango wa maendeleo kwa ajili ya mradi

Tathmini hizi zinaweza kufanywa kwenye karatasi au kielektoniki (kwenye mtandao au bila mtandao).

**Je, maswali haya ya mwongozo yanatumiwa na nani?** Wafanyakazi, timu na watu kwenye ngazi zote.

**Je, tathmini ya tafakuri inapaswa kufanyika wakati gani?** Muda wowote wakati wa mradi, lakini ni bora zaidi ikifanyika kabla ya kutumia zana zingine zilizomo kwenye kijitabu hiki.



8 The guiding questions are adapted from DFID (2008). The Gender Manual: A Practical Guide.

## MAELEKEZO

Zana hii imeundwa kwa ajili ya watu kutathmini uwezo wao wa kushughulikia kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Maswali ya mwongozo yameundwa kulisaidia shirika la World Vision kubaini mapungufu ya uelewa wa wafanyakazi katika kushughulikia masuala ya GESI. Mfano wa zana ya uchanganuzi ya kutumia programu ya komputa ya Exel inayowasilishwa hapa chini inaweza kuonyesha majibu ya watu na kuwasilisha matokeo kwa kiashiria cha rangi za taa za barabarani:

- **Kijani** = Watu wengi wana mtazamo chanya, fikra na imani katika kuondoa ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijami
- **Njano** = Nusu ya wafanyakazi wana mtazamo chanya, fikra na imani katika kuondoa ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii
- **Nyekundu** = Watu wengi wana mtazamo hasi, fikra na imani katika kuondoa ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii

Kila mwanatimu anapaswa kujaza tafakuri hii ili kusaidia kubaini uwezo na udhaifu. Matokeo yanapaswa kuwa sehemu ya mkakati ya mradi/ ujifunzaji na maendeleo kwenye timu.

**Jedwali 2 | Orodha ya Tafakuri ya Mtu Mmoja Mmoja yenye Muitikio wa GESI**

| Kiashiria | Swali | Weka Tiki | | Mapendekezo |
|---|---|---|---|---|
| | | Ndio | Hapana | |
| **Mtazamo wa mtu mmoja mmoja juu ya umuhimu wa GESI kwenye shirika la World Vision** | 1. Je, unafikiri kuwa shughuli za mradi zinazozingatia jinsia zinahitajika ili kuongeza ufanisi wa shirika la World Vision? | | | |
| | 2. Je, unafikiri shughuli maalumu za mradi zinahitajika kwa manufaa ya watu waliokandamizwa ili kuhakikisha wanafaidika kwa usawa? | | | |
| | 3. Je, unafikiri kuwashirikisha wanaume na wavulana, na viongozi wa jadi / jamii / dini itasaidia shirika la World Vison kuwa na matokeo bora katika kuwezesha usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa kijamii? | | | |
| | 4. Je, ni muhimu kwa mradi wako kuhakikisha kuwa aina mbalimbali za ukosefu wa uhusishaji (yaani kijamii, kiuchumi au kisiasa) zinazingatiwa? Je, ni muhimu kuzingatia athari zote mbili za kiuchumi za kuwa na ulemavu na zile za unyanyapaa wa kijamii unaohusiana na kuwa na ulemavu? | | | |
| **Majukumu na uwajibikaji wa kujumuisha GESI** | 5. Je, unaamini kuwa una jukumu la kujumuisha GESI katika kazi yako? | | | |
| | 6. Je, unawawajibisha wengine ili kuhakikisha kuwa shirika lako na timu yote pamoja na miradi yako ina uhusishaji? | | | |
| | 7. Je, ulishawahi kuwawajibisha wengine ili kupata ufanisi wa GESI? | | | |

| Kiashiria | Swali | Weka Tiki | | Mapendekezo |
|---|---|---|---|---|
| | | Ndio | Hapana | |
| | 8. Je ulishawahi kufanya jambo lolote la ziada ili kuhakikisha usalama wa wanawake na wanaume katika timu yako na washiriki wa mradi? | | | |
| | 9. Je, unaonyesha sifa za uhusishaji kwenye uongozi, kama vile kuzingatia mahitaji ya wafanyakazi, wabia, watu wenye ulemavu wanaojitolea, au kutoka kwenye jamii zilizokandamizwa, taaluma, dini, n.k? | | | |
| | 10. Je, umeweka ulazima wa ushiriki sawa au malengo ya ushiriki katika timu yako na / au katika shughuli zako? | | | |
| | 11. Je, ni muhimu kuhakikisha kuwa wanawake na / au wafanyakazi kutoka kwenye makundi yaliyo kandamizwa katika mradi / timu yako wana nafasi za uongozi? | | | |
| | 12. Je, umejumuisha njia za kukuza uwezo wa kufanya maamuzi kwa wanawake katika kaya wanazoishi na katika jamii? | | | |
| | 13. Je, umefikiria jinsi eneo unalotumia kuendeshea mafunzo linavyoweza kuwa na changamoto kwa watu wenye ulemavu kuhudhuria(kwa mfano wale wenye ulemavu wa mwili au viti vya magurudumu) na je,umeandaa mpango wa kupunguza vizuizi hivi (kama vile kujenga kidaraja cha kuteremkia kwa urahisi au lifti)? | | | |
| | 14. Je, umefikiria jinsi watu wenye ulemavu wa kuona au kusikia wanavyohitaji njia tofauti tofauti za mawasiliano na mafunzo? | | | |
| **Uelewa wa GESI** | 15. Je, unajua jinsi ya kuendeleza mipango ya kushughulikia tamaduni za kijamii zenye ubaguzi na zisizo na usawa zinazoathiri utekelezaji wa miradi? | | | |
| | 16. Je, unafahamu jinsi miradi itakavyoathiri makundi mbalimbali ya kijamii kwa namna tofauti totauti (wanawake, wanaume, watoto, watu wenye ulemavu n.k.)? | | | |
| | 17. Je, unaelewa ni nini kinazuia wanawake na watu wenye ulemavu kuhudhuria hafla za mradi (kwa mfano, utunzaji wa watoto, ukosefu wa uhuru wa kutembea) na je, umeandaa mpango wa kupunguza vizuizi hivi (kama vile kutoa pesa ya kumlipa mlezi wa watoto, kuomba ruhusa kutoka kwa mume)? | | | |
| | 18. Je, unajua jinsi ya kushughulikia mila, maoni na mitazamo kandamizi? | | | |
| | 19. Je, unajua jinsi ya kushughulikia na kubadilisha sheria, sera, na vitendo vya kibaguzi? | | | |

| Kiashiria | Swali | Weka Tiki | | Mapendekezo |
|---|---|---|---|---|
| | | Ndio | Hapana | |
| | 20. Je, unajua jinsi ya kushughulikia mahusiano, majukumu na miundo isiyo na usawa? | | | |
| | 21. Je, unajua jinsi ya kuwawezesha wanawake uwezo wa kuwa viongozi na kufanya maamuzi? | | | |
| | 22. Je, unajua jinsi ya kufanya kazi na watu wenye aina mbalimbali za ulemavu?? | | | |
| **Kujenga uwezo wa GESI** | 23. Je, umepata mafunzo yoyote ya jinsi ya kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia kupitia afua za shirika la World Vision? | | | |
| | 24. Je, umewahi kupata mafunzo yoyote yanayohusu uhusishaji wa kijamii (ukizingatia uhusishaji wa walengwa mbalimbali kama vile watu wenye ulemavu, dini tofauti, na makundi mengine yanayokandamizwa)? | | | |
| | 25. Je, unadhani kuwa unaweza kuzungumza kuhusu uhusishaji wa wanawake na watu wenye ulemavu kwenye majukwaa yote unavyoshiriki? | | | |

## MFANO WA ZANA YA UCHANGANUZI KWA AJILI YA TATHMINI YA TAFAKURI

Ufuatao ni mfano wa namna ambavyo shirika la World Vision linaweza kuchanganua data zizokusanywa kutoka kwenye tathmini za mtu mmoja mmoja. Kwa kutumia programu ya kompyuta ya Excel, data zilizokusanywa zinaweza kuambatanishwa na namba ya utambulisho wa mtu.Ili kuwezesha mgawanyo wa data na uchanganuzi, tafadhali hakikisha unakusanya data ya sifa mbalimbali kama vile jinsi na umri. Ingiza data iliyokusanywa kwenye zana ya uchanganuzi kwenye karatasi au kidigitali. Kisha, weka alama ya "X" kwenye kila swali kama inavyoonekana kwenye karatasi ya kukusanyia data. Kwa kutumia Excel, unaweza kutengeneza zana ya uchanganuzi ili ichanganue moja kwa moja majibu ya mtu mmoja mmoja kwa kila kiashiria na kuwasilisha majibu ya mitazamo ya kila mtu, uelewa na majukumu yao kwenye GESI. Tunza karatasi za data kwa madhumuni ya kutunza taarifa.

**Jedwali 3 | Mfano wa Zana ya Uchanganuzi wa Kitakwimu wa Tathmini ya Tafakuri**

| Mhojaji (kwa sifa mbalimbali kama jinsi, umri, nafasi) | | | Kiashiria 1 | | | | | | Kiashiria 2 | | | | | | Kiashiria 3 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Q1 | | Q2 | | Q3 | | Q4 | | Q5 | | Q6 | | Q7 | | Q8 | |
| | Jinsi | Nafasi | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana |
| P1 | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| P2 | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Px | | | | | | | | | | | | | | | | | | |



# Sehemu 2
# Jinsi ya Kufanya Uchanganuzi wa GESI

Sehemu hii inaelezea uchanganuzi wa GESI kama mkabala wa kiuchanganuzi unaotusaidia kubaini, kuelewa na kuelezea mapungufu na tofauti kulingana na ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Sehemu hii inawasilisha zana moja:

**ZANA 2.1** Uchanganuzi wa GESI

## ZANA 2.1 UCHANGANUZI WA GESI

Kuna njia mbalimbali za kufanya uchanganuzi wa GESI. Zana hii inawasilisha mwongozo wa wakati gani, sababu, na jinsi ya kufanya uchanganuzi wa GESI, inatoa hatua nne ambazo zinaweza kufaa kwenye mchakato huu.Uchanganuzi wa GESI unaweza kuibua maswali, kuchanganua na kuripoti taarifa na kutengeneza mikakati muhimu ya kuongeza usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Kukamilisha uchanganuzi wa GESI inasaidia kugundua desturi za kijamii, imani,matendo na mitazamo inayosababisha tofauti za mahitaji ya mtu mmoja mmoja, vikwazo na fursa.

### KWA NINI TUNAFANYA UCHANGANUZI WA GESI?

Desturi za kijinsia na kijamii na mahusiano ya kimamlaka husababisha tofauti za watu katika upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma, matarajio, ufanyaji maamuzi, ushiriki, miundo ya fursa, na ustawi kwa ujumla. Ikiwa mienendo hii haieleweki vizuri wakati wa usanifu wa programu, basi moja kwa moja ukosefu wa usawa utaongezeka. Tunapaswa kufanya kitu tofauti au jambo la ziada ili kuhakikisha tunakuwa na muitikio wa kijinsia na uhusishi wa kijamii.

**Uchanganuzi wa GESI husaidia:**

- Kuongeza ufahamu binafsi na wa taasisi kuhusu GESI na kujali GESI.
- Kubainisha mahitaji tofauti tofauti, vipaumbele na mazingira hatarishi ya wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Kuelewa majukumu na wajibu wa kijinsia-yupi,anafanya kipi, kwa nini na wakati gani?
- Kutambua nani ana upataji na ufikiaji, udhibiti na mamlaka ya kufanya maamuzi.
- Kubaini sababu za kina zinazoendeleza mila na desturi kandamizi za kijinsia na kijamii na mazoea (mahusiano ya kijamii, taasisi, na miundo).
- Kuweka wazi matokeo, faida ma athari za shughuli za programu kwa wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Kubainisha tofauti zingine miongoni mwa watu (ukabila, hali ya kijamii na kiuchumi, na sifa zingine) zinazoathiri jinsi wanavyoyatazama maisha na shughuli za mradi.

## UCHANGANUZI WA GESI UNATAKIWA KUFANYIKA LINI?

Uchanganuzi wa GESI unapaswa kufanywa mwanzoni mwa mradi au wakati wa hatua ya kuunda wazo la mradi ili kufanikisha usanifu na utekelezaji wa mradi. Unaweza pia kutumiwa wakati wa kuandika pendekezo la mradi na kwenye hatua ya usanifu wa mradi, kwenye utekelezaji wa mradi kama mkakati wa ufuatiliaji, na wakati wa tathmini (utafiti wa kwanza, wa kati au wa mwisho wa mradi).

## NANI HUONGOZA UCHANGANUZI WA GESI?

Mameneja wa programu au mradi na wafanyakazi wenye utaalamu, washauri wa GESI, wawezeshaji wa jamii au wataalamu wa kutoka nje ya mradi wenye uzoefu wa GESI ambao wamepewa kazi kwenye mchakato wa tathmini ya nje.

## HATUA ZA KUFANYA UCHANGANUZI WA GESI

Zana hii ina hatua nne zinazoweza kufuatwa katika kufanya uchanganuzi wa GESI:

| | |
|---|---|
| **Hatua 1** | Tafakuri ya Pamoja |
| **Hatua 2** | Mapitio ya Maandiko na Ukusanyaji wa Data za Upili wenye Muitikio wa GESI |
| **Hatua 3** | Ukusanyaji wa Data za Msingi wenye Muitikio wa GESI |
| **Hatua 4** | Uchanganuzi wa Data na Uandishi wa Ripoti wenye Muitikio wa GESI (Rejea ZANA 4.3) |

**Kidokezo!**

Fanya uchanganuzi wa GESI mwanzoni mwa programu. Hii itasaidia GESI kujumuishwa vizuri kwenye shughuli na kuwekewa bajeti. Ni vigumu kujumuisha GESI baada ya programu kuanza.

Kimsingi uchanganuzi wa GESI hutumia hatua zote nne, lakini wakati mwingine hili haliwezekani. Hivyo basi, kila hatua imeundwa kama hatua inayojitegemea. Ikiwa una changamoto ya fedha au muda, unaweza kufikiria kuchanganya hatua zozote. Mkabala wa 'kiwango cha dhahabu' ni kuchukua hatua zote nne, 'kiwango cha fedha' ni hatua ya tatu, na 'kiwango cha shaba' ni kufanya hatua moja tu.

Kuna maswali mengi ambayo unaweza kuyajibu kwenye uchanganuzi wa GESI. Ni muhimu kuyapa kipaumbele maswali ambayo ni muhimu katika kuwezesha programu kuwa na mabadiliko ya GESI. Maswali haya yanaweza kujibiwa na njia yoyote kati ya hizi zilizoorodheshwa kwenye hatua nne.Ili kuwezesha utambuzi wa maswali muhimu, tumia vikoa vitano vya GESI kuandaa swali moja katika kila kikoa halafu ongezea maswali ya ziada yatakayokusaidia kujibu hilo swali muhimu. Hapa chini utaona vikoa vitano vimebadilishwa kuwa maswali.

**Kutegemeana na malengo ya programu yako, utahitaji kutumia haya maswali kama mwongozo wa kuandaa maswali yako katika vikoa vitano vya GESI.**

Maswali maalumu ya kila sekta yanaweza kupatikana kwenye miongozo ya ujumuishaji wa GESI kwenye sekta. Lakini pia hapa chini kuna mwongozo wa mambo ya kufikiria katika vikoa vya GESI.




## UPATAJI NA UFIKIAJI

- Je, ni mabadiliko gani yanatakiwa yafanyike ili kila mtu awe na uwezo wa kupata na ku¬fikia, kutumia, na/au kumiliki mali, rasilimali, fursa, huduma, faida, na miundombinu?
- Je, ni makundi yapi hayahusishwi kwenye rasilimali, fursa, huduma, faida, na miundombinu kwa sasa?
- Kwanini hayahusishwi?

### UFANYAJI MAAMUZI

- Je, ni kwa namna gani kila mtu anaweza kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi bila kulazimishwa kwenye ngazi ya mtu binafsi, kaya, jamii, na jumuiya?
- Je, maamuzi gani ni muhimu na nani huwa anafanya maamuzi hayo?
- Je, ni kwa nini baadhi ya makundi hayahusishwi katika ufanyaji maamuzi?

### USHIRIKI

- Je, ni kwa namna gani kila mtu anaweza kuwa na uwezo wa kushiriki na kujihusisha katika masuala ya jumuiya na mifumo ya kimamlaka ambayo inashawishi na kuamua kuhusu maendeleo, shughuli za maisha na matokeo?
- Je, ni shughuli zipi na mifumo gani ya kimamlaka ni muhimu? Nani huwa anashiriki?
- Je, ni kwa nini baadhi ya makundi hayashiriki katika shughuli hizo na mifumo ya kimamlaka?

### MIFUMO

- Je, ni kwa namna gani tunaweza kuchochea uwepo wa mifumo yenye usawa ambayo inashughulikia mahitaji mbalimbali ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, na kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya uhusishwaji wao?
- Je, mifumo muhimu iliyo rasmi na isiyo rasmi iliyopo kwa sasa ni ipi?
- Je, ni kwa namna gani mifumo hii huchochea kukosekana kwa usawa, na kushindwa kukabili mahitaji ya watu walio katika mazingira hatarishi au haiwahusishi katika mambo mbalimbali?

### USTAWI

- Je, ni kwa namna gani tunaweza kuimarisha hisia ya kuwa na thamani, uwezo, hadhi, ujasiri, utu, usalama, afya, na ustawi wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, na kiroho kwa ujumla. Hii ni pamoja na kuishi bila ukatili wa kijinsia na aina zote za unyanyapaa na ubaguzi?
- Je, ustawi wa nani hauimarishwi? Nini kinatakiwa kifanyike ili kuimarisha ustawi wa watu hawa?

## Hatua 1 | Tafakuri ya Pamoja

Hatua hii inalenga kwenye tafakuri ya pamoja ili kuelewa ni nani hahusishwi katika jamii, mienendo ya kimamlaka inayohusika na ukosefu wa uhusishaji, na jinsi ya kuhakikisha ushiriki kamili wa makundi yaliyotengwa katika mipango ya maendeleo. Lengo ni kubaini makundi yanayokandamizwa na yaliyo katika mazingira hatarishi ni yapi, sababu za kukandamizwa na kuwa katika mazingira hatarishi, na wahusika wengine muhimu ambao wanaathiri matarajio na tabia za makundi yaliyotengwa. Tafakuri ya pamoja inaweza pia kusaidia kuchanganua kiwango cha athari zinazoweza kuupata mradi, kama vile athari zinazotarajiwa za kukosa uhusishaji kwenye mradi, mikakati ya kutatua hilo tatizo, na taarifa nyingine yoyote inayohitajika kuboresha uhusishaji kwenye mradi.

### NANI HUSHIRIKI?

Watu walioko kwenye timu ya mradi, wafanyakazi wa mradi walio na uelewa, viongozi wa kijamii, na wawakilishi kutoka kwenye makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi au yanayokandamizwa au yasiyohusishwa. Ni muhimu kuhakikisha kwamba makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, yaliyokandamizwa au yasiyohusishwa yanawakilishwa na yanashiriki kwenye mchakato huu, vinginevyo hatutaweza kupata picha kamili. Ukiwa unawahusisha watu wenye ulemavu, hakikisha aina mbalimbali za ulemavu zinawakilishwa (ulemavu wa kuona, kusikia, kutembea, ufahamu na akili).

## MAELEKEZO

Fanya shughuli zifuatazo hapo chini kulingana na mwongozo wa hatua kwa hatua ambao umetolewa. Hatua hizo zitakusaidia kubaini watu ambao hawahusishwi kwenye eneo la mradi unaopendekezwa na kusaidia kuweka wazi sababu za kutohusishwa kwao. Baada ya hapo, unaweza kushughulikia mazingira hatarishi uliyoyabainisha. Matokeo ya shughuli lazima yajumuishwe katika mawazo thabiti na kurekodiwa kwenye jedwali hapa chini.

**Vitendea kazi na vifaa vinavyohitajika:** kompyuta, projekta, bango kitita na kalamu za wino mzito.

**Rasilimali watu inayohitajika:** Mwezeshaji mmoja na mwandika vitini mmoja.

## Mwongozo Hatua kwa Hatua

1. Andaa kikundi cha washiriki.
2. Tumia maswali yafuatayo kuongoza tafakuri yako ya pamoja:
    a. Je, ni makundi gani ya kijamii yapo katika eneo lako la mradi pendekezwa (kwa mfano watu wenye ulemavu, kabila, dini, kazi, hali ya uchumi, tabaka, nk)?
    b. Je, kati ya makundi haya ni yapi yanakandamizwa, hayahusishwi, au yako katika mazingira hatarishi zaidi?
    c. Je, ni kwa namna gani makundi haya yako katika mazingira hatarishi, yanakandamizwa zaidi, au hayahusishwi?
    d. Je, kuna makundi yoyote ya watu ambao kwa lugha za mahali husika yanatambuliwa kwa namna hasi au za dharau? Ikiwa jibu ni ndiyo, ni makundi yapi?
    e. Je, ni mila na desturi zipi za kijamii zipo katika eneo hili ambazo huzuia watu wengine kufaidika na mradi?
    f. Je, ni wadau gani muhimu au watu wanaochochea ukosefu wa uhusishaji wa makundi ya watu wanaokandamizwa au walio katika mazingira hatarishi?
    g. Je, ni makundi yapi yenye ushawishi au taasisi zipi zinasisitiza ufuataji wa mila na desturi kandamizi za kijinsia na za kijamii?
    h. Je, ni kwa namna gani wadau hao wenye ushawishi au watu, makundi, au taasisi zinaimarisha mila na desturi za kijamii na kijinsia ambazo zinazuia uhusishaji wa kijamii?
    i. Je, madhara ya kutowashirikisha wale wanaokandamizwa na walio katika mazingira hatarishi katika mradi huu ni yapi?
    j. Je, jukumu la wadau au watu, makundi au taasisi zenye ushawishi katika kubadilisha mila na desturi za kijamii ili kuendeleza usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii ni lipi?
    k. Je, ni kwa namna gani wale wasiohusishwa, wanaokandamizwa na walio katika mazingira hatarishi wanaweza kulengwa kwenye mradi na kunufaika na afua za mradi?
3. Pitia kila swali:
    a. Andika maoni kwa kila swali ukiwa peke yako. Andika kile kinachokujia akilini mwako kwanza (dakika 10). Tafakuri ya kimya ina nguvu!!
    b. Mkiwa wawili wawili jadilini majibu yenu swali kwa swali (dakika 10). Je, mmeandika nini kinachofanana? kuna kitu kingine ulifikiria wakati mnajadiliana?
    c. Kisha fanyeni kazi katika timu na pitia kila swali kujadili na andika maoni ambayo yanafanana na kingine chochote kinakosekana (dakika 30). Chagua mtu mmoja awe mwongozaji, hii itasaidia kuhakikisha kuwa kila mtu kwenye timu anatoa maoni yake.
4. Jadili maswali haya kwenye timu. Andika majibu kwenye bango kitita.
    a. Je,ni kwa namna gani mradi wako unaweza kubadilisha uhusiano / hali ya watu wanaokandamizwa katika kaya na jamii? (dakika 10).

b. Je, kati ya chaguzi zote ulizoorodhesha ni zipi zinawezekana/zinafaa kushughulikiwa na mradi wako? Ruhusu kila mtu aweke alama kwenye chaguo lake kwa faragha (dakika 5). Unganisha majibu ya wote na ruhusu majadiliano kuona utofauti (dakika 10-15). Mwishoni, unapaswa kuwa na angalau maoni matatu mazuri/yenye uwezekano wa kuhusishwa kwenye mradi wako.

c. Je, ni taarifa gani ya ziada inakosekana? Je,unahitaji kujua nini zaidi ili kusaidia mradi kuwa na uhusishaji zaidi (kuhakikisha watu waliokandamizwa, walio katika mazingira hatarishi na waliotengwa,wanahusishwa na kufaidika na mradi)?

d. Je, ni kwa namna gani taarifa ya ziada au iliyopungua inaweza kupatikana?

5. Kamilisha jedwali kwa pamoja kama timu. Chini ya vichwa vya kila safu wima ni marejeo ya maswali maalumu ambayo yatasaidia kukamilisha safu wima (kwa mfano, swali 2a husaidia kukamilisha safu wima ya kwanza).

6. Onyesha jedwali kwenye chati mgeuzo na waombe washiriki wajaze jedwali kwa pamoja (orodha ya makundi ya kijamii yaliyokandamizwa, sababu za kukandamizwa/ na kuwa katika mazingira hatarishi, orodha ya watu/makundi na taasisi zenye ushawishi wa kubadilisha matarajio na tabia za watu wasiohusishwa, hatari ya kutengwa, na kupendekeza mikakati ya kupunguza jambo hili na kuhimiza uhusishaji).

7. Hii itakusaidia kuelewa aina ya taarifa uliyonayo na maelezo ziada unayohitaji kutoka kwenye tathmini za GESI (inaweza kutoka kwenye mapitio katika hatua ya 2 au uchanganuzi shirikishi wa GESI katika hatua ya 3 kupitia majadiliano ya vikundi na mahojiano).

8. Hii itakusaidia kujenga uelewa halisi juu ya jinsi suala lenye changamoto linavyoweza kushughulikiwa na maeneo ambayo unaweza kuwekeza juhudi zako.

**Jedwali 4 | Tafakuri ya Pamoja**

| Makundi ya kijamii yanayokandamizwa | Sababu za kukandamizwa na kuwa katika mazingira hatarishi | Watu muhimu wenye ushawishi wa kubadilisha matarajio na tabia za watu wasiohusishwa (Makundi yenye ushawishi) | Hatari za kutohusishwa kwenye mradi | Mapendekezo ya mikakati ya kupunguza tatizo | Unahitaji kufahamu nini kingine ili kuboresha uhusishaji kwenye mradi? |
|---|---|---|---|---|---|
| **2a, 2b** | **2c, 2d, 2e** | **2f, 2g** | **2b, 2c, 2e, 2h, 2i** | **2j, 2k, 4a, 4b** | **4c, 4d** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

Taarifa hii itatumika kwenye hatua ya 2.

*Kuwa mdadisi! Tafiti zana zingine, kama uchanganuzi wa kijamii wa kijitabu cha utekelezaji wa vitendo cha shirika la CARE .*

Kidokezo!

# Hatua 2 | Mapitio ya Maandiko na Ukusanyaji wa Data za Upili wenye Muitikio wa GESI

## MUHTASARI

Shughuli za mapitio ya maandiko huhusisha mapitio ya machapisho,kukusanya na kuchanganua data za upili, na kutengeneza orodha ya nyaraka muhimu zinazohusiana na mada husika. Ikiwa unafanya hatua hii kama muendelezo wa Hatua 1 (tofauti na shughuli inayojitegemea), tumia matokeo ya Hatua 1 kuongoza utafutaji wako.Kwa mfano, hakuna haja ya kutafuta taarifa inayowahusu vijana ikiwa hili si kundi la waliokandamizwa lililobainishwa kwenye Hatua1. Hakikisha unafanya hatua hii kulingana na vikoa vya GESI – angalia Sehemu 1. Ni muhimu kuhakikisha kuwa taarifa iliyokusanywa inatoa mwanga kwenye kila kikoa.

Mapitio ya maandiko ya GESI hubainisha sababu muhimu zinazoathiri makundi maalumu mbalimbali kwa kutumia vikoa vya GESI. Pia hutoa tarifa muhimu kuhusu hali ya GESI inayoelezewa kwenye maandiko na husaidia kuthibitisha taarifa ambazo zilikuwa zimebadilika baada ya muda fulani au ambazo haziko sahihi kwa sasa. Data zinazokusanywa kwa kutumia mapitio ya maandiko zinaweza kutumika kama utafiti wa msingi kuelewa mabadiliko yanayosababishwa na utekelezaji wa mradi. Mapitio ya maandiko yanaweza pia kufanyika wakati wa tathmini ya programu. Hii itahusisha mapitio ya nyaraka zote za programu na uchanganuzi wa malengo ya programu ya GESI, na mikakati ya utekelezaji na majadiliano ya masuala ya GESI. Hii inaweza kubaini mapungufu yanayotakiwa kushughulikiwa kwenye programu yetu ili iweze kuleta mabadiliko ya GESI.

**Jedwali 5 | Mapitio ya Maandiko ya Data za GESI**[9]

| Aina ya Nyaraka | Taarifa Unazoweza Kukusanya |
|---|---|
| **Nyaraka za programu, mradi, au za shirika:** Mipango kazi, maelezo ya programu,ripoti za utafiti wa awali, ripoti ya uchanganuzi wa vikwazo, mpango wa ufuatiliaji na tathmini na ripoti nyingine za kuanzisha mradi | Kuelewa muktadha wa programu<br>Kama mtazamo wa GESI umejumuishwa kwenye usanifu,ufuatiliaji na athmini<br>Kama kuna mapungufu yoyote kwenye ujumuishaji wa GESI |
| **Data za kitakwimu:** Tafiti za kidemografia na kiafya, data kutoka Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa na takwimu za serikali zinazohusu vikoa vya GESI | Kitakwimu, taarifa zilizogawanywa, za kimuktadha juu ya GESI ndani ya nchi/jamii |
| **Data za kitaamuli:** Tafiti za GESI zilizofanywa na wengine, uchanganuzi wa GESI au ripoti za tafiti juu ya vikoa vya GESI | Kitaamuli, taarifa zilizogawanywa, za kimuktadha zinazohusiana na mahusiano ya GESI ndani ya nchi/jamii |
| **Nyaraka za serikali:** Sheria na sera | Kuelewa muktadha wa sheria na siasa ambamo programu inafanya kazi<br>Kubaini mafanikio na mapungufu kwenye haki za wanaume,wanawake, watoto,watu wenye ulemavu na makundi mengine yanayoishi katika mazingira hatarishi katika vikoa vitano vya GESI |

Mapitio ya maandiko yanaweza kufanywa kwa njia mbili: mapitio ya machapisho na ukusanyaji wa data ya upili na unaweza kukusanya zote; data za kitaamuli na data za kitakwimu.[10]

9 Ramdhani, et. al (2014). Writing a Literature Review.
10 WFP (2009). Comprehensive Food Security and Vulnerability Analysis.

## MAPITIO YA MAANDIKO YENYE MUITIKIO WA GESI

Mapitio ya maandiko ni majadiliano ya taarifa iliyochapishwa hapo awali juu ya mada au maswali yanayohusiana na GESI. Mapitio ya maandiko yanaweza kukusanya data za upili zote za kitaamuli na za kitakwimu zinazohusiana na mada yako.Data hizi zinaweza kukusaidia kubaini mapungufu na changamoto husika na/au fursa zinazotakiwa kushughulikiwa.

### Mwongozo Hatua kwa Hatua[11]

1. **Chagua mada au swali la utafiti**: Hii ni muhimu kwa sababu mada unayochagua itakuongoza kujua aina ya taarifa ya kutafuta na mambo ya kuzingatia wakati wa kutafiti na kuandika mapitio yako. Hakikisha mada yako ina muitikio wa GESI na inajumuisha vikoa vitano vya GESI.Kwa mfano, athari za kiwango cha elimu katika upatikanaji na ufikiaji wa huduma za afya kwa wanawake, wanaume, na watu wenye ulemavu nchini Malawi.

2. **Tafuta mapitio yanayohitajika:** Anza kwa kubaini maandiko yaliyochapishwa unayohitaji. Tafuta kwa mfumo wa elektroniki vitabu, makala, nyaraka za kiserikali, au ripoti juu ya mada yako. Tumia maneno muhimu na chuja ambayo unafikiri yanaweza kubainisha vema mada inayohusika. Kwa mfano, utafutaji wa awali wa "kiwango cha elimu na upataji na ufikiaji wa huduma za afya" unaweza kuleta makala zinazozungumzia kiwango cha elimu, ufikiaji wa huduma za afya, na jinsia lakini ambazo pia zinajadili "ujumuishaji wa kijamii". Vyanzo vya miaka ya karibuni ni bora zaidi (angalau ndani ya miaka 5-7 iliyopita).

3. **Bainisha vyanzo vya msingi na kanzidata:** Siku hizi, mapitio ya maandiko huweza kufanywa kwa urahisi mkondoni ambapo unaweza kutafuta nakala za kielektroniki, ripoti, na safu za data.[12] Kama mapitio hayapatikani mkondoni, unaweza kutafuta maktaba iliyo karibu kuona kama kuna vitabu na makala zinazohusu mada yako. Maktaba nyingi hutoa huduma ya kuazima vitabu kutoka kwenye maktaba zingine kama hawana makala unazohitaji. Jambo la muhimu ni kwa vyanzo vilivyobainishwa kutoa mwangaza juu ya vikoa vya GESI.

Vyanzo bora kwa ajili ya mapitio ya maandiko ni vyanzo vya msingi au halisi kama vile:

- Ripoti za shirika la World Vision na mashirika mengine ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGO) zilizoandika nyaraka za za programu za GESI katika nchi au kanda, ikiwa ni pamoja na tathmini za shirika la World Vision juu ya watoto walio katika mazingira hatarishi, tathmini za awali za walezi na vijana
- Tathmini za USAID juu ya ujumuishaji wa kijinsia na kijamii kwa kila nchi
- Ripoti za Umoja wa Kimataifa Wanawake katika nchi za mbalimbali
- Mifumo ya Maendeleo ya Jinsia ya shirika la UNDP[13] na Mifumo ya Maendeleo ya Watu[14]
- Kielelezo jumuishi cha umaskini cha shirika la UNICEF[15]
- Kitengo cha Data za Jinsia cha Benki ya Dunia[16]
- Takwimu za Wizara Kitaifa (pamoja na data za sensa na tafiti za kijamii)
- Tafiti za Kitaifa za Kaya na Idadi ya Watu
- Mkakati / Sera ya Kitaifa inayohusu Jinsia
- Mkakati wa Kitaifa wa Ujumuishaji wa kijamii / Sera ya Watu wenye Ulemavu Katiba za Nchi
- Ripoti za Tathmini
- Ripoti za Haki za Binadamu za Idara za Serikali nchini Marekani
- Ripoti za Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu
- Ripoti za Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake
- Ripoti za Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto
- Mapitio ya majarida yaliyochapishwa

11 Adapted from Rennison and Hart (2019).Research Methods in Criminal Justice and Criminology.
12 Ramdhani, et. al (2014). Writing a Literature Review
13 Click on the country report for national gender data differences: hdr.undp.org/en/content/gender-development-index-gdi
14 UNDP Human Development Index: hdr.undp.org/en/content/human-development-index-hdi
15 For more information on the statistics used to measure multi-dimensional child poverty see UNICEF (2011).
16 The World Bank Gender Data Portal: atatopics.worldbank.org/gender/

4. **Punguza vyanzo vya data:** Chunguza kichwa cha habari na usome ikisiri au utangulizi kubaini mapitio ambayo ni sahihi na maneno muhimu ambayo yanaweza kukusaidia kupanua utafutaji wako. Ikisiri (abstract) itatoa muhtasari wa malengo, mbinu, matokeo na hitimisho katika aya moja. Pia, unaweza kuangalia orodha ya marejeleo ya mapitio ambayo umeyabainisha kuwa ni muhimu katika kupata marejeleo mengine utakayohitaji kuyasoma.[17] Pitia kurasa za yaliyomo kwenye vitabu, ripoti, sera au nyaraka ili kuona kama kuna sura yoyote au sehemu ambayo inahusiana na mada yako.

5. **Andika muhtasari wa taarifa muhimu:** Soma na uchanganue habari muhimu kutoka kila chanzo. Andika aya ya muhtasari kwa kila chanzo.Taarifa zifuatazo zinapaswa kuwekwa:[18]
   - Mada na malengo: taarifa hii inaweza kupatikana kutoka kwenye ikisiri, utangulizi na hitimisho
   - Je, mapitio yana umuhimu gani, yanajaribu kuziba pengo gani? Ikiwa mapitio yanaongozwa na nadharia, basi huna budi kuweka taarifa zake
   - Je, data zilikusanywa na kuchanganuliwa vipi, data ni ya kipindi cha muda gani? Unazeza kupata hizi taafifa kwenye kipengele cha methodolojia
   - Je, matokeo au uvumbuzi ni upi? hitimisho lilikuwa lipi?
   - Je, kuna maudhui mengine yaliyoibuka? Ni muhimu kuzingatia kwamba maudhui unayochagua yanaakisi vikoa vya GESI. Kwa mfano, athari ya kiwango cha elimu juu ya upatikanaji na ufikiaji wa maji salama ya kunywa kwa vikundi mbalimbali vya kijamii, au athari ya kiwango cha elimu kwa ustawi wa kihisia wa watoto.

Kidokezo!

Unaweza kutumia baadhi ya viunzi vya kimataifa kama mwongozo wako wa mapitio ya maandiko. Mfano *Kiunzi cha Uchanganuzi wa Jinsia cha Havard au Kiunzi cha Mpangilio wa Jinsia cha Moser's*

17 Rennison and Hart (2019). Research Methods in Criminal Justice and Criminology

18 Rennison and Hart (2019). Research Methods in Criminal Justice and Criminology.

## ZANA YA JEDWALI MATRIKI SANISI KWA AJILI YA MAPITIO YA MAANDIKO

Jedwali la matriki sanisi (synthesis matrix) linaweza kutumika kubainisha, kuunganisha, na kupangilia vyanzo vya mapitio yako. Kwanza bainisha mapitio kumi au zaidi ambayo yanahusiana sana na mada yako. Kisha kwa kila chanzo orodhesha mwandishi na mwaka wa chapisho, bainisha madhumuni ya mapitio,mbinu iliyotumika kukusanya data, sifa ya sampuli, matokeo makuu, maudhui makuu unayoweza kuyatoa kwenye matokeo, namna matokeo yanavyoendana au kuunga mkono taarifa kutoka kwenye vyanzo vingine (vinavyofanana), na namna zinavyotofautiana na matokeo yaliyopatikana kutoka kwenye vyanzo vingine (upekee).[19] Kisha kamilisha jedwali la matriki sanisi hapa chini.

**Jedwali 6 | Zana ya Matriki Sanisi**[20]

| Chanzo: Makala, kitabu, ripoti, sera n.k. | Mwandishi na Mwaka | Madhumuni | Mbinu | Sampuli | Matokeo | Kufanana | Upekee |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chanzo 1 | | | | | | | |
| Chanzo 2 | | | | | | | |
| Chanzo 3 | | | | | | | |
| Chanzo 4 | | | | | | | |
| Chanzo 5 | | | | | | | |
| | | | | | | | |

6. **Baini maudhui, uhusiano, mwenendo na mapungufu:** Kusanya, changanua kwa kina, tathmini na andika muhtasari wa taarifa kulingana na maudhui. Kuwa makini na uhusiano, mwenendo, na mapungufu yanayoibuka juu ya mada.[21] Hamisha sentensi kutoka kwenye muhtasari wa aya na uziweke pamoja katika mada. Kwa mfano, unaweza kusema, mapitio ya maandiko yanaonyesha kuwa wanawake wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kutokuwa na ufikiaji na upataji wa maji safi ya kunywa ukilinganisha na makundi mengine ya kijamii. Kisha angalia sentensi inayozungumzia jambo hili katika kila aya ya muhtasari. Kumbuka kuwa, jambo la msingi ni kubaini muhtasari wa vyanzo vyote vinavyohusiana na mada. Angalia kama kuna mawazo yoyote yanayopingana kwenye mada.

7. **Amua kuhusu muundo na mpangilio wa mapitio yako:** Baada ya kuandika muhtasari wa mapitio yako kulingana na maudhui, unapaswa kuamua jinsi utakavyoapangilia maudhui hayo. Anza na utangulizi ukifuatiwa na madhumuni ya mapitio ya maandiko. Kisha pangilia mapitio yako katika vipengele, mada kuu, na mada ndog.[22] Kwa mfano, unaweza kuwa na kipengele juu ya faida za upataji na ufikiaji wa maji safi na salama. Mada hizi ndogo zitaonyesha athari kwa kila kundi: wanawake, wanaume, watoto, watu wenye ulemavu,n.k. Unaweza pia kugawa vipengele vyako kwenye mada kubwa kama vile vikoa vya GESI, kwa mfano, athari ya upataji na ufikiaji wa maji safi na salama kwenye ustawi. Kisha utajadili namna upatiaji na ufikiaji wa maji safi na salama umeathiri kila kundi la kijamii kwa kila kikoa cha GESI.

8. **Andika mapitio:** Mapitio yako ya maandiko yanapaswa kuwa na utangulizi, sehemu kuu, hitimisho na orodha ya marejeleo. Malengo ya mapitio yako yataamua kile kinachotakiwa kuandikwa kwenye kila kipengele. Baada ya kuandika rasimu ya kwanza, utatakiwa kuisoma, kufanya marekebisho pale panapohitajika, na kisha kuandika rasimu ya mwisho[23]

    - **Utangulizi:** Unapaswa kutoa muhtasari, taarifa za usuli, umuhimu na malengo ya mapitio ya maandiko. Tambulisha maudhui utakayojadili kwenye sehemu kuu ya ripoti.

19 Ramdhani, et. al. (2014). Writing a Literature Review.
20 Ramdhani, et. al. (2014). Writing a Literature Review.
21 USAID (2014a).Toolkit for Monitoring and Evaluating Gender-Based Violence Interventions.
22 Rennison and Hart (2019).Research Methods in Criminal Justice and Criminology.
23 Cronin, et. al (2008); Rennison and Hart (2019).

- **Sehemu kuu:** Unaweza kuigawa sehemu kuu kwenye vipengele vikuu na vipengele vidogo au vichwa vya habari vya maudhui yako (kulingana na urefu wa mapitio yako). Unapaswa kufanya yafuatayo:
  - Andika muhtasari na sanisi vipengele vikuu vya kila chanzo kwa kutumia maneno yako mwenyewe
  - Changanua na kutoa tafsiri yako mwenyewe ya matokeo
  - Toa tathmini yenye kukosoa juu ya uzuri na udhaifu wa vyanzo vyako vya taarifa
- **Hitimisho:** Andika muhtasari wa matokeo muhimu na umuhimu wake kwa wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Kumbuka unafanya muhtasari wa mawazo makuu ya masuala yote kwenye vyanzo vyako. Usianzishe utafiti wala maudhi mapya kwa sasa. Bainisha matatizo, changamoto ambazo hazijatatuliwa, na mapungufu ambayo tafiti zijazo zinaweza kuyashughulikia. Toa mapendekezo ya namna ambavyo tafiti zijazo zinaweza kufidia mapungufu au kushughulikia matatizo uliyobaini kwenye maandiko.[24]
- **Marejeleo:** Unapaswa kutoa orodha kamili ya vitabu, majarida, ripoti na mapitio mengine uliyorejelea kwenye mapitio yako. Utatakiwa kuweka muundo wa marejeleo yako kulingana na mtindo unaouchagua. Hakikisha unaandika kila chanzo ulichokitumia kwenye maandiko yako na panga marejeleo kwa kufuata herufi ya jina la mwisho la mwandishi.

## MAELEZO MAFUPI KUHUSU NCHI

Maelezo mafupi kuhusu nchi yanatoa usuli kuhusu hali ya GESI katika nchi juu ya mifumo mbalimbali na namna inavyoathiri makundi mbalimbali ya jamii. Vilevile inasaidia kubaini mienendo ya GESI yenye mafanikio, fursa na mapungufu, na kutoa taarifa ya jinsi mifumo inavyoathiri haki za kijamii, kiuchumi, kitamaduni, na kisiasa kwa makundi mbalimbali ya kijamii. Ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii haufanyiki majumbani na kwenye familia tu, bali hufanyika pia katika taasisi mbalimbali. Taasisi hizi zinashabihiana na kuhusiana. Mabadiliko katika sera au shughuli katika taasisi moja yanaweza kuleta mabadiliko au kuathiri wengine. Kwa hiyo, inashauriwa kwamba maelezo mafupi kuhusu nchi yaangalie taasisi hizi zote kwa pamoja.[25]

### Maelekezo

- Maelezo mafupi kuhusu nchi yanapaswa kuanza na mapitio ya maandiko yenye muitikio wa GESI. Bainisha mapitio na data zinazohusu nchi hiyo. Jumuisha data zenye mgawanyo wa GESI kama zipo. Ikiwa data hizo hazipo, andika kuhusu jambo hilo
- Baada ya kupitia maandiko, unaweza kuwahoji watendaji wakuu katika wizara, mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi za kiraia, taasisi zilizopo eneo hilo, n.k. Weka upendeleo maalumu kwenye mtazamo juu ya wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, wazee, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi
- Maelezo mafupi kuhusu nchi hayapaswi kuwa zaidi ya kurasa 30. Maelezo zaidi yanaweza kuwekwa kwenye viambatanisho.[26] Jedwali hapa chini ni zana ya maelezo mafupi kuhusu nchi ambayo imechukuliwa kutoka Wakala wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uswisi -SIDA (2010)

24 Cronin, et. al (2008).Undertaking a Literature Review.
25 March & Mukhopadhyay (1999). A Guide to Gender-Analysis Framework.
26 Sida (2010). Guide to the Elaboration of Country Gender Profiles.

**Jedwali 7 | Maelezo Mafupi Kuhusu Nchi[27]**

| Kipengele | Taarifa ya kuandika |
|---|---|
| 1. Muhtasari | • Muhtasari wa hali ya GESI |
| 2. Utawala, mifumo ya uongozi na GESI | • Jitihada zozote za kupambana na ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii<br>• Miundo yoyote ya kitaasisi au kiutawala ambayo inaendeleza desturi ambazo zinasababisha kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii |
| 3. Mifumo ya kitaifa (sera, sheria, mikakati, programu na jitihada) | • Sheria rasmi,sera,taasisi au programu zilizopo ambazo zinakusudia kukuza GESI, mfano mpango wa Utekelezaji Kitaifa, Mkakati wa Kupunguza Umaskini<br>• Kiwango ambacho zinahimiza GESI<br>• Kiwango ambacho zinaonyesha ubaguzi wa wazi kwa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi |
| 4. Desturi za kijamii/sheria za kimila na taasisi | • Desturi za kijamii/sheria za kimila na tamaduni zinazokusudia kuhimiza GESI<br>• Kiwango ambacho zinahimiza GESI<br>• Kiwango ambacho zinaonyesha ubaguzi wa wazi kwa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi |
| 5. Haki za binadamu | • Zana za kimataifa za haki za binadamu zilizo wekewa sahihi au kupokelewa kama vile Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (*Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women-CEDAW*)<br>• Viunzi vya kisheria (kama katiba, urithi, umiliki wa ardhi,haki za makazi, sheria za familia na sheria ya kazi), utekelezaji wa sheria na usawa katika ufikiaji na upataji wa haki<br>• Taarifa kuhusu uwingi wa sheria (sheria ya kitamaduni, sheria ya kidini na sheria ya kiraia<br>• Sheria zipi huonyesha yafuatayo:<br>– Kuchochea GESI<br>– Kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii<br>– Ulinzi na haki za watoto<br>– Kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi<br>– Kuboresha upataji na ufikiaji huduma za afya ya uzazi kwa wanawake |
| 6. Hali ya kisiasa | • Ushiriki na uwezo wa kushawishi ufanyaji maamuzi kwenye ngazi zote<br>• Uwezo wa serikali kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ushiriki wa kisiasa kwa wanawake, na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi na kutoa huduma pasipo upendeleo wa kijinsia |
| 7. Hali ya kijamii na kiuchumi | • Hali ya umaskini, mgawanyo wa rasilimali na muda, na jinsi inavyoathiri makundi mbalimbali ya kijamii<br>• Majukumu ya kijinsia, upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma<br>• Huduma za kijamii (kama afya na elimu) na namna zinavyofikia mahitaji ya kibinadamu na haki za wanaume, wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi |



27 Sida (2010). Guide to the Elaboration of Country Gender Profiles.

| Kipengele | Taarifa ya kuandika |
|---|---|
| 8. Ukatili wa kijinsia | • Aina mbalimbali za ukatili wa kijinsia (ukeketaji,ukatili wa kingono na ukatili wa majumbani n.k.)<br>• Ukatili dhidi ya makundi yaliyo katika mazingira hatarishi (kama watoto, wazee, watu wenye ulemavu)<br>• Hatua za kisheria za kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia<br>• Upataji na ufikiaji wa huduma kwa waliotendewa ukatili |
| 9. Hitimisho, changamoto na fursa | • Uwezekano wa kupiga hatua<br>• Mambo yanayotia shaka na vikwazo<br>• Chochote kinachokosekana (kama sheria isiyo bagua, usawa wa kijinsia,ukatili wa kijinsia, unyanyasaji wa kingono,uhusishaji wa kijamii n.k.)<br>• Maeneo muhimu yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi<br>• Kutokana na hitimisho hilo, je, unaona mapungufu gani? ni yapi kati ya hayo yanaweza kushughulikiwa na mradi ili kufanikisha GESI?<br>• Mapendekezo kwa ajili ya mifumo yenye mabadiliko ya GESI |

## UKUSANYAJI WA DATA ZA UPILI ZA GESI

Hii inaongelea data za GESI ambazo zilikusanywa na mtu mwingine. Data za upili zinaweza kutoa taarifa ya kitaamuli na kitakwimu juu ya masuala mbalimbali ya GESI kama mienendo, mapungufu, na fursa zinazohusiana na mada yako. Vyanzo vingi vya data za upili huwa ni rahisi kupatikana kwa watu wote, kwa mfano, takwimu rasmi kama sensa, utafiti wa kaya na idadi ya watu, tafiti za kijamii, ripoti za utafiti, UNICEF, USAID, kanzidata za Benki ya Dunia, sera za kitaifa, majarida ya kitaaluma, vitabu vya rejea, mapitio ya maandiko, n.k.[28] Mbali na taarifa ya idadi za watu kama vile umri, hali ya ulemavu, mapato, kiwango cha elimu, dini, kabila, n.k, vyanzo vya data za upili zinaweza kutoa taarifa juu ya vikoa vitano vya GESI katika sekta zote. Data za upili zinaweza kutumika katika kukusanya data za msingi, kubainisha hali, changamoto, na visababishi vya nje ambavyo vinaweza kuathiri utekelezaji na utendaji wenye muitikio wa GESI.[29] Pia, waweza pia kukusanya taarifa za namna ambavyo programu zinazofanana na hii zilishughulikia changamoto hizi.

### Hatua za kukusanya data za upili:[30]

1. Bainisha mada yako, madhumuni ya kukusanya data, na aina ya taarifa unazohitaji ili kujibu maswali yako na kufikia lengo lako.
2. Angalia vyanzo vya data vilivyopo, bainisha ni nani anaweza kuwa alishakusanya data unazoihitaji. Mahali pazuri pa kuanzia ni kwenye ripoti na data za shirika la World Vision, nyaraka za serikali, takwimu rasmi na data kutoka kwenye mashirika ya maendeleo ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia, UNDP, FAO, WHO, ICRW, n.k. Kama unatafuta data za eneo husika, waweza kulazimika kuzitafuta kwenye ripoti za mashirika yasiyo ya kiserikali na machapisho mengine.
3. Zingatia sana kukusanya data zilizogawanywa kwa jinsi, hali ya ulemavu, umri, na sifa zingine za kijamii.
4. Amua jinsi unavyoweza kupata data unazohitaji.

28 USAID (2014a). Toolkit for Monitoring and Evaluating Gender-Based Violence Interventions.
29 USAID (2019). Data Collection Methods and Tools.
30 CARE (2005). Tips for Collecting, Reviewing, and Analyzing Secondary Data.

**Jedwali 8 | Maswali ya Mwongozo ya Ukusanyaji wa Data za Upili**

| Swali | Kikoa cha GESI |
|---|---|
| 1. Je, kuna takwimu zilizopo ambazo zinaonyesha tofauti zinazohusiana na GESI kwenye upataji na ufikiaji au ufanyaji maamuzi kuhusu rasilimali na huduma? | Upataji na ufikiaji<br>Ufanyaji Maamuzi |
| 2. Je, wanawake wana hali ya chini kulinganisha na wanaume? Kama ndiyo, ni kwa namna gani? (mfano, takwimu juu ya kiwango cha elimu/usomi na afya)? | Ushiriki |
| 3. Je, watu wenye ulemavu au makundi ya kijamii yanayokandamizwa wametengwa zaidi? na kama ndiyo, ni kwa namna gani? | Ushiriki<br>Upataji na ufikiaji |
| 4. Je, data kutokana na Maswali ya Kikundi cha Washington[31] zimekusanywa kwa ajili ya nchi na matokeo ni yapi? (kuwepo kwa watu wenye ulemavu na hali nyingine) kama watu wenye ulemavu wa uoni, kusikia, kutembea, kumbukumbu na kuwasiliana kwa lugha yao ya kimila? | Ustawi<br>Ushiriki |
| 5. Je, sera za kitaifa (mfano sera ya kitaifa ya wanawake na jinsia, sera ya walemavu, sera ya ustawi wa mtoto) zinalenga kwenye maeneo gani? ni viashiria vipi vinatumiwa? | Mifumo |
| 6. Je, kuna tofauti kati ya takwimu za nchi na sera za nchi za usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii? | Mifumo |
| 7. Je, kuna tofauti zozote za kijiografia za GESI na maeneo yenye mazingira hatarishi ambazo zimebainishwa kwenye nchi na zingeweza kuathiri usanifu na utekelezaji wa programu? | Ustawi |
| 8. Je, sera za nchi zinahusisha jamii? kivipi? sera zimemhusisha nani? | Mifumo |
| 9. Je, kuna aina yoyote ya desturi za kijamii zinazotenga wengine kwenye sera za nchi? | Mifumo |

Ifuatayo ni mifano miwili ya data za upili za GESI unazoweza kukusanya.

## Mfano 1: Data za Upili Kuhusu Ustawi

Taarifa za ustawi wa wanajamii zinaweza kupatikana kutoka kwenye vyanzo vya data za upili kama vile sensa, tafiti za jamii, ripoti za wizara za serikali, na ripoti nyingine za utafiti. Jedwali hapa chini linaweza kukuongoza unapokuwa unakusanya data za upili zinazohusu ustawi, ambacho ni kikoa cha GESI cha shirika la World Vision. Unaweza kukusanya data kwa ajili ya wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Ongeza safu wima kwa ajili ya walio katika mazingira hatarishi kadiri unavyohitaji.

31 For more information on the Washington questions please visit www.washingtongroup-disability.com/washington-group-question-sets/short-set-of-disability-questions

**Jedwali 9 | Data za Upili Kuhusu Ustawi**

| | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Watu wenye ulemavu |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. Ustawi wa Vitu na Mali** | | | | | |
| 1. Mgawanyo wa umri | | | | | |
| 2. Kiwango cha elimu | | | | | |
| 3. Wastani wa kipato | | | | | |
| 4. Ajira | | | | | |
| 5. Usalama wa chakula | | | | | |
| 6. Ubora wa makazi | | | | | |
| 7. Upataji na ufikiaji wa huduma zenye ubora mfano afya,elimu,maji | | | | | |
| | | | | | |
| **B. Ustawi Kimahusiano** | | | | | |
| 1. Familia isiyo yumba | | | | | |
| 2. Kuwa kwenye kikundi cha dini | | | | | |
| 3. Kutendewa uhalifu/ukatili | | | | | |
| 4. Kujisikia salama kwenye kaya na jamii | | | | | |
| 5. Viwango vya kujiua | | | | | |
| 6. Kupata ulinzi wakati wa dharura | | | | | |
| | | | | | |
| **C. Ustawi Kimtazamo** | | | | | |
| 1. Kujisikia kuwezeshwa | | | | | |
| 2. Kujisikia kuthaminiwa na kuheshimiwa | | | | | |
| 3. Kujiamini | | | | | |
| | | | | | |

## Mfano 2 | Data za Upili Kuhusu Desturi za Kijinsia na Kijamii

Data za upili kuhusu desturi za kijinsia na kijamii zinaweza kupatikana kwenye tafiti za kaya zilizofanywa na taasisi mbalimbali ikiwemo Tafiti za Demografia na Afya, Tafiti za UNICEF za Viashiria Mbalimbali na Tafiti za Benki ya Dunia za Kupima Hali ya Maisha (*Living Standards Measurements Survey*). Mara nyingi tafiti za taasisi hizo hufanywa kwa ubia na serikali za nchi na hutoa data zenye mgawanyiko wa jinsi, jamii, na sifa za kidemografia (kama vile, umri, kipato, kiwango cha elimu, n.k) zilizokuswanywa kutoka kwenye sampuli kubwa.[32] Kwenye jedwali hapa chini, ODI(2015) ametoa muhtasari wa data zinazopatikana kuhusu desturi za kijinsia na kijamii kutoka kwenye tafiti mbalimbali za kaya zilizofanywa na taasisi hizi za kimataifa.

**Jedwali 10 | Muhtasari wa Data Zilizopo Kuhusu Desturi za Kijinsia na Kijamii Kutoka kwenye Tafiti Kubwa za Kaya [33]**

| Aina ya tafiti | Mila na tamaduni kandamizi | Mikakati ya maamuzi ya maisha | Matumizi ya rasilimali |
|---|---|---|---|
| 1. Tafiti za Viashiria Mbalimbali | Ndoa za utotoni/kuzaa utotoni<br>Ukeketaji<br>Ukatili wa kijinsia (mtazamo kuhusiana na hili) | Mafanikio kielimu (yamegawanya kwa jinsi)<br>Tofauti za kiumri na kielimu kwa wanandoa<br>Tabia za kutafuta huduma za afya | Umiliki wa makazi, ardhi ya kilimo, mifugo (imegawanywa kwa jinsi) |
| 2. Tafiti za Demografia na Afya | Ukeketaji<br>Ukatili wa kijinsia (mtazamo kuhusiana na hili)<br>Ndoa za utotoni/kuzaa utotoni | Mafanikio kielimu Ajira na kazi<br>Uzazi wa mpango<br>Maoni ya wanawake kama mwanamke ana uwezo wa kukataa kufanya tendo la ndoa na mume wake<br>Changamoto wanazopata wanawake katika kupata na kufikia huduma za afya<br>Uhuru wa kwenda popote | Umiliki wa rasilimali<br>Udhibiti wa kipato kwa mtu binafsi<br>Tofauti za umri na kiwango cha elimu kwa wanandoa<br>Ushikiri wa wanawake katika kufanya maamuzi kwenye kaya |
| 3. Tafiti za Kupima Hali ya Maisha | | Mafanikio kielimu (pamoja na swali maalum la kwa nini mtoto haendi shule)<br>Je, mfanya maamuzi mkuu kwenye familia ni nani? | Maamuzi kuhusu matumizi ya rasilimali zilizopatikana kama "kipato cha ziada" |

32 ODI (2015). What Can Internationally Comparable Quantitative Data Tell Us About How Gender Norms are Changing?
33 ODI (2015).What Can Internationally Comparable Quantitative Data Tell Us About How Gender Norms Are Changing?

## Hatua 3 | Ukusanyaji wa Data za Msingi wenye Muitikio wa GESI

Kuna aina mbalimbali za njia ambazo unaweza kuzitumia kukusanya data za msingi. Njia zinazotumika sana ni pamoja na tafiti za kaya, Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL), mahojiano na watu muhimu, mahojiano ya kina, na ushuhudiaji (wa kushiriki au kutazama bila kushiriki). Njia hizi huwawezesha watendaji kuelewa sababu za muktadha ambazo zinaathiri maisha ya makundi ya kijamii yanayotengwa na kuzishughulikia kupitia afua za mradi. Hatua hii inatumia mifano kutoka kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) na tafiti za kaya. Kabla hujatumia njia hizi zingatia masuala yaliyotajwa kwenye Jedwali 11 maana yataongeza uwezekano wa kukusanya data zenye muitikio wa GESI.

**Jedwali 11 | Mipango ya Kukusanya Data zenye Muitikio wa GESI**

| Mambo ya kuzingatia | Sababu | Mfano |
|---|---|---|
| 1. Bainisha malengo ya kukusanya data zenye muitikio wa GESI (takribani 2-3) | Kusaidia ufanyaji maamuzi kuhusu jinsi ya kushughulikia masuala ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. | • Kama programu inalenga kuwalinda watoto wanaoishi kwenye maeneo yaliyokumbwa na dharura, lengo la kukusanya data linaweza kuwa ni kuelewa jinsi wavulana na wasichana wanapata na kufikia huduma muhimu.<br>• Kama programu inalenga kuboresha uhakika wa kupata chakula, lengo la kukusanya data linaweza kuwa ni kuangalia jinsi desturi za kijinsia na kijamii zinavyoweza kuathiri ufanyaji maamuzi juu ya matumizi ya chakula unavyoweza kufanyika. |
| 2. Tambua washiriki walipo na vyanzo vya data | Wakilisha makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. | • Kusanya data kutoka kwa watu walio na uhusiano na washiriki. Mfano, kwa miradi inayowalenga watoto, wahusishe wazazi na walimu kama watoa taarifa muhimu.<br>• Hata hivyo, watoa taarifa muhimu wasichukue nafasi ya makundi ya wale walio katika mazingira hatarishi, mfano, watu wenye ulemavu. |
| 3. Panga kugawanya data | Inajenga uelewa kamili wa washiriki na jinsi ya kushughulikia mahitaji yao ya kipekee. | • Mgawanyiko wa data unatakiwa kujumuisha tofauti za kijinsia na sifa za kijamii.<br>• Kwa mfano, unapohoji kaya zinazoongozwa na wanawake, onyesha mgawanyiko kwa jinsi, umri, hali ya hali ya ulemavu, n.k. |
| 4. Chagua mbinu | Zinapaswa zishabihiane na malengo na zitofautiane kulingana na aina ya washiriki. | • Mikabala yenye muitikio wa GESI inaunga mkono mbinu za uchangamani, kwa kutumia methodolojia za ukusanyaji data na uchanganuzi wa data za kitaamuli na kitakwimu unaofaa kwa ajili ya kundi lengwa.<br>• Oanisha mbinu za programu na malengo ya kukusanya data. |
| 5. Zingatia athari na vikwazo vya kimaadili vinavyoweza kutokea | Kujumuisha hatua na tahadhari za kulinda haki, utu na ustawi wa watafitiwa. | • Endapo haikubaliki kimila kwa mtafiti wa kiume kumhoji mwanamke nyumbani kwake, badilisha mahali pakufanyia mahojiano, au badilisha atakaye endesha mahojiano/mwezeshaji, au badilisha mbinu ya kukusanya data. |
| 6. Fanya jaribio kabla ya kufanya utafiti halisi | Kuamua kama mbinu na maswali yanafaa kwa wahusika. | • Jaribio kabla ya kufanya utafiti halisi lifanane na mazingira halisi ya ukusanyaji wa data, ingawa litafanyika kwenye mawanda madogo.<br>• Pia ni fursa ya kufanya majaribio ya awali ya zana kwa makundi ya watu mahususi, pale inapofaa, kama vile watu wenye ulemavu. |

## MAJADILIANO YA VIKUNDI LENGWA (MVL)

Kuna aina 4 za Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) yanayoweza kufanyika peke yake au kwa pamoja, kulingana na kiwango cha taarifa zinazohitajika:

**MVL 1:** husaidia kuelewa mazingira hatarishi.

**MVL 2:** utambuzi wa jamii ni zana ya kuelewa ngazi mbalimbali za upataji na ufikiaji, na udhibiti wa rasimali na huduma kati ya makundi mbalimbali ya watu (wanaume, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, na watu wengine waliotengwa). Hii inasaidia kubaini shughuli ambazo makundi mbalimbali ya watu hutumia muda wao mwingi na namna ambayo wanasafiri. Hii inaweza kubaini mikakati ya kuboresha uwezo wa watu wanaokandamizwa au wasio husishwa kupata, kufikia na kudhibiti rasimali na huduma kwa kuhakikisha ushiriki wa watu wasiohusishwa kwenye mradi na faida za miradi. Inasaidia pia kubaini maeneo sahihi kwa ajili ya mafunzo.

**MVL 3:** ni uchanganuzi wa majukumu na ukubwa wa kazi ili kuwasaidia wafanyakazi wa programu (na washiriki) kubaini nani anafanya shughuli ipi na jinsi ambavyo wanatumia muda wao kila siku.

**MVL 4:** ni tathmini ya desturi za kijinsia na kijamii.

## NANI HUSHIKIRIKI?

- Timu ya mradi
- Wafanyakazi wa mradi
- Wanajamii
- Wafanyakazi wa maendeleoya jamii
- Watafiti

Kwa kila moja ya aina nne za MVL hapo juu, fanya angalau majadiliano manne tofauti (16 jumla). Aina ya watu ambao wanapaswa kushiriki katika kila majadiliano hutegemea muktadha na wanaweza kupangwa kwa njia tofauti tofauti. Hata hivyo, inashauriwa kwamba kundi mojawapo liwe la wanawake peke yao (hakikisha kwamba wanawake walioolewa na wanawake ambao ni wakuu wa kaya/viongozi wa familia wanakuwepo). Pia uwe na kundi la wanaume peke yao (hakikisha wanaume ambao hawajaoa wanakuwepo); kundi la walemavu (hakikisha jinsi zote zimewakilishwa) na kundi moja lenye vijana (mchanganyiko wa jinsi). Ikiwa rasilimali, muda na bajeti inaruhusu, kundi la vijana linaweza kugawanywa kulingana na hali ya ulemavu.

Lazima isisitizwe kuwa haya ni maoni tu. Aina ya watu wanaopaswa kushiriki kwenye kila mjadala hutegemea muktadha. Ni muhimu kuangalia mawazo yako (kwa mfano, kikundi cha vijana wa jinsia tofauti bado kina mienendo ya kijinsia inayotakiwa kuzingatiwa).

Baadhi ya zana za MVL hapa chini ni vielelezo (kama vile ramani ya kijamii, utambuzi wa sehemu waendazo watu, na ratiba ya shughuli za kila siku) ambazo huongeza ushiriki na uchangiaji katika mjadala kwa washiriki wengi. Kwa mfano, zana hizo zinaweza pia kuongeza uelewa wa washiriki kuhusu masuala yanayojadiliwa.

Hata hivyo mwezeshaji anapaswa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wana vifaa vya ziada na usaidizi unaohitajika kama vile, wakalimani wa lugha ya alama maana vielelezo vinavyoonekana kwa macho peke yake havitoshi.

**Kidokezo!**

Kama Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) hayakidhi mahitaji yako au unataka tu kutafiti kwa kutumia zana nyingine, tazama Kijitabu cha Uchanganuzi wa Kijamii na Juhudi za Utekelezaji-hususani Kisanduku cha zana ya Jinsia ya shirika la CARE (CARE's *Social Analysis and Action Implementation Manual).*

# Hatua 4 | Uchanganuzi wa Data na Uandishi wa Ripoti wenye Muitikio wa GESI

## Kuchanganua Data za MVL

Rejea ZANA 4.3 kwa ajili ya mwongozo zaidi. Kuchanganua data kutoka kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) ni kama kuchanganua data za aina nyingine kama vile usaili wa mtu mmojammoja. Kwa kila aina nne za MVL hapo juu, mchakato ufuatao unaweza kufuatwa:

a. Hakikisha maoni yote kutoka kwa MVL yamebadilishwa kutoka kwenye sauti na kuwekwa kwenye maandishi.
b. Chambua maoni kutoka kwenye MVL mbalimbali juu ya kila swali (kwa mfano, kwa swali 1, maoni kutoka kwa MVL vya wanawake tu na MVL vya wanaume tu yanapaswa kuunganishwa chini ya kichwa cha 'swali la1').
c. Kwa kila swali, angalia maoni makuu yanayojitokeza kwenye majadiliano ya majibu.
d. Angalia ni maoni gani makuu yanajitokeza mara kwa mara. Kumbuka kwamba wakati mwingine mawazo yaleyale hutokea kwenye majibu ya maswali tofauti.
e. Fikiria kwa kina juu ya maoni yanayojirudia ili kubaini mada. Mada inaweza kuhusisha maoni mbalimbali.
f. Baini nukuu ambazo zinatoa muhtasari bora kwa kila mada.
g. Tumia nukuu hizi kuandika masimulizi yanayoshirikisha na yaliyooana kuhusu mada.
h. Ikiwa Hatua 1 na 2 za mwongozo huu zimekamilika, weka majadiliano ya jinsi mada hizi zinavyofanana (au tofauti) kutoka kwenye matokeo kwenye Hatua1 na 2.

## MVL 1: Kuelewa Mazingira Hatarishi

Majadiliano haya yanahusika na kukusanya data kuhusu mazingira hatarishi kwa baadhi ya makundi ya kijamii na sababu ambazo zinaweza kuathiri ushiriki wao katika mradi, au fursa zao. Zana hii inajumuisha mwongozo wa hatua kwa hatua ambao unaelezea jinsi ya kutambua makundi na watu walio katika mazingira hatarishi. Lengo ni kubaini makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kwenye jamii; kuelewa kiasi na kiwango cha mazingira hatarishi au kutohusishwa kwa baadhi ya makundi ya watu; kutafuta makundi yaliyo katika mazingira hatarishi au yasiyohusishwa kwa mahojiano na walengwa, na kuhamasisha majadiliano juu ya sababu na aina za mazingira hatarishi na kutohusishwa.

**Maelekezo**
Andika umri, jinsi, hali ya ulemavu, hali ya ndoa, lugha mama na dini ya kila mshiriki wa kundi. Hakuna haja ya kuandika majina yao.

**Vifaa vinavyohitajika:** Chati mgeuzo, kalamu za wino mzito na shanga au mawe, ramani ya kijamii
**Watu wanaohitajika:** Mwezeshaji mmoja, mchukua vitini mmoja na mshuhudiaji mmoja
**Muda:** Saa 1.5 – 2
**Viburudisho:** Maji, juisi, au vitafunwa kadiri itakavyofaa- Majadiliano ya Vikundi Lengwa yanaweza kuwa marefu yanaweza kuwachosha washiriki

## Jinsi ya Kutumia Zana Hii

Zana hii inahusisha mwongozo wa hatua kwa hatua ambao unaelezea namna ya kubaini makundi na watu walio katika mazingira hatarishi. Hata hivyo, kuna hatua muhimu za kuzingatia kabla na wakati wa kukusanya data. Kabla ya kutumia zana hii, timu ya utafiti inatakiwa kurejea matokeo ya hatua ya 1 na ya 2 kubaini makundi kwa ajili ya Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL).

## Mwongozo wa Hatua kwa Hatua

1. Waulize washiriki kuwa jamii yao inafasilije kuwa katika mazingira hatarishi. Hii itaweka msimamo kwenye akili za watu na kufikiria kwa usahihi. Andika fasili hii.

2. Weka chati mgeuzo chini. Chora visanduku vitatu tofauti (kuwasilisha walio katika mazingira hatarishi kwenye jamii zao) kwenye karatasi.

3. Kulingana na fasili yao ya 'kuwa katika mazingira hatarishi', wadadisi washiriki wakuambie vigezo wanavyotumia kuwaweka watu 'kundi la kuwa katika mazingira hatarishi' na 'kutokuwa katika mazingira hatarishi.' Kisha waambie wawape sifa watu walio katika mazingira hatarishi' na 'wasio katika mazingira hatarishi' kwenye jamii yao. Angalia kwa makini sababu zinazofanana na zinazotofautiana na uziandike kwenye vitini vyako. Hii itasaidia:

    a. Waulize washiriki kuwa jamii yao inafasilije kuwa katika mazingira hatarishi. Hii itaweka msimamo kwenye akili za watu na kufikiria kwa usahihi. Andika fasili hii.

    b. Weka chati mgeuzo chini. Chora visanduku vitatu tofauti (kuwasilisha walio katika mazingira hatarishi kwenye jamii zao) kwenye karatasi.

    c. Kulingana na fasili yao ya 'kuwa katika mazingira hatarishi', wadadisi washiriki wakuambie vigezo wanavyotumia kuwaweka watu 'kundi la kuwa katika mazingira hatarishi' na 'kutokuwa katika mazingira hatarishi.' Kisha waambie wawape sifa watu walio katika mazingira hatarishi' na 'wasio katika mazingira hatarishi' kwenye jamii yao. Angalia kwa makini sababu zinazofanana na zinazotofautiana na uziandike kwenye vitini vyako. Hii itasaidia:

4. Waulize washiriki kwa nini makundi haya yako katika mazingira hatarishi. Uliza swali hili kwenye kila kundi (mfano ni kwa nini watu wenye ulemavu wako katika mazingira hatarishi?)

5. Wape washiriki shanga 10 na waambie wakisie uwiano wa 'kuwa katika mazingira hatarishi zaidi', 'kuwa katika mazingira hatarishi,' na 'kutokuwa katika mazingira hatarishi' kwenye jamii yao kwa kugawanya shanga kwenye kila kundi. Hii inapaswa itanguliwe na maelezo ya sifa kwa washiriki kulingana na sifa za kila kundi lililoelezewa na washiriki.

6. Dodosa kuhusu mazingira hatarishi kwa kigezo cha usalama wa chakula,upataji na ufikiaji wa elimu, afya, vyanzo vya maji,ulinzi wa kijamii, kuwa katika mazingira hatarishi au matatizo ya hali ya hewa, majanga ya asili,uhaba wa ardhi,uwezo na idadi ya watoto, n.k. Zingatia kwamba sifa zilizopo kweney hatua iliyopita zinaweza kuwa mazingira hatarishi kati ya na juu yao.

    a. Hii itakufanya uelewe changamoto na fursa walizonazo makundi mbalimbali ya kijamii katika kupata rasilimali na huduma mbalimbali.

    b. Kutoka katika mazingira hatarishi kulikobainishwa-waulize washiriki yapi yanaonekana kuwa ni vikwazo cha usalama wa kijamii. Vibainishe.

7. Waambie washiriki wabainishe familia 10 ambazo ziko katika mazingira hatarishi zaidi kwenye jamii yao na mahali zilipo familia hizi 10 kwenye jamii (pia zingatia jinsi,hali ya ndoa, umri, tabaka n.k.) kulingana na sifa na kigezo cha kuwa katika mazingira hatarishi zilizojadiliwa kwenye hatua iliyopita.

8. Waulize washiriki ni kundi lipi (katika mazingira hatarishi zaidi, katika mazingira hatarishi, kutokuwa katika mazingira hatarishi) ambalo mara nyingi huhusishwa kwenye jitihada za maendeleo au ulinzi wa kijamii. Waulize sababu.

9. Waambie washiriki wajadili namna ambavyo kila kundi lililo katika mazingira hatarishi linaweza kushiriki, kuhusishwa na kulengwa kwenye afua.

10. Waulize washiriki ni kwa namna gani na njia gani makundi yaliyo katika mazingira hatarishi au yasiyohusishwa yanaweza kunufaika na mradi.

11. Panaweza kuwa na maswali yayonafanana na maswali hayo hapo juu, au kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) yanayofuata, au ngazi mbalimbali za kuhusika kwa washiriki. Hii ni sawa, hakikisha tu watu wote wanaendelea kuhusishwa na kuielewa shughuli mnayofanya. Usisite kuchukua na kuacha baadhi ya maswali ambayo hayana umuhimu. Hakikisha mjadala unaendelea.

12. Kamilisha jedwali hapa chini kwa pamoja kwa kuwa sasa umefikiria na kujadili kwa kina zaidi kuhusu mazingira hatarishi.
    a. Onyesha kwenye matriki ya chati mgeuzo na waambie washiriki wajaze matriki kwa pamoja (sifa ya kuwa kwenye kundi la mazingira hatarishi, sababu za kuwa kwenye kundi, watu kwenye kila kundi, sifa za kundi n.k.). Kutokana na mjadala wenu, waelekeze washiriki wajaze matriki hapo chini kama matokeo au muhtasari wa taarifa iliyokusanywa kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL)1.
    b. Hii itakusaidia kuelewa taarifa ulizonazo tayari na kufahamu unahitaji taarifa gani zingine kutokana na tathmini ya ufuatiliaji wa GESI.
    c. Tena, hii inakuwezesha kuwa na uelewa halisi wa namna utakavyoweza kuhusisha na kushughulikia ukosefu wa uhusishaji kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kwa kuwalenga kwenye miradi kama washiriki.

**Jedwali 12 | Viwango vya Mazingira Hatarishi**

| Kundi la mazingira hatarishi | Sifa ya kundi inayotofautisha viwango vyao vya upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, fursa na ustawi | Sababu za kuwa katika mazingira hatarishi | Uwiano wa kila kundi kwenye jamii | Hao watu ni akina nani/ familia zipi? | Mapendekezo ya mikakati ya kuwezesha kujumisha watu walio katika mazingira hatarishi kwenye mradi na kuboresha ushiriki wao kadri iwezekanavyo |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. Wako katika mazingira hatarishi zaidi** | | | | | |
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| **B. Wako katika mazingira hatarishi** | | | | | |
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3 | | | | | |
| **C. Hawako katika mazingira hatarishi** | | | | | |
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3. | | | | | |

Kidokezo!

Wakati wa majadiliano ya vikundi lengwa unaweza kuangalia maneno ambayo wanajamii wanayatumia kuelezea baadhi ya makundi ya watu maana maneno hayo yanaweza kuwa na lugha ya dharau au kibaguzi. Sehemu ya mwongozo wako inatakiwa ijumuishe utumiaji wa lugha inayoheshimu wengine.

## MVL2: Ramani ya Kijamii

Majadiliano haya husaidia kuelewa upataji na ufikiaji na kumiliki rasilimali na huduma kwa makundi mbalimbali na watu binafsi. Na pia inasaidia kuelewa uwezo wa kutembea wa makundi mbalimbali ya kijamii kwa kutengeneza ramani ya kijamii.[34] Wakati unaandaa ramani ya kijamii, zana hii inasaidia kuendesha majadiliano kuhusu mamlaka, jinsia na desturi za kijamii na kuwadodosa washiriki kuhusu uwezo wao wa kufanya maamuzi juu ya rasilimali na huduma muhimu. Data zilizopatikana kupitia Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) zinaweza kuwa muhimu kwa kusaidia kulenga makundi ya kijamii yaliyo katika mazingira hatarishi kwa ajili ya afua za mradi, kama vile, mafunzo au mikutano na kuongeza ushiriki na manufaa ya watu waliokandamizwa na walio katika mazingira hatarishi katika mradi. Pia hii itahakikisha upataji na ufikiaji wao, na udhibiti wa rasilimali muhimu na kuboreshwa kwa huduma.

**Malengo**

- Kutathmini tofauti za upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma muhimu kwa watu wa makundi mbalimbali ya kijamii (wanawake, wanaume, wavulana na wasichana, watu wenye ulemavu n.k.)
- Kutathmini udhibiti wao wa rasilimali na huduma hizo muhimu
- Kubaini sababu (zinazohusiana na desturi za kijamii na miundo isiyo na usawa) zinazosababisha tofauti katika upataji na ufikiaji, na udhibiti wa rasilimali na huduma
- Kubaini fursa na changamoto katika kuhakikisha uwepo wa usawa kwenye upataji na ufikiaji na udhibiti wa rasilimali na huduma kwa makundi mbalimbali ya kijamii
- Kubaini shughuli na afua zinaimarisha usawa wa fursa katika makundi mbalimbali ya kijamii (wanawake,wanaume,wavulana na wasichana, watu wenye ulemavu n.k)

**Maelekezo**

Andika umri,jinsi,hali ya ulemavu, hali ya ndoa, lugha mama na dini ya kila mshiriki wa kundi. Hakuna haja ya kuandika majina yao.

Kama washiriki wamegawanyika kwenye makundi kwa jinsi, majadiliano yanaweza kulenga kwenye kutengeneza ramani ya kijamii kwa mitazamo ya wanaume na wanawake, namna ambavyo hii itakuwa tofauti na makundi yaliyo kinyume chake, ni tofauti zipi na kwa nini. Kama makundi yamegawanya kwa umri au waliooa/olewa na ambao hawajaoa/olewa, MVL yanaweza kuanzishwa ili kuwa na majadiliano juu ya ramani zinazo kinzana.

Japokuwa majadiliano haya yana uwezo mkubwa wa kuongeza ushiriki na uelewa wa washiriki kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii (watu wasiojua kusoma, wenye ulemavu kama vile ulemavu wa kusikia,kukumbuka) zana hii si rafiki kwa watu wenye changamoto ya kuona. Hivyo ili kuhakikisha zana hii inahusisha watu wenye ulemavu wa kuona wakati wa kuandaa ramani ya kijamii, mwezeshaji anapaswa kuhakikisha kuwa watu hawa wanasaidiwa kwa kuelezea kila hatua kwa kina. Zaidi ya hapo, wanapaswa kupewa nafasi ya kuelezea uzoefu wao namna wanavyopata rasilimali na huduma mbalimbali zilizotajwa wakati wa majadiliano (kutengeneza ramani kwa mazungumzo). Ramani ya kijamii huisaidia wanajamii kuelewa maeneo yanayohitaji mabadiliko na jinsi ya kupanga mipango kwa ajili ya mabadiliko hayo.

**Vifaa vinavyohitajika:** Chati mgeuzo,kadi,kalamu ya wino mzito,majivu/chaki (ikiwa ramani imechorwa chini)
**Rasilimali watu inayohitajika:** Mwezeshaji mmoja na mchukua vitini mmoja
**Muda:** Saa 1.5
**Viburudisho**: Maji, juisi, chakula kinachofaa kulingana na mazingira na aina ya washiriki



34 CARE USA (2018). Social Analysis and Action Global Implementation Manual.

## Mwongozo wa Hatua kwa Hatua

1. Eleza madhumuni ya majadiliano na jibu maswali yote ya awali. Wapatie watu nafasi ya kujiengua kwenye majadiliano kutokana na ufafanuzi wako. Hakikisha kila mtu anaelewa nini kitafanyika na matokeo yake yatakuwa ni yapi.

2. Waombe washiriki wa Majadiliano ya Kikundi Lengwa (MKL) wachore ramani ya kijamii na ramani ya jinsi watu wanavyozunguka/tembea kwenye jamii

    a. Chagua mtu mmoja au wawili wajitolee kuchora ramani. Ijapokuwa washiriki hawa wawili watachora ramani halisi, wengine watashiriki kuchora kwa kutoa maoni na kuonyesha maeneo maalumu ya rasilimali na huduma kwenye ramani.

    b. Kwanza waambie washiriki wachore ramani/mipaka ya jamii chini au kwenye chati mgeuzo. Ni muhimu kuanzia kwenye eneo ambalo mkutano unafanyikia kama rejea au alama kuu kama vile barabara inayoelekea kijijini.

    c. Baada ya kukamilisha kuchora ramani (au mipaka ya jamii) waambie washiriki wachore/ waonyeshe miundombinu muhimu (kama vile barabara,mifereji ya maji na n.k.), taasisi (kama vile kituo cha afya,mashule,ofisi za serikali ya mtaa n.k.) na huduma/rasilimali za jamii (kama vile vyanzo vya maji vya umma, misitu, nyaya za umeme, soko,maduka,vituo vya kidini, n.k.) kwa kutumia alama au picha.

    d. Kisha waulize washirikini maeneo yapi ambayo huwa wanatembelea? (inaweza kuwa visimani,kwenye mito, baa za kienyeji,vituo vya tiba, kanisa, bustani, mikutano ya kijamii,mashule, kambi za kichifu, masoko n.k. au yanaweza kuwa ni majina ya miji iliyoko jirani).

        – Kisha uliza, ni watu wangapi hutembelea sehemu hizi kila mwezi na sababu za matembezi hayo

        - Tumia mistari ya aina mbalimbali (kama vile vinukta/vidoti,vimistari,rangi za aina mbalimbali) kuonyesha madhumuni na idadi ya ziara/matembezi mfano mstari uliokolezwa wino unamaanisha mara nyingi, mstari wenye wino mwepesi unamaanisha mara kwa mara na mstari wa vinukta/vidoti unamaanisha mara chache sana.

    e. Baada ya kuikamilisha ramani ya kijamii, muombe mshiriki mmoja aielezee ramani hiyo kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu rasilimali za umma na huduma zilizopo kwenye jamii kwa kurejelea ramani ya kijamii waliyoitengeneza. Pia, wape nafasi ya kuongeza rasilimali na huduma yoyote ambayo walikuwa wamesahau kuiweka

3. Waambie washiriki waitathmini ramani hiyo kwa jozi (wawili wawili). Mtu mmoja anauliza maswali na mwingine anajibu. Zingatia vigezo vyovyote vinavyofaa kwa ajili ya kuwagawa watu kwenye jozi (mfano wanaume na wanawake, watu wenye ulemavu na watu wasio na ulemavu).

    a. Weka ramani ya kijamii sehemu ambayo kila mtu anaweza kuiona na kuitumia kama rejelea wakati wanaendelea na majadiliano.

    b. Waulize washiriki kuhusu uwezo wao wa kupata, kufikia na kudhibiti rasilimali na huduma zilizotajwa kwenye ramani ya kijamii.

    c. Waulize washiriki ni sehemu/huduma na rasilimali gani ambazo hazipatikani kwa kundi maalumu (mfano wanaume/wanawake,wasichana/wavulana/ watu wenye ulemavu)? kwa nini?

    d. Je, kuna maeneo maalumu ambayo wanajamii maalumu wanaishi? Je, wanakumbana na aina yoyote ya ubaguzi?

4. Waonyeshe ramani kwa pamoja na waulize:

    a. Watu walio katika mazingira hatarishi kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa(MVL) 1 wanaweza kupatikana wapi?

    b. Kulingana na taarifa iliyotolewa, ni mahali gani watu hawa wanaweza kujisikia vizuri zaidi kushiriki, kama vile kwenye mafunzo na warsha.

    c . Je, ni mahali gani matangazo ya mikutano ya jamii au mradi yanapaswa kuwekwa ili kuyafikia makundi haya ya watu?

5. Waulize washiriki kuhusu ushiriki na uwezo wao wa kufanya maamuzi kuhusu rasilimali na huduma zilizotajwa kwenye ramani ya kijamii
    a. Onyesha matriki hapa chini kwenye bango kitita lililoko sakafuni.
    b. Chagua rasilimali, taasisi na miradi mingine na huduma za jamii zilizobainishwa kwenye ramani ya kijamii na ziandike kwenye matriki.
    c. Waambie washiriki waonyeshe rasilimali na huduma tano amazo ni vipaumbele kwao na ambazo ni muhimu kwa wao kuhusishwa kwenye mradi unaokusudiwa.
    d. Waambie washiriki wabainishe watu wenye mamlaka ya kufanya maamuzi kwa kila rasilimali,taasisi na huduma iliyotajwa. Wagawie washiriki mbegu 10[35] kama kundi, waambie wazigawe mbegu hizo 10 kwenye safu wima kulingana na uwezo wao wa ufanyaji wa maamuzi au kulingana na ambaye hufanya maamuzi mengi kuhusu rasilimali na huduma. Kundi ambalo halina uwezo wowote wa kufanya maamuzi wa rasilimali/huduma maalumu hawapata mbegu yoyote, na kundi lenye mamlaka yote ya kufanya maamuzi litapata mbegu 10.
6. Baada ya kila kundi kumaliza, andika muhtasari wa majibu yaliyojitokeza mara nyingi na yatumie kwenye mkakati wako lengwa.

**Kumbuka**: Unapokuwa unakusanya taarifa kuhusu upataji na ufikiaji, na udhibiti wa rasilimali na huduma, ni muhimu pia kudodosa na kupata maelezo ya kina kuhusu sababu za kijamii na kitamaduni zinazoweza kuathiri haya:[36]

- Sababu za kidemografia pamoja na watu walio kwenye kaya na ukuu wa kaya
- Hali za kiuchumi kwa ujumla, kama vile kiwango cha umaskini, kupanda na kushuka kwa thamani ya pesa, mgawanyo wa kipato na miundombinu
- Sababu za kitamaduni na kidini
- Viwango vya elimu
- Sababu za kisiasa, kitaasisi na kisheria kama sera za nchi zinazohusu umiliki wa kisheria wa mali na rasilimali (mfano uwezo wa wanawake kumiliki mali kisheria bila ruhusa ya mwanaume, umiliiki wa pamoja, uwezo wa kufanya maamuzi juu ya mali); sera za nchi zinazohusu wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi juu ya upataji na ufikiaji wa ardhi, maji na rasilimali zingine; sera za nchi kuhusiana na urithi; haki ya kupata huduma kama vile afya, elimu n.k.



35 Adapted from Jayarakan (2002). The Ten Seeds Technique.
36 Srinivas (2015). Towards A Gender Analysis Framework.

**Jedwali 13 | Ramani ya Kijamii**

| | Upatikanaji na Ufikiaji | | | | Udhibiti | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana |
| | | | | | | | | |
| **A. Rasilinali** | | | | | | | | |
| 1. Ardhi | | | | | | | | |
| 2. Vyanzo vya maji | | | | | | | | |
| 3. Teknolojia | | | | | | | | |
| 4. Mkopo | | | | | | | | |
| 5. Vifaa vya kilimo | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| **B. Huduma** | | | | | | | | |
| 1. Elimu | | | | | | | | |
| 2. Afya | | | | | | | | |
| 3. Usafi wa mazingira | | | | | | | | |
| 4. Huduma za ushauri na msaada wa kilimo | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

Kidokezo!

Mwezeshaji anatakiwa aamue kama washiriki watatengeneza ramani ya kijamii na watajadili huduma kwa ajili ya kundi lao wenyewe au kama watafanya vyote kwa ajili yao na kundi lingine (mfano ikiwa Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) ni ya wanawake tu, wanaweza kujadili kuhusu upataji na ufikiaji wa huduma na rasilimali mbalimbali za kijamii kwa ajili yao au na kwa ajili ya wanaume pia).

Ikiwa Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) ni ya watu wenye ulemavu, kwa ajili ya zoezi la kutengeneza ramani ya kijamii utatakiwa upange kuwapatia mahitaji kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wao.

Inawezekana kukawa na uhusiano kati ya maswali hapo juu au tofauti za uchangia hoja kutoka kwa washiriki. Hiyo ni sawa– hakikisha watu wanaendelea kuchangia mawazo yao na kwamba wameelewa zoezi lote kwa ujumla. Usisite kubadili au kuruka baadhi ya maswali kama hayahusiki. Wewe endeleza majadiliano tu!

## MVL3: Uchanganuzi wa Majukumu na Wingi wa Kazi

Majadiliano haya husaidia kubaini majukumu ya kijinsia na wingi wa kazi kwa makundi mbalimbali ya kijamii (wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine ya kijamii). Chati ya shughuli za kila siku ni zana inayowataka wanajamii kuchunguza aina mbalimbali za kazi/ shughuli zinazofanywa kwa siku na wingi wa majukumu kati ya wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine ya jamii. Vielelezo vya pande mbili vya majukumu na shughuli tofauti zinazofanywa na makundi tofauti ya kijamii katika siku ya kawaida huonyesha nani hufanya kazi masaa mengi zaidi, anayefanya shughuli ndogondogo, ambaye hugawanya muda wake kwenye shughuli nyingi mbalimbali, na ambaye ana muda zaidi wa kupumzika na kulala. Inaweza pia kuonyesha tofauti ya kazi za wanawake na za wanaume kulingana na msimu. Ili kufanya hivyo, unahitaji kufanya zoezi la kuangalia muda unaotumika kufanya shughuli mbalimbali kwa siku mara kadhaa kulingana na idadi ya misimu katika eneo hilo. Zana hii imechukuliwa kutoka ACDI VOCA (2012)[37] ana inaweza kutumiwa kuchunguza makundi ya kijamii zaidi ya yale yanalitofautishwa kijinsia. Unachotakiwa kufanya ni kuongeza safu wima kwenye jedwali hapa chini ili uongezee makundi mengine ya kijamii (kama watu wenye ulemavu).

**Lengo la Chati ya Shughuli za Kila Siku**

Kukusanya data kuhusu wanawake na wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu, na makundi mengine ya kijamii ambayo itatusaidia:

- Kuelewa majukumu mbalimbali na matumizi ya muda na kutathmini wingi wa kazi zao
- Kuelewa namna majukumu mbalimbali yanavyoathiri jinsi wanavyotumia muda wao na kushiriki katika programu
- Kutathmini vizuizi na fursa mbalimbali zinazoweza kuzuia au kuwezesha ushiriki wao na kufaidika na programu

**Maelekezo**

Andika umri, jinsi,hali ya ulemavu, hali ya ndoa, lugha mama, mahali au dini ya kila mshiriki wa mahojiano. Hakuna haja ya kuandika majina yao. Mwezeshaji anatakiwa kuamua namna ambavyo washiriki watagawanywa kwenye makundi ya majadiliano kulingana na muktadha wa eneo husika, kama vile wanawake-tu, kwa umri n.k. na ikiwa watu wenye ulemavu watakuwa na Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) peke yao au watachanganyika na watu wasio na ulemavu.

**Vifaa vinavyohitajika:** Mbegu/Mawe, bango kitita, kalamu ya wino mzito

**Muda:** Saa 1.5

**Rasilimali watu inayohitajika:** Mwezeshaji mmoja na mchukua vitini mmoja

**Viburudisho:** Juisi, maji na chakula. Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) yaweza kuwa ya muda mrefu na yenye kuchosha kama hapatakuwa na viburudisho



37 Meyers and Jones (2012). Gender Analysis, Assessment and Audit.

## Mwongozo wa Hatua kwa Hatua

Mwezeshaji anapaswa kuamua kama washiriki wanapaswa kugawanywa kwenye majadiliano ya vikundi kulingana na muktadha wa sehemu husika kama vile wanawake tu na wanaume tu, kwa umri n.k na kama watu wenye ulemavu watakuwa kwenye Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) tofauti au watachanganywa na watu wasio na ulemavu.

1. Waambie washiriki waorodheshe shughuli za wanawake na wanaume, wasichana na wavulana kwenye chati yao ya shughuli za kila siku.
    a. Chora duara mbili mapema kabisa ili kutengeneza " chati ya shughuli za kila siku"kwenye bango kitita au sakafuni.
    b. Waambie washiriki wajadili uhalisia wa jinsi siku yao ilivyo katika maisha ya wanawake,wanaume, wasichana, na wavulana kwenye kaya au jamii. Waambie kuwa utawaonyesha kazi zinazofanywa na wanawake,wanaume, wasichana na wavulana kwa siku nzima. Mwezeshaji anaweza kulazimika kufasili maana ya kazi za nyumbani ni nini.
        - Waulize washiriki walioko kwenye makundi ya wanawake kwamba mwanamke au msichana huwa anafanya kazi gani tangu anapoamka hadi anapokwenda kulala.
        - Kisha waambie kundi lingine (kundi la wanaume) kufanya vile vile kwa wanaume (mwanaume au mvulana huwa anafanya kazi gani tangu anapoamka hadi anapokwenda kulala).
    c. Mtu mmoja anaweza kukupatia muhtasari. Kisha utawaeleza wakuambie saa kwa saa. Kwa kutumia mshale wa "saa" kwenye bango kitita onyesha namna wanavyotumia kila saa ya siku yao kuanzia mawio hadi machweo. Jumuisha muda wa kustarehe na kupumzika, kazi yenye malipo na isiyo ya malipo.
    d. Wadadisi washiriki waongeze shughuli zaidi kama mwezeshaji utagundua kuna baadhi ya shughuli ambazo bado hazijajadiliwa.
    e. Hakikisha unauliza kila shughuli wanayofanya na inawachukua muda gani kuikamilisha. Shughuli zinazofanywa kwa wakati mmoja, kama vile kulea watoto na kutunza bustani zinaweza kuandikwa kwenye sehemu moja.
    f. Wakati huu utakuwa umeweka muda kwenye kila shughuli za siku nzima kwa wote wanawake na wanaume kutoka kwenye makundi mbalimbali (watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu).
    g. Ongoza mjadala kuhusu wingi wa kazi na ratiba za wanawake na wanaume kwenye misimu mbalimbali (kama inafaa na kama muda unaruhusu).
2. Uliza maswali yoyote ya kufuatilia na andika majibu wakati wa majadiliano ya pamoja ili kuelewa matumizi ya muda kwa wanaume na wanawake na athari zake kwenye wingi wa kazi na ushiriki kwenye shughuli za mradi.
3. Kutoka kwenye majadiliano ya shughuli za kila siku, bainisha aina mbalimbali za kazi za nyumbani kwa wanawake,wanaume,wasichana na wavulana.
    a. Mwezeshaji atawasaidia washiriki kuorodhesha kazi za nyumbani/kaya (mfano kupika, kukamua maziwa n.k.) na kazi za uzajishaji (ufugaji, kilimo,kupalilia,kuuza bidhaa, n.k) na kazi za kijamii. Hii ni mifano tu– siyo lazima uitumie kama haihusiki.
    b. Ongoza makubaliano kuhusu shughuli kuu tano katika kila kipengele (kuhusu kiasi cha muda unaotumika kila siku). Tambua kwamba mchukua vitini anaweza kuwa msaada mkubwa sana katika kuhesabu kura za watu na kufikia makubaliano.
    c. Chora jedwali kuonyesha makundi mbalimbali ya watu kwenye orodha ya kazi na itandaze sakafuni.
4. Waambie washiriki wajadili na waonyeshe tofauti za kijinsia kwenye majukumu na wajibu.
    a. Onyesha matriki hii hapo chini kwenye bango kitita au sakafuni kwa ajili ya kulijaza.
    b. Wagawie washiriki kwa Pamoja mbegu 10 waambie wazigawe mbegu hizo 10 kwenye safu wima kulingana na majukumu yao, nani hufanya zaidi kila kazi iliyotajwa. Mbinu ya mbegu 10 inaweza kutusaidia kuelewa mgawanyo wa majukumu ya kijinsia kwa makundi mbalimbali ya kijamii.[38] Ikiwa kikundi hakina jukumu kwenye jukumu husika, basi hakitapata mbegu yeyote, pale kikundi kitakapokuwa na jukumu maalumu kitapata mbegu 10.Kundi ambalo halifanyi shughuli yoyote maaulumu kwenye jukumu husika hawapata mbegu yoyote, na kundi lenye jmajukumu mengi litapata mbegu 10.

38 Adapted from Jayarakan (2002). The Ten Seeds Technique.

5. Waambie washiriki waelezee wanatumia muda gani kukamilisha shughuli na mahali ambapo shughuli hufanyika. Taarifa kuhusu mahali ambapo shughuli hufanyika inasaidia kuelewa jinsi watu wanavyotembea au kuhama.

6. Waambie washiriki wajadili matokeo. Ongoza majadiliano ili washiriki wafikie mwafaka. Wakati wote angalia sehemu ambazo hawakubaliani na ziandike.

**Kumbuka**

- Hakikisha unawadadisi washiriki waelezee kuwa ni nani huwa anafanya kazi nyingi zaidi hata kama wakati mwingine wanaweza kusema kazi hizo zinafanywa na kila mtu, inawezekana mtu mmoja anafanya kazi mara mbili ya wengine.
- Shawishi majadiliano ya kutoa maelezo kuhusiana na ushiriki wa makundi mengine kwenye shughuli za kila siku mfano watu wenye ulemavu, watu waishio na virusi vya ukimwi n.k. (Tafadhali ongeza makundi yasiyohusishwa kadiri inavyohitajika kulingana na muktadha).
- Kusanya maoni yao kama wanakubaliana au hawakubaliani na utaratibu uliopo, na kwa nini.
- Wadadisi waelezee kama shughuli hizi zinaweza kubadilika badilika kulingana na msimu mfano msimu wa mvua na kiangazi.

**Jedwali 14 | Chati ya Shughuli za Kila Siku**

| Jukumu/Shughuli | Nani hufanya shughuli nyingi zaidi? | | | | Inachukua muda gani kumaliza shughuli hiyo? | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | Wasichana | Wavulana |
| **A. Majukumu ya Uzazi** | | | | | | | | |
| 1. Kusafisha na kufua | | | | | | | | |
| 2. Kuandaa chakula | | | | | | | | |
| 3. Kuhudumia wagonjwa | | | | | | | | |
| 4. Kuhudumia watoto | | | | | | | | |
| 5. Kuchota maji na kusanya kuni | | | | | | | | |
| 6. Kulisha mifugo | | | | | | | | |
| **B. Majukumu ya Uzalishaji Mali** | | | | | | | | |
| 1. Shughuli za kilimo (bainisha, mfano kupanda, kupalilia, kuvuna,ufugaji uvuvi, n.k.) | | | | | | | | |
| 2. Ajira rasmi | | | | | | | | |
| 3. Kuuza bidhaa na kutoa huduma | | | | | | | | |
| 4. Yanayohusiana na shule | | | | | | | | |
| 5. Mafunzo na warsha za kuongeza ujuzi na kujenga uwezo | | | | | | | | |
| 6. Shughuli zingine zisizohusiana na kilimo (bainisha, mfano ushonaji, kazi za ujenzi, useremala n.k.) | | | | | | | | |
| **C. Shughuli za Kijamii** | | | | | | | | |
| 1. Kusafisha vyanzo vya maji kwenye jamii | | | | | | | | |
| 2. Kujitolea kwenye shule iliyopo kwenye jamii | | | | | | | | |
| 3. Kuhudhuria mikutano ya kijamii | | | | | | | | |
| 4. Kampeni za kisiasa | | | | | | | | |

## MVL4: Tathmini ya Desturi za Kijinsia na Kijamii

Majadiliano haya husaidia kubaini desturi za kijamii na kijinsia katika jamii. Pamoja na kwamba Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) haya yako tofauti na yale mengine (kwa sababu maswali maalumu ya kupigiwa kura huwa yanaulizwa), lengo ni kuchochea majadiliano yenye manufaa baada ya kila swali na kuwezesha uelewa mkubwa kuhusu masuala ya kijamii na kijinsia katika jamii. Kuelewa desturi za tabia kutasaidia kuelewa jinsi desturi na tamaduni za kijamii zinavyoathiri wanawake na wanaume, wasichana na wavulana na makundi mengine ya kijamii.

**Maelekezo**
Andika umri, jinsi, hali ya ulemavu, ndoa,lugha,mahali na dini ya kila mshiriki. Hakuna haja ya kuandika majina ya washiriki. Kumbuka kutumia taratibu za Majadiliano ya Vikundi Lengwa hivi kulingana na usahihi wake kimuktadha.

**Vifaa vinavyohitajika**: Kadi za rangi ya bluu na nyekundu, sanduku la kupigia kura au tumia vifaa mbadala vilivyopo

**Muda**: Dakika 45–saa 1

**Rasilimali watu inayohitajika**: Mwezeshaji mmoja na mchukua vitini mmoja

**Viburudisho**: Juisi, maji na chakula. Majadiliano ya Vikundi Lengwa (MVL) yanaweza kuwa marefu na za kuchosha kama hakutakuwa na viburudisho

### Mwongozo Hatua kwa Hatua

1. Utahitaji kadi za rangi ya bluu na nyekundu na sanduku la kupigia kura.
2. Wape washiriki wote kadi moja ya bluu na moja nyekundu.
3. Soma maelekezo yafuatayo kwa sauti wakati umesimama mbele ya washiriki:
    a. Kwenye jamii ambayo si rahisi watu kushawishiwa na watu wengine, waambie:
        – Nitawasomea orodha ya maoni na ninawaomba mfikirie kuhusu majibu yenu. Pigia kura kila swali kwa kutumia kadi.
        – Inua kadi ya bluu juu ya kichwa chako kama unakubaliana na sentensi zifuatazo na inua kadi ya rangi nyekundu kama hukubaliani. Kama hujui, shusha mikono yako chini.
    b. Kwenye jamii ambayo ni rahisi watu kushawishiwa na wengine, waambie:
        – Nitawasomea orodha ya maoni na ninawaomba mfikirie kuhusu majibu yenu. Pigia kura kila swali kwa kutumia kadi.
        – Waambie wapigie kura kila sentensi kwa siri kwa kutumia kadi yenye rangi tofauti: kama unakubalina na sentensi zifuatazo tumia kadi ya bluu na iwapo hukubali tumia rangi nyekundu. Weka kadi yenye rangi kwa kila sentensi kwenye sanduku la kura, na iwapo huna uhakika kuhusu sentensi usiweke chochote kwenye sanduku.
        – Mwishoni kura za bluu na nyekundu zitahesabiwa na kujumlishwa.
4. Hakikisha kila mtu ameelewa maelekezo na aanze kusoma maoni kutoka kwenye jedwali hapa chini.
5. Andika majibu kila baada ya swali (au andika jumla ya kura, ikiwa unatumia mbinu ya sanduku la kura).
6. Baada ya kila swali, wadadisi washiriki ili upate maoni yao kama tabia hiyo inakubalika au haikubaliki kwenye kundi hilo, na kwa nini. Kwa mfano, kama wanawake hawaruhusiwi kumiliki ardhi, angalia kama wanawake wenyewe wanakubali au hawakubaliani na hii mila.
7. Wadadisi washiriki waelezee sababu za kuwepo kwa mila hii. Kwa mfano, kwa nini ni kawaida kwa wanaume kuwapiga wake zao na si kinyume chake?

8. Kisha uliza madhara gani ya kijamii yanaweza kutokea ikiwa mila hii itavunjwa na kuna adhabu gani za kijamii ambazo huweza kupewa kwa wasio tii hii mila. Je, watu hao bado wasingetii hio mila kama pangekuwa hakuna madhara?
9. Wadadasi washiriki wajadili matumizi ya desturi ya kijamii kwa makundi mengine ya kijamii.
10. Waulize kama kuna mtu yeyote anayetaka kutoa maoni au kujadili majibu yao. Wanaposema kitu, wadadisi watoe maelezo zaidi. Ni sawa kuruhusu mazungumzo yaendelee juu ya hizi mada.
11. Kama una muda, ruhusu majadiliano kufanyika kila baada ya swali maana inaweza kutoa ufafanuzi mzuri kuhusu tabia za desturi. Pia inakusaidia wewe kuelewa aina ya jamii unayofanya nayo kazi. Aidha, kutumia maelezo mafupi na maswali ya kudodosa kunaweza kukusaidia.
12. Zana hii ni rahisi lakini ni thabiti katika kuwasaidia watu kutafakari kwa namna ambayo wamekuwa wakiwaza siku zote.

**Jedwali 15A | Tathmini ya Desturi za Kijinsia na Kijamii**

[Nakili idadi ya kadi za bluu na nyekundu na idadi ya watu ambao hawajazichagua

| Sentensi | Bluu= Nakubali | Nyekundu= Sikubali | Sijui |
|---|---|---|---|
| 1. Katika jamii yangu, wanawake hufurahi pale wanaume wanapofanya sehemu kubwa ya shughuli za nyumbani. | | | |
| 2. Mwanamke anajisikia huru kumuomba mwenzi wake amsaidie shughuli za nyumbani. | | | |
| 3. Katika jamii yangu, wanaume hutaniwa wanapowasaidia wake zao kufanya shughuli za nyumbani. | | | |
| 4. Sababu kubwa ya wanaume kuwasaidia wake zao mara chache ni jamii kuwadhihaki/kuwakaripia. | | | |
| 5. Katika jamii yangu, wanaume hujivunia pale wanapomiliki biashara (kama kuuza mifugo, duka, n.k.) | | | |
| 6. Jamii haikubaliani na suala la mwanamke aliyeolewa kuwa chanzo kikuu cha kipato kwa familia yake. | | | |
| 7. Katika jamii yangu, wanaume hulaumiwa pale wanaposhindwa kupata kipato kwa ajili ya familia zao. | | | |
| 8. Jamii haikubaliani na suala la mwanamke kuhudhuria mikutano (kama vile mafunzo na ziara za kikazi). | | | |
| 9. Jamii haikubaliani na suala la wanaume kuwaruhusu wake zao kushiriki katika shughuli za miradi. | | | |
| 10. Jamii yangu haikubali na suala la wanaume kushirikisha wake zao katika kufanya maamuzi yanayohusiana na biashara, shughuli za kuongeza kipato, au rasilimali muhimu kwa ajili ya riziki ya familia. | | | |
| 11. Jamii yangu haikubaliani na wanawake wanaozungumza hadharani katika mikutano au mikusanyiko mingine ya kijamii kuhusu haki zao na ustawi. | | | |
| 12. Watoto huteseka pale mwanamke anapofanya kazi nje ya nyumbani. | | | |
| 13. Wanawake hupendelea kufanyia kazi nyumbani. | | | |

| Sentensi | Bluu= Nakubali | Nyekundu= Sikubali | Sijui |
|---|---|---|---|
| 14. Katika jamii yangu, siku zote mwanamume huwa wa kwanza kula chakula. | | | |
| 15. Mume anastahili kupata mlo mzuri zaidi kuliko wengine wote. | | | |
| 16. Katika jamii yangu, wanaume hufanya maamuzi makubwa karibu yote. | | | |
| 17. Mwenza wangu ana miliki ardhi iliyoandikwa kwa jina lake. | | | |
| 18. Wanawake kwenye jamii yangu wanaweza kumiliki ardhi kama wanaume. | | | |
| 19. Wanawake kwenye jamii yangu wanaweza kuwa viongozi kama wanaume. | | | |
| 20. Wanawake kwenye jamii yangu wana fursa sawa na wanaume | | | |
| 21. Katika jamii yangu, wanaume hushiriki kwenye mikutano karibu yote (mfano mikutano ya kijamii na kisiasa) | | | |
| 22. Kwa mawazo yako, je, inakubalika kwa mtu kumpiga mkewe au mumewe (kwa mfano akishindwa kuhudumia watoto vizuri, akikataa kufanya tendo la ndoa, mabishano,n.k.)? | | | |
| 23. Katika jamii yangu, watu wenye ulemavu hapaswi kushiriki katika shughuli yoyote ya kiuchumi na kuzalisha kipato. | | | |
| 24. Katika jamii yangu, haki ya watu wenye ulemavu juu ya upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma za kijamii wanazohitaji kwa ajili ya ustawi wao sio muhimu. | | | |
| 25. Katika jamii yangu, ni sawa kwa familia au wanajamii kufanya maamuzi kwa niaba ya watu wenye ulemavu juu ya mahitaji yao binafsi bila kuwahusisha kwenye maamuzi hayo. | | | |
| 26. Ili kuhakikisha upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma kwa watu wenye ulemavu, mtu kutoka nje ya jamii anapaswa kuja na kusaidia watu wenye ulemavu.[39] | | | |
| 27. Vitini / matokeo / mambo ya kuangalia: | | | |

### Vitini vya Mwezeshaji

Kama una muda, ruhusu majadiliano yafanyike kila baada ya swali maana yanaweza kutoa ufafanuzi mzuri kuhusu tabia za desturi. Pia itakusaidia wewe kuelewa aina ya jamii unayofanya nayo kazi. Kwa mwongozo zaidi juu ya jinsi ya kudadavua desturi za kijinsia na kijamii, tafadhali angalia sehemu inayofuata.

39 World Vision (2010). Travelling Together

## KUELEWA DESTURI ZA KIJINSIA NA KIJAMII

Desturi za kijinsia na kijamii zinagusa vikoa vyote vitano. Kwa hiyo ni muhimu kuwa na uelewa mzuri wa desturi hizi na jinsi zinavyoathiri tabia maalum ambayo ni muhimu katika kufikia malengo na madhumuni ya mradi. Zana ya kutathmini destruri za kijinsia na kijamii ni mahali pazuri pa kuanzia ili kubainisha baadhi ya desturi zilizopo zinazohusiana na mahusiano na ulemavu lakini maelezo ya ziada yatahitajika katika kudadavua desturi hizo ili kuunda mkakati wa mabadiliko ya kijamii na tabia.Kuna zana kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya hivyo. Jedwali linatoa muhtasari wa kila zana, jinsi inavyoweza kutumika, ubora na udhaifu wake. Zana zote zitatoa taarifa kuhusu destruri za kijinsia na kijamii lakini pia zitatoa maelezo ya ziada. Kwa mfano, kikundi lengwa cha majadiliano cha 'Five Whys' katika zana ya uchunguzi wa desturi za kijamii (*social norms exploration tool–SNET*) itatoa sababu zinazohusiana na vikwazo vya kifedha au kimazingira kwenye tabia pamoja na vile vinavyohusiana na desturi.Mwezeshaji atatakiwa kuyapa kipaumbele maswali ambayo yanawezesha uelewa wa vikwazo vinavyosababishwa na desturi.

**Jedwali 15B | Mifano ya Maswali Kusaidia Uelewa wa Vikwazo Vinavyohusiana na Desturi za Kijamii**

| Zana | Maelezo | Matumizi | Ubora | Udhaifu |
|---|---|---|---|---|
| 1. Uchanganuzi wa Vikwazo | Hoji watu 45 walio na hiyo tabia na 45 wasio kuwa nayo | Kuelewa ubora wa visababishi mbalimbali vya tabia | Hufafanua umuhimu wa visababishi mbalimbali | Inahitaji ufuatiliaji wa ziada ili kuelewa sababu zilizo nyuma ya visababishi |
| 2. Kubaini watu wenye ushawishi | Mahojiano na wanaume 15 na wanawake 15 kutoka kwenye kundi la walengwa juu ya nani anayewashawishi kwenye tabia zao | Kuelewa washawishi wa kundi letu lengwa | Inabaini watu weney ushawishi ambao wanahita kuhamasishwa kuendeleza tabia | Mahojiano ya Vikundi Lengwa na washawishi yatahitajika baadaye |
| 3. Mahojiano ya Vikundi Lengwa kwa ajili ya uchunguzi wa desturi za kijamii | Mjadala shirikishi kulingana na *'Five Whys', Problem Tree au vignette* | Kuelewa mienendo ya desturi za kijinsia na kijamii zinazo sababisha tabia | Hudadavua desturi kwa kina na kuruhusu ujumbe wa mabadiliko ya kijamii na tabia kuandikwa | Haibaini umuhimu wa desturi katika kusababisha tabia |
| 4. Mahojiano ya Vikundi Lengwa kwa kutumia ramani ya mchakato | Washiriki wanatoa maoni kuhusu uzoefu wao katika mchakato | Kubaini vikwazo na viwezeshi katika hatua mbalimbali za kwenye mchakato | Maoni bayana juu ya vikwazo vilivyopo katika mchakato | Inahitaji ufuatiliaji wa ziada ili kudadavua vikwazo vinavyohusiana na desturi |
| 5. Mapitio ya Data za Upili | Pitia machapisho yaliyopo ambayo yatakusaidia kuelewa maswali muhimu yanayohusiana na desturi | Kujibu maswali muhimu kuhusu desturi | Njia rahisi, yenye gharama nafuu ya kubaini kile kinachojulikana tayari, kupunguza kiasi cha ukusanyaji wa data za msingi | Data zinaweza zisiwe za eneo lengwa au tabia halisi na zinahitaji kuthibitishwa |
| 6. Mahojiano ya watoa taarifa maalumu | Maswali muhimu yanayoulizwa kwa watu binafsi kuhusu desturi | Kuelewa maswali muhimu kuhusu desturi | Uwezekano wa kuwa wazi na bayana zaidi katika kujibu kuliko katika kikundi | Taarifa zinatakiwa zihakikiwe |

## UCHANGANUZI WA VIKWAZO

Uchanganuzi wa Vikwazo ni utafiti ulioundwa kwa ajili ya kuboresha uelewa wa mambo ambayo huathiri tabia fulani. Watekelezaji hutumia matokeo kutoka kwa Uchanganuzi wa Vikwazo kuunda afua za mabadiliko ya kijamii na kitabia (*Social and Behavior Change-SBC*) zenye ufanisi zaidi[40]. Uchanganuzi wa Vikwazo mara nyingi hutumika kama sehemu ya mchakato wa usanifu wa mabadiliko ya tabia ambapo matokeo ya Uchanganuzi wa Vikwazo hutumiwa katika kuunda afua au mipango ya mabadiliko ya kijamii na kitabia.Katika utafiti wa Uchanganuzi wa Vikwazo, wahojiwa huulizwa kama wanafanya au hawashiriki katika tabia maalumu (kwa mfano, kupeleka mtoto wao kwenye chanjo). Wahojiwa wanaoripoti kuwa na tabia hiyo wanaainishwa kama "wanaofanya" na wale wanaoripoti kutokuwa na tabia hiyo wanaainishwa kama "wasiofanya." Kisha kila mhojiwa anaulizwa msururu wa maswali kuhusu sababu za kibinafsi, kijamii na kimazingira ambazo zinaweza kuathiri tabia hiyo. Na mwisho, data zinachanganuliwa kwa kulinganisha sababu za kibinafsi, kijamii, na kimazingira kati ya "wanaofanya" na wale "wasiofanya." Ikiwa majibu kati ya vikundi viwili ni sawa, basi sababu hiyo haizingatiwi kuwa ni sababu ya ushawishi katika tabia yenyewe. Ikiwa majibu ya "wanaofanya" na "wasiofanya" ni tofauti, basi dhana ni kwamba sababu hio huathiri tabia kwa namna fulani.

Uchanganuzi wa Vikwazo unaweza kutumika mwanzoni mwa programu ya kubadilisha tabia ili kubainisha ujumbe na afua muhimu. Unaweza pia kutumika katika programu inayoendelea inayozingatia tabia ambazo hazijabadilika sana (licha ya jitihada za mara kwa mara) kuelewa ni nini kinawazuia watu kufanya mabadiliko fulani. Ingawa tafiti za Uchanganuzi wa Vikwazo wakati mwingine zinaweza kuwa muhimu kupata wazo la jumla la visababishi muhimu vya tabia katika eneo kubwa kama vile katika wilaya nzima- **Uchanganuzi wa Vikwazo una manufaa ZAIDI unapotumika katika jamii husika au miongoni mwa watu mahususi kwani visababishi vinavyoathiri tabia mara nyingi hutofautiana katika jamii au kabila, lugha, au vikundi vya kidini.** Miradi mara nyingi huona ni bora kufanya tafiti za Uchanganuzi wa Vikwazo baada ya kukamilisha utafiti wa kimsingi ambao unawezesha kubainisha tofauti kuu kati ya makundi mbalimbali ndani ya eneo la mradi.

Mafunzo ya awali ya wakufunzi wa Uchanganuzi wa Vikwazo kwa kawaida huchukua siku nane kamili. Wahitimu wa mafunzo haya ya awali ya wakufunzi kwa kawaida wanaweza kusanifu Uchambuzi wa Vikwazo, kutoa mafunzo kwa timu ya waandikishaji 4-6, kufanya uchunguzi kamili wa wafanyaji 45 na wasiofanya 45, na kuchanganua matokeo kwa takribani siku tano au chini ya hapo. Ingawa inawezekana kuajiri kampuni nyingine kufanya Uchambuzi wa Vikwazo na kuchanganua matokeo, miradi mingi inapendelea kutumia wafanyakazi wao wenyewe kukusanya na kuchanganua data. Wafanyakazi wengi hujifunza taarifa muhimu sana na kupata mitazamo muhimu kuhusu jumuiya wanazofanyia kazi wakati wanakusanya na kuchanganua data za Uchanganuzi wa Vikwazo.

Katika Uchanganuzi wa Vikwazo uliokamilika, maswali yanayohusiana na "Visababishi 12 vya tabia" kuhusiana na tabia maalumu inayolengwa yanajumuishwa. Visababishi hivi vinatokana na nadharia za tabia (hasa kutoka kwa Muundo wa Imani ya Afya na Nadharia ya Kitendo cha Kufikiri– au kwa kiingereza ni (*Health Belief Model and the Theory of Reasoned Action*), na vinajumuisha mitazamo ya watu ya:

1. **Kujitosheleza**: Imani kwamba mtu ana uelewa na ujuzi wa kuwa na tabia hiyo.
2. **Desturi**: Mtazamo kwamba watu walio muhimu wanadhani mhusika anapaswa au hawapaswi kuwa na tabia hiyo.
3. **Matokeo Chanya:** Mambo mazuri ambayo mtu anadhani yatatokea kutokana na kuwa na tabia hiyo.
4. **Matokeo Hasi:** Mambo mabaya ambayo mtu anadhani yatatokea kutokana na kuwa na tabia hiyo.
5. **Upataji na Ufikiaji:** Upatikanaji wa bidhaa au huduma zinazohitajika ili kuwa na tabia hiyo. Hii inajumuisha vikwazo vinavyohusiana na gharama, umbali, na kukubalika kwa kitamaduni kwa bidhaa na huduma.
6. **Sera**: Uwepo wa sheria na kanuni ambazo zinaweza kuathiri uwezo wa watu kuwa na tabia hiyo.
7. **Mila**: Kiwango ambacho historia, desturi, mitindo ya maisha, maadili na mazoea zinaweza kuathiri tabia.

40 Explanations offered in this section draw heavily from: The Technical and Operational Performance Support (TOPS) Program. 2016. Decision Guide for Program Managers: What You Need to Know About the Designing for Behavior Change Approach. Washington, DC: The Technical and Operational Performance Support Program; Kittle, Bonnie. 2017. A Practical Guide to Conducting a Barrier Analysis (2nd ed.). New York, NY: Helen Keller International; and The HALO Trust. Using Barrier Analyses to Improve Explosive Ordnance Risk Education.

8. **Vidokezo vya kuwa na tabia / Vikumbusho:** Uwepo wa vikumbusho vinavyomsaidia mtu kukumbuka kufanya tabia.
9. **Uwezekano wa athari:** Mtazamo wa mtu juu ya uwezekano kwamba matokeo mabaya yatatokea.
10. **Kiwango cha athari:** Mtazamo juu ya kiwango cha ukali wa matokeo mabaya ambayo yanaweza kutokea
11. **Ufanisi wa tabia:** Kiwango ambacho mtu anaamini tabia itasababisha matokeo mazuri yanayohusiana au kuepuka athari mbaya.
12. **Mapenzi ya Mungu:** Kiwango ambacho mtu anaamini matendo na athari zake ni matokeo ya mapenzi ya Mungu na kwa hiyo iko nje ya udhibiti wao.

Kwa sababu maswali ya uchunguzi yameandaliwa kwa kila moja ya visababishi hivi 12, inawezekana wakati wa uchanganuzi wa data kugundua ni yupi kati ya visababishi kumi na mbili vina ushawishi mkubwa juu ya tabia fulani. Kihistoria, vinne vya kwanza: kujitosheleza, desturi, matokeo chanya, na matokeo hasi ni viashiria muhimu zaidi vya tabia. Kwa hivyo, inashauriwa vijumuishwe kila wakati, ingawa vingine vinaweza kuwa muhimu zaidi au kidogo kulingana na muktadha.

## ZANA YA UCHUNGUZI WA DESTURI ZA KIJAMII (SNET)[41]

Zana ya uchunguzi wa desturi za kijamii (kwa lugha ya kiingereza ni *social norms exploration tool au kwa kifupi ni SNET*) ni mwongozo shirikishi na zana za kutafsiri nadharia kuwa ni mwongozo wa vitendo ili kusaidia uchunguzi wa desturi za kijamii. Inajumuisha mwongozo wa hatua kwa hatua, mazoezi, na violezo kwenye kijitabu cha zana kinaweza kusaidia watekelezaji wa programu:

| |
|---|
| Kuelewa nadharia na dhana za desturi za kijamii |
| Kuwaandaa wafanyakazi kubaini na kuchunguza desturi za kijamii |
| Kushirikisha wanajamii kwa kutumia mazoezi shirikishi ya kujifunza ili: 1) kubainisha washawishi wa tabia na 2) kuchunguza kanuni za kijamii zinazoathiri tabia |
| Kuchanganua taarifa kwa kushirikiana na timu ya mradi na wanajamii |
| Kutumia matokeo katika usanifu wa shughuli za kubadilisha desturi na kutengeneza zana za tathmini zinazozingatia desturi |



**Zana ya uchunguzi wa desturi za kijamii ina hatua tano:**

1. **PANGA NA JIANDAE:** Tafakari juu ya desturi zinazoweza kuathiri matokeo ya tabia unayoitaka, kisha fafanua malengo ya uchunguzi, chagua na uandae mazoezi shirikishi.
2. **BAINISHA WASHAWISHI WA TABIA:** Tumia mazoezi shirikishi kwa washiriki wa mradi kubaini washawishi wa tabia na fanya uchanganuzi wa haraka.
3. **CHUNGUZA DESTURI ZA KIJAMII:** Tumia mazoezi shirikishi kwa washiriki wa mradi na washawishi wa tabia kuhusu mambo yanayoathiri tabia maalum, dadavua desturi na na ushawishi wake
4. **CHANGANUA MATOKEO:** Fanya uchanganuzi shirikishi ili kulinganisha na kubainisha mada na kuandika muhtasari wa matokeo.
5. **TUMIA MATOKEO:** Tumia matokeo kusanifu au kuboresha programu kwa ajili ya utekelezaji, ukizingatia kubuni mikakati mahususi ya kushughulikia desturi muhimu zaidi na kushirikisha washawishi wa tabia kwenye jamii.

41 Institute for Reproductive Health (irh.org)

## TAFITI ZA KAYA KUHUSU UFANYAJI MAAMUZI, USHIRIKI NA USTAWI

Tafiti za kaya ni moja ya mifano ya mbinu unazoweza kutumia kukusanya data za kitakwimu zenye muitikio wa GESI katika ngazi ya kaya na mtu binafsi.Tafiti zinakusanya taarifa kuhusu sifa, idadi ya watu, tabia, mahitaji, uzoefu na maoni ya makundi mbalimbali ya watu. Tafiti za kaya pia hutoa taarifa halali kitakwimu kuhusu watu wengi. Tafiti nyingi hutumia maswali yasiyoruhusu kujieleza lakini pia zinaweza kujumuisha maswali yanayoruhusu kujieleza ili kufafanua majibu ya maswali yasiyoruhusu kujieleza. Data ziliyogawanywa za GESI zinaweza kukusanywa kutoka kwa kaya hiyo hiyo au watu hao hao kwa kipindi cha muda fulani ili kupata taarifa za muelekeo au mabadiliko kwa kipindi cha muda fulani. Kwa mfano, unaweza kukusanya data za msingi, kabla ya kuanza, katikati au mwishoni mwa mradi kutoka kwenye kaya au watu walewale na kulinganisha matokeo. Tafiti za kaya huweza kufanywa kabla ya utekelezaji wa mradi, na wakati wa ufuatiliaji na tathmini ya mradi.

Jedwali 16, 17 na 18 ni mifano ya maswali unayoweza kutumia kwenye tafiti za kaya ili kukusanya data za kitakwimu zenye muitikio wa GESI.

**Jedwali 16 | Tafiti za Kaya Kuhusu Ufanyaji Maamuzi**

| **Shughuli** | **Je, kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita ulifanya maamuzi ya kushiriki kwenye shughuli hii?**<br>**1 = Ndiyo**<br>**2 = Hapana** | **Je, ulitoa mchango wa mawazo kiasi gani kwa ajili ya maamuzi?**<br>**1 = Sikutoa**<br>**2 = Nilitoa kwenye maamuzi machache**<br>**3 = Nilitoa kwenye baadhi ya maamuzi**<br>**4 = Nilitoa kwenye maamuzi yote**<br>**5 = Sikufanya maamuzi yoyote** | **Je, ni nani alifanya maamuzi ya namna ya kufurahia faida/ kutumia mapato yaliyo tokana na shughuli hiyo?**<br>**1 = Mimi mwenyewe**<br>**2 = Sote pamoja lakini nilifanya maamuzi mengi zaidi**<br>**3 = Sote pamoja lakini mwenza /mume/ mke alifanya maamuzi mengi zaidi**<br>**4 = Mengine (taja)** | **Je, unafikiri ni kwa kiasi gani unaweza kufanya maamuzi yako mwenyewe kuhusu shughuli hizi pasipo kulazimishwa/ kushurutishwa?**<br>**1 = Hapana kabisa**<br>**2 = Kiasi kidogo**<br>**3 = Wastani**<br>**4 = Kiasi kikubwa** |
|---|---|---|---|---|
| **A. Shughuli za Kiuchumi** | | | | |
| 1. Kilimo cha mazao ya chakula | | | | |
| 2. Shughuli za uchumi zisizo za kilimo | | | | |
| 3. Kilimo cha mazao ya biashara | | | | |
| 4. Ufugaji | | | | |
| 5. Shughuli za kujipatia kipato[42] | | | | |
| 6. Mafunzo na warsha za kuongeza ujuzi na kujenga uwezo | | | | |
| 7. Kuuza mazao ya kilimo | | | | |
| 8. Shughuli za kujipatia riziki wakati wa dharura | | | | |

42 This does not include the broader household income or cash earned by the spouse/partner or other household members.

| Shughuli | Je, kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita ulifanya maamuzi ya kushiriki kwenye shughuli hii?<br>1 = Ndiyo<br>2 = Hapana | Je, ulitoa mchango wa mawazo kiasi gani kwa ajili ya maamuzi?<br>1 = Sikutoa<br>2 = Nilitoa kwenye maamuzi machache<br>3 = Nilitoa kwenye baadhi ya maamuzi<br>4 = Nilitoa kwenye maamuzi yote<br>5 = Sikufanya maamuzi yoyote | Je, ni nani alifanya maamuzi ya namna ya kufurahia faida/ kutumia mapato yaliyo tokana na shughuli hiyo?<br>1 = Mimi mwenyewe<br>2 = Sote pamoja lakini nilifanya maamuzi mengi zaidi<br>3 = Sote pamoja lakini mwenza /mume/ mke alifanya maamuzi mengi zaidi<br>4 = Mengine (taja) | Je, unafikiri ni kwa kiasi gani unaweza kufanya maamuzi yako mwenyewe kuhusu shughuli hizi pasipo kulazimishwa/ kushurutishwa?<br>1 = Hapana kabisa<br>2 = Kiasi kidogo<br>3 = Wastani<br>4 = Kiasi kikubwa |
|---|---|---|---|---|
| **B. Shughuli za Kijamii** | | | | |
| 1. Kamati za maendeleo ya uchumi wa jamii | | | | |
| 2. Jumuiya za watumiaji wa maji/ kamati za maji | | | | |
| 3. Halmashauri za serikali za mitaa | | | | |
| **C. Shughuli za Jamii** | | | | |
| 1. Watoto wanaenda shule | | | | |
| 2. Kazi ya afya ya uzazi kwenye vituo vya afya | | | | |
| 3. Kutumia huduma za afya | | | | |
| **D. Shughuli za Kisiasa** | | | | |
| 1. Kupiga kura kwa ajili ya maofisa wa ngazi zote za serikali | | | | |
| 2. Kugombea nafasi ya uongozi katika ngazi zote za serikali | | | | |

**Jedwali 17 | Tafiti za Kaya Kuhusu na Ushiriki**

| Je, huwa unashiriki kwenye...... | Kushiriki<br>1 = Sijawahi<br>2 = Mara moja moja<br>3= Mara nyingi<br>4 = Wakati wote | Kama hujawahi, je, sababu kubwa tatu ni zipi? | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Sababu 1 | Sababu 2 | Sababu 3 |
| 1. Mafunzo ya WASH? | | | | |
| 2. Kuchota maji? | | | | |
| 3. Tabia za usafi wa mazingira na usafi wa kimwili? | | | | |
| 4. Jumuiya ya watumiaji maji? | | | | |
| 5. Kutumia teknolojia za WASH (vituo vya kunawa mikono, machujio ya maji,vyoo) kwenye kaya zao? | | | | |
| 6. Shughuli za WASH kwenye jamii (kuchimba kisima kwa ajili ya matumizi ya umma, kufanya kazi kwenye mfumo wa usambazaji wa maji kwenye jamii n.k.)? | | | | |
| 7. Shughuli mbalimbali za kilimo? | | | | |
| a. Kutayarisha shamba | | | | |
| b. Kupanda | | | | |
| c. Kupalilia | | | | |
| d. Kuhifadhi | | | | |
| e. Kulima | | | | |
| f. Kuchakata | | | | |
| g. Kutafuta soko | | | | |
| 8. Kikundi cha biashara, kikundi cha kuweka akiba au kukopeshana pesa, au vyama vya ushirika? | | | | |
| 9. Sokoni kama mchuuzi, msambazaji, au muuzaji wa bidhaa za jumla? | | | | |
| 10. Mafunzo kuongeza ujuzi na maarifa kwa ajili ya fursa za ajira? | | | | |
| 11. Kufanya kazi zinazohusiana na afya ya mambo ya uzazi kwenye kituo cha afya kilichopo karibu? | | | | |
| 12. Kuwahudumia wagonjwa? | | | | |
| 13. Kuhudhuria mafunzo juu ya ukatili wa kijinsia? | | | | |
| 14. Watoto wanashiriki kwenye shughuli za shuleni kama klabu, michezo? | | | | |
| 15. Mikutano ya kijamii au makundi mengine ya pamoja? | | | | |
| 16. Kujenga uwezo/kipindi cha mafunzo juu ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kwenye jamii? | | | | |
| 17. Kuzungumza kuhusu usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii na masuala mengine ya kijamii kwenye jamii. | | | | |
| 18. Nafasi muhimu za uongozi? | | | | |

**Jedwali 18 | Tafiti za Kaya Kuhusu Ustawi**

| | Jibu | |
|---|---|---|
| **Swali** | **1= Ndio 2=Hapana** | **Kama ni "hapana", sababu kubwa ni nini?[a]** |
| 1. Je, unaridhika na ubora wa chanzo cha maji ya kunywa? | | |
| 2. Je, unaridhika na mgawanyo wa muda na majukumu unaotumiwa na wanawake kwenda kuchota maji? | | |
| 3. Je, huhofii sana kuhusu uwezo wako kuhudumia mahitaji ya kaya yako? | | |
| 4. Je, unajiamini katika uwezo wako kujihudumia wewe na familia yako? | | |
| 5. Je, unaridhika na shughuli zako za kujipatia riziki? | | |
| 6. Je, umewahi kukumbana na ukatili wa kimwili au wa kingono kwenye kipindi cha miezi 12 iliyopita? | | |
| 7. Je, unafahamu sehemu unazoweza kwenda kupata msaada iwapo utakumbana na ukatili wa kimwili au wa kingono? | | |
| 8. Je, unahisi kuwa wahudumu wa afya wanakuhudumia kwa heshima na utu? | | |
| 9. Je, unahisi kuwa unapata huduma za afya za kutosha? | | |
| 10. Je, unajisikia kuwa umewezeshwa (kwa namna yoyote unavyodhani) | | |
| 11. Je, unahisi kujiamini na kujithamini | | |
| 12. Je, unahisi uko salama ndani ya kaya na jamii? | | |
| 13. Je, unaridhika na ubora wa elimu ya mtoto/watoto wako? | | |

[a] Sababu kuu ni nini:

1 = Kabila
2 = Dini
3 = Mwanamke
4 = Ulemavu
5 = Umasikini
6 = Kutokuwa na elimu
7 = Uzee
8 = Idaya ya maji/wauzaji wana tamaa
9 = Rushwa/matumizi mabaya ya madaraka
10= Mfumo wa kijamii hauna usawa
11= Sijui
99= mengineyo (taja) __________

## Hatua 4 | Kuchanganua na Kuripoti Data kwa Mwitikio wa GESI

Rejea ZANA 4.3, Ukurasa 84.


World Vision

# Sehemu 3

# Ujumuishaji wa GESI kwenye Usanifu wa Programu

Sehemu hii inahusu zana ambazo zinaweza kutoa mwongozo wa namna ya kujumuisha GESI kwenye usanifu wa mradi. Sehemu hii ina zana tano:


**ZANA 3.1** Mwongozo wa Kuandika Pendekezo la Mradi

**ZANA 3.2** Ujumuishaji wa GESI kwenye Usanifu wa Programu

**ZANA 3.3** Viashiria vya GESI

**ZANA 3.4** Mpango Kazi wa Ujumuishaji wa GESI

**ZANA 3.5** Uandaaji wa Bajeti yenye Muitikio wa GESI


## ZANA 3.1 MWONGOZO WA KUANDIKA PENDEKEZO LA MRADI

Zana hii ni orodha yenye maswali muhimu ya kuzingatia katika kuandika na/au kufanya mapitio ya ubora wa mapendekezo ya mradi ambayo yanashughulikia usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kuanzia mwanzo wa usanifu wa programu. Zana hii inakusudiwa kutumiwa na viongozi wa programu na mameneja wa miradi,sekta za kiufundi na wataalamu wa ufuatiliani na tathmini . Maswali ya mwongozo ni mfano wa orodha ambayo unaweza kuitumia katika sekat yoyote bila kujali mtazamo wa kisekta.[43]

**Jedwali 19 | Orodha ya Mapitio ya GESI Kuhusu Ubora wa Pendekezo la Mradi**

| Orodha | 1=Ndiyo<br>2=Hapana<br>3=Kiasi tu | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **1. Maelezo ya Programu** | | |
| 1.1. Je, uchanganuzi wa hali iliyopo umezingatia hali mbalimbali za kijamii, kiuchumi,kiutamaduni na kisiasa kwa wanaume, wanawake, wavulana, wasichana na makundi mengine yanayokandamizwa kama yalivyobainishwa kupitia uchanganuzi wa GESI? | | |
| 1.2. Je, uchanganuzi wa hali iliyopo umejumuisha matokeo ya uchanganuzi wa GESI na unaonyesha ufahamu wa mapungufu ya kijinsia na ubaguzi wa kijamii? | | |
| 1.3. Je, maelezo ya changamoto yamefafanua mapungufu ya kijinsia na ukosefu wa uhusishaji wa kijamii ambao programu imedhamiria kushughulikia? | | |
| 1.4. Je, data zilizogawanywa kwa jinsi na umri, na takwimu za jinsia na ulemavu zimetolewa kama maelezo ya usuli na/au umuhimu wa afua? | | |

43 Adapted from USAID (2013). How-to Note: Addressing Gender and Inclusiveness in Project Design.

| Orodha | 1=Ndiyo<br>2=Hapana<br>3=Kiasi tu | Mapendekezo |
|---|---|---|
| 1.5. Kama hapana, je, sababu zimetolewa (mfano kukosekana kwa data za aina hiyo, kutokuwa na umuhimu wa mgawanyo wa data dhidi ya kiashiria husika)? | | |
| 1.6. Je, kundi lengwa la washiriki linadhaniwa kuwa liko katika mazingira hatarishi au kukandamizwa? na je, hii inaendana na taarifai zilizoko kwenye na takwimu/ushahidi uliowasilishwa? | | |
| 1.7. Je, uchanganuzi wa athari umeangalia suala la kukosekana kwa uwezo wa kuwafikia na kufanya kazi na watu wasiohusishwa na wanawake, pamoja na suala la mikakati ya kupunguza athari hiyo? | | |
| 1.8. Je, uchanganuzi wa athari unajumuisha uwezekano wa vikundi vilivyowezeshwa (kama wanaume) kupinga kikamilifu uwezeshaji wa makundi yanayokandamizwa (kama wanawake), pamoja na mkakati wa kupunguza athari hiyo? | | |
| **2. Mpango wa Utekelezaji** | | |
| 2.1. Je, mpango wa utekelezaji unashughulikia vizuri masuala ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kama ilivyoelezwa katika uchanganuzi wa GESI? Kama hapana, je, mpango unapendekeza jinsi ya kutatua mapungufu? | | |
| 2.2. Je, shughuli zilizopendekezwa zinahusisha shughuli mahususi kuhusu jinsia na ukosefu wa uhusishaji? Je, shughuli hizi ni sahihi na zinatosha kuhakikisha kuwa ukosefu wa usawa hauogezeki? Je, zimegusia angalau vikoa vitatu kati ya vikoa vitano vya GESI? | | |
| 2.3. Je, shughuli zinajumuisha afua za kuendeleza uwezeshaji wa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi (mfano kuunda vikundi vya wanawake, kuvisaidia vikundi hivyo, kujenga uwezo wa vikundi vilivyo katika mazingira hatarishi, mafunzo ya wanaume kuhusu jinsia, kutengeneza fursa kwa wanawake waweze kushiriki katika ufanyaji maamuzi, kuongeza uwezo wa upataji na ufikiaji wa huduma na rasilimali, kuwasaidia kufanya kazi ambazo walikuwa hawafanyi kwa sababu za kitamaduni. | | |
| 2.4. Je, shughuli zinahusisha afua za kuendeleza uwezeshaji wa watu waliokandamizwa (kama vile kulenga watu wenye aina mbalimbali za ulemavu, kusaidia makundi haya, mafunzo kwa watu hao, kuongeza uwezo wa upataji na ufikiaji wa huduma na rasilimali, kuboresha ushiriki wao na uwezo wa kufanya maamuzi kwenye mradi)? | | |
| 2.5. Je, kuna bajeti kwa ajili ya kuwajengea wafanyakazi uwezo wa kutafakuri, kuelewa na kutetea GESI? | | |
| 2.6. Je, uchapishaji wa vipeperushi na nyaraka zinavyohusiana na GESI umejumuishwa kama tokeo mojawapo, kwa mfano nyaraka kuhusu utafiti wa athari za desturi za kijinsia kwenye uwezeshaji wanawake? | | |

| Orodha | 1=Ndiyo<br>2=Hapana<br>3=Kiasi tu | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **3. Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini** | | |
| 3.1. Je, mpango wa ufuatiliaji na tathmini umejumuisha mikakati ya kushughulikia mapungufu ya data za usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii katika mradi? | | |
| 3.2. Je, data zilizokusanywa kipindi chote cha mradi ziligawanywa kwa jinsi, ulemavu, umri, na makundi mengineyo? | | |
| 3.3. Je, mbinu shirikishi za utafiti wa kitaamuli unaohusisha makundi yanayokandamizwa zimejumuishwa kama sehemu ya mpango wa ufuatiliaji? | | |
| 3.4. Je, mpango wa ufuatiliaji unajumuisha muda wa kufanya tafakuri kwa pamoja na warsha za GESI? | | |
| 3.5. Je, mafanikio na vigezo vya athari na viashiria vina masuala ya kijinsia na uhusishaji kama ipasavyo? | | |
| 3.6. Je, mkabala wa ufuatiliaji una viashiria vya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii vinavyopimika na vilivyo stahiki kwa programu? | | |
| 3.7. Endapo ni viashiria vya ujumla tu ndio vimewekwa je, kuna viashiria vingine maalumu ambavyo vinaweza kupendekezwa ili kufuatilia masuala ya GESI? | | |
| **4. Bajeti** | | |
| 4.1. Je, kuna fungu la fedha limetengwa kwenye bajeti kwa ajili ya kusaidia uhusishaji wa kijamii na wafanyakazi waliojitolea kutekeleza mipango ya GESI? | | |
| 4.2. Je, rasilimali za kutosha zimetolewa kwa ajili ya shughuli za GESI zilizopendekezwa na ufuatiliaji na tathmini? | | |
| 4.3. Je, kuna fedha za kutosha kwa ajili ya wafanyakazi kushiriki katika shughuli za kuongeza uwezo wa GESI, na mafunzo ya kuboresha ujuzi wa wafanyakazi? | | |
| **5. Mengineyo** | | |
| 5.1. Je, matokeo ya kina ya uchanganuzi wa GESI yamejumuishwa kwenye kiambatanisho cha andiko la mradi? | | |

# ZANA 3.2 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE USANIFU WA PROGRAMU

## LENGO

Zana hii ina lengo la kutoa mwongozo katika mchakato wa kusanifu programu/mradi, ambao hujumuisha uandaaji wa mkabala na mipango mbali mbali. Usanifu wa programu wenye muitikio wa GESI husaidia kuboresha kiwango cha matokeo katika ngazi ya mradi,kupunguza hatari ya madhara yasiyokusudiwa na kuhakikisha kuwa mahitaji na changamoto maalumu za watu na makundi mbalimbali zimeshughulikiwa katika programu.

Zana hii ina sehemu mbalimbali - sehemu moja kwa kila aina ya mkabala na mpango wa programu, ambao hutengenezwa wakati wa usanifu wa programu. Zana hii inazungumzia:

- Ujumuishaji wa GESI kwenye Lengo, Madhumuni, na Matokeo ya Programu
- Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Shughuli
- Ujumuishaji wa GESI kwenye Mkakati wa Kupunguza Athari
- Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini
- Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Kuajiri/ Kuongoza Timu

## NANI ANAPASWA KUTUMIA ZANA HII?

Zana hii imekusudiwa kutumiwa na timu za wasanifu wa programu, lakini pia inaweza kutumiwa na viongozi wa timu, maofisa wa bajeti na fedha, mameneja wa programu, wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini na wataalamu wa mambo ya jinsia ambao wanaweza kuwa wamechangia mchakato wa usanifu wa programu.

## JINSI YA KUTUMIA ZANA HII

Zana hii imepangiliwa kulingana na aina kuu za viunzi vya programu na mipango ambayo mara nyingi hutengenezwa kwenye hatua ya usanifu wa programu. Kila sehemu ina maelekezo na maswali ya mwongozo wa mchakato wa usanifu.[44] Kama timu ya usanifu inaamua kutengeneza jedwali la shughuli za mradi (log-frame), sehemu za zana hii zitatumika kuelezea kila sehemu ya jedwali la shughuli za mradi. Kwa mfano, mpango wa ufuatiliaji na tathmini unapaswa kuendana na viashiria, matokeo, na vyanzo vya uthibitisho vilivyoorodheshwa kwenye jedwali la shughuli za mradi.

**Kidokezo!**

Rejelea mara kwa mara matokeo ya uchanganuzi wa GESI ili kuendelea kuona uhalisia na uzoefu wa vikundi vya watu wanaolengwa na programu. Ni muhimu daima kukumbuka kwamba unasanifu programu hizi kwa ajili ya watu halisi katika jamii. Ikiwa umekwama kwenye namna ya kuhakikisha kama kila mpango, mfumo, au shughuli inaitikia GESI, basi rejelea mifano na marejeleo mahususi ya sekta.

Zana hii husaidia wafanyakazi wa shirika la World Vision kutazama kwa kina zaidi masuala ya GESI ndani ya vikoa vitano (upataji na kufikiaji, ufanyaji maamuzi, ushiriki, mifumo, na ustawi) kama mradi ulivyosanifiwa.Pamoja na kuwa shirika la World Vision linaweza kuwa tayari na zana madhubuti za kusanifu programu ambazo zinatumika katika ujumuishaji na uhusishaji wa masuala ya kijinsia, zana hii inaelezea kwa kina zaidi dhana nzima ya GESI.

Kabla ya kusanifu mifumo ya programu na shughuli zake, ni vema kufanya uchanganuzi wa GESI na kuchanganua data kwanza. Matokeo na maelezo ya kina yanayotokana na uchanganuzi wa GESI huweka msingi wa programu zinazoleta mabadiliko ya GESI.

44 Some guiding questions have been adapted from USAID (2013). How-to Note: Addressing Gender and Inclusiveness in Project Design.

## USHAURI WA MAANDALIZI

- Kusanya data zote zilizokusanywa wakati wa uchanganuzi wa GESI (angalia ZANA 2.1) ikiwa ni pamoja na mapitio ya maandiko,vitini vya mwezeshaji, maoni ya washiriki na uelewa uliopata
- Hakikisha data inawakilisha makundi mbalimbali ambayo mahitaji yake yatashughulikiwa kwenye usanifu wa programu
- Ikiwa kuna matokeo ya kustaabisha au kushangaza,wasiliana na wataalamu wa GESI na waalike kwenye vipindi vya kusanifu/kupanga programu
- Kwa kuongezea kama kuna mapungufu makubwa kwenye data iliyokusanywa (mfano baadhi ya makundi hayakuwekwa kwenye uchanganuzi wa GESI), tengeneza mpango wa kumaliza kukusanya data. Hakikisha timu ya wasanifu wa mradi (wakiwemo wale waliofanya uchanganuzi wa GESI) inahusisha makundi yote muhimu kama vile wanaume,wanawake,wavulana,wasichana wakiwemo watu wenye ulemavu na makundi yanayokandamizwa
- Hakikisha mbinu za kukusanya data zinaruhusu mawazo na uzoefu wa watu mbalimbali (wanawake, wanaume wavulana,wasichana wakiwemo watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi) kusikika
- Hakikisha kila sehemu ya mchakato iliyo na uwezekano wa kutohusisha mahitaji maalumu ya makundi yaliyotengwa, kama vile kuhakikisha muda na eneo la kufanyia usaili, majadiliano ya vikundi lengwa yanafanyika kwenye sehemu salama kwa watu wote, yanahusisha matumizi ya mtindo wa mawasiliano kwa walemavu kama vile kuwa na mkalimani wa lugha ya alama
- •Hakikisha kuwa shirika la World Vision na wabia wake wana uwezo na wamejitolea kusanifu miradi jumuishi yenye muitikio wa GESI. Kama sivyo, andaa mipango kwa ajili ya uimarishaji wa uwezo na uelewa kuhusu mikabala yenye muitikio na mabadiliko ya GESI.

## UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE LENGO, MADHUMUNI, NA MATOKEO YA PROGRAMU

Lengo na madhumuni yanaweza yasiwe yamelenga moja kwa moja kwenye usawa wa kijinsia au uhusishaji wa kijamii, lakini yanapaswa kushughulikia mahitaji na changamoto za watu na makundi yaliyobainishwa kwenye uchanganuzi wa GESI. GESI inapaswa kujumuishwa kwenye Nadharia ya Mabadiliko kama inavyoelezewa kwenye ZANA 1.1. Hakikisha kuwa lengo linaakisi tofauti za makundi mbalimbali ya kijamii (mfano jinsi,umri, ulemavu n.k) yaliyobainishwa wakati wa uchanganuzi na kuzingatia vigezo vifuatavyo:

- Madhumuni ya programu huchangia kuongezeka kwa ufanisi katika upataji na ufikiaji,ufanyaji maamuzi,ushiriki, mifumo na ustawi wa kundi moja au zaidi la watu waliokandamizwa
- Matokeo yanayotarajiwa yanakusudia kuhakikisha kuwa usawa wa fursa unatolewa kwa makundi yote ya kijamii na hili halitaleta vikwazo kwa baadhi ya makundi ya jamii kama watu wenye ulemavu
- Lengo na matokeo yanakusudia kuangalia changamoto za kijinsia,ulemavu na desturi zingine za kijamii ambazo kwa sasa zinasababisha kukandamizwa na kutengwa. Malengo na matokeo ya programu yanapaswa kushughulikia japo vikoa vitatu kati ya vitano
- Matokeo yanamaanisha mabadiliko yanayohusiana na GESI yanayotarajiwa kwa ajili ya makundi maalumu ya kijamii na pia kuhakikisha kuwa mabadiliko yanayotarajiwa yanawalenga wanawake, wanaume, wavulana,wasichana, waviulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yasiyohusishwa

**Jedwali 20 | Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Madhumuni, Lengo na Matokeo ya Programu**

| Mfano wa Sekta ya WASH | |
|---|---|
| Madhumuni ya Programu | Kuboresha afya miongoni mwa wanafunzi wa shule ya msingi |
| Lengo | Kuboresha upatikanaji wa maji salama ya kunywa mashuleni |
| Matokeo | Wasichana na wavulana, ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu, wanapata maji ya kunywa yaliyo salama kwa usawa |
| Vikoa ya GESI | Upataji na ufikiaji na ustawi |

## USANIFU KWA AJILI YA WOTE

Kanuni ya usanifu kwa ajili ya watu wote ilianza katika usanifu wa majengo(architecture). Wazo lilikuwa ni kujenga majengo yenye muundo unaokidhi mahitaji ya mtumiaji yeyote na majngo yaliyo bora kwa kila mtu. Kwa mfano, kuweka lifti, vidaraja, vyoo vinavyoweza kufikiwa, na milango mipana ni muhimu kwa watumiaji wa viti vya magurudumu lakini pia ni nzuri kwa watu ambao wana changamoto ya kupanda ngazi au wanaosukuma kigari cha kubebea mtoto.

Kanuni inamaanisha kwamba tunaweza kuhakikisha ufikiaji wa huduma kwa kila mtu ikiwa tutabuni huduma zinazokidhi mahitaji ya watu wanaoishi katika jamii za kijijini sana au za kuhamahama, ambao hawana usafiri, ambao hawawezi kusubiri kwa muda mrefu, ambao wanahitaji kusindikizwa na wanaume, wasio jua kusoma wala kuandika, wanaohitaji taarifa, na mtu wa kuwasaidia kujibu maswali kwa kilugha chao, wasio na pesa na wenye muda mchache, ambao hawana imani na serikali, ambao wanakabiliwa na hatari za kiusalama katika kupata na kufikia huduma zozote, ambao hawawezi kuwaacha watoto wengine nyumbani wanapohitaji kwenda kupata huduma.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia na baadhi ya hatua za kuchukua ili kutimiza mambo hayo. Tazama Kiambatanisho cha 3 chenye zana ya kuhakikisha ubora ili kubaini kama huduma unayotoa imesanifiwa kwa ajili ya watu wote kama inavyopaswa kuwa.

| KIKWAZO | HATUA UNAYOWEZA KUCHUKUA |
|---|---|
| **Lugha** | Kuweka wakalimani, toa taarifa katika lugha zote |
| **Mazingira hafifu** | Kuboresha mwanga ili kusaidia wale walio na uoni hafifu; kupunguza kelele; kuboresha mazingira kwa ujumla |
| **Utamaduni** | Kuajiri watu kutoka makundi yaliyo na watu wachache; kutoa mafunzo kwa watoa huduma ili wawe makini na mahitaji ya kitamaduni |
| **Umbali** | Kupeleka huduma kwa wahusika mahali walipo, au kutoa huduma kwenye makazi yao ili kuongeza huduma zilizopo |
| **Imani ya dini** | Kuwashirikisha viongozi wa dini katika mawasiliano kwa ajili ya mabadiliko ya tabia |
| **Fedha** | Kutenga bajeti ya mfuko wa ujumuishi ili kusaidia upataji na ufikiaji; kusaidia vikundi vya akiba au shughuli za kuongeza mapato; wakati upataji na ufikiaji unapaswa kuwa wa bure lakini sio wa bure, tumia utetezi |
| **Changamoto ya kutembea** | Kutoa vifaa vya usaidizi (kama viti vya magurudumu/magongo), usafiri unaoweza kufikiwa; vidaraja; vyoo vinavyopitika kwa viti vya magurudumu na vifaa vingine kwa ajili ya kula na kunawa kwenye jamii |
| **Vizuizi kwa mtu binafsi kusafiri na kufanya maamuzi** | Ziara za kaya ili kujadili ruhusa ya kupata huduma; mawasiliano ya mabadiliko ya tabia ili kuongeza uwezo wa mtu binafsi; utoaji ya kuwafuata wahitaji mahali walipo |
| **Mtazamo** | Mawasiliano ya kubadilisha tabia |
| **Malezi ya watoto** | Kutoa huduma za malezi ya watoto wakati wa kujifungua |
| **Usalama** | Kutoa huduma katika maeneo salama na nyakati ambazo zinafikiriwa kuwa ni salama |
| **Unyanyapaa/ ubaguzi** | Kuandamana na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi; kufanya kazi na watoa huduma kushughulikia unyanyapaa au ubaguzi wowote; kuhamasisha fikra/sifa nzuri juu ya makundi yasiyohusishwa |

## UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE MPANGO WA SHUGHULI

Shughuli hutengeneza msingi wa programu, kwa sababu wafanyakazi wa programu na washiriki hujihusisha mara kwa mara na shughuli kama vile mafunzo,warsha na mikutano. Pamoja na kwamba si shughuli zote zitalenga GESI kwa ufasaha, hata hivyo shughuli zote ni lazima zisanifiwe ili makundi yanayokandamizwa yaweze kujumishwa. Kwa kuongezea, shughuli maalumu zitahitajika ili kuwezesha programu kufanyia kazi mahitaji maalumu ya watu walio katika mazingira hatarishi. Pale ambapo GESI ni mada mtambuka na programu haina malengo au shughuli maalumu zinazohusiana na GESI, msanifu wa shughuli ni lazima azingatie namna ya kufanikisha malengo madogo na makubwa yanayohusiana na GESI. Kwa mfano, wakati wa kuandaa kikundi cha kuweka akiba, anaweza akazingatia kama maamuzi ya wanawake na upataji na ufikiaji vitaboreshwa kwa kuwahusisha wanawake hao na wenza wao ili kuendesha mjadala unaohusu mali za kifedha, au kama mwanzoni wanawake wanahitaji kutenganishwa na wanaume hadi watakapoweza kujenga uelewa na ujuzi wao. Unapofanya kazi ya usomaji wa madarasa ya awali, zingatia namna ambavyo kambi za usomaji zilizoko kwenye jamii zinaweza kuboreshwa ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali na walio katika mazingira hatarishi.

Daima tunapaswa kuunda shughuli zinazolingana na matokeo ya programu. Unaweza kutumia shughuli zifuatazo kulingana na malengo ya programu yako:

- Shughuli zinazojenga uwezo na kukuza uelewa wa wafanyakazi wa shirika la World Vision na wabia kuhusu taratibu zao wenyewe zinazohusu GESI na mitazamo kuhusu njia za kutekeleza mikabala yenye mabadiliko na muitikio wa GESI
- Shughuli zinazojumuisha mafunzo ili kuongeza elimu, ujuzi, na uwezo kwa makundi yanayokandamizwa ili kuboresha uwezo wao wa kupata na kufikia taarifa na kuongeza ushiriki na kunufaika na mradi. Mafunzo yote yanatakiwa yawe yanapatikana kwa urahisi, japokuwa kuna baadhi ya mafunzo yanaweza kulenga mahitaji maalumu ya baadi ya makundi. Kwa mfano, wanawake wanaweza kupewa mafunzo ya awali kuhusu jinsi serikali za mitaa zinavyoandaa bajeti kabla ya kuhudhuria mkutano wa umma unaojadili matumizi ya serikali za mitaa kwa mwaka unaofuata. Ni muhimu kuwashirikisha katika maboresho ili kushughulikia vikwazo vya ushiriki wao
- Shughuli zinazo hamasisha ongezeko la upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma, uongozi imara, ujumuishaji, ushiriki na ufanyaji maamuzi kwa watu mbalimbali katika jamii. Si mara zote shughuli hizi zinaongozwa au kusimamiwa na wafanyakazi wa shirika la World Vision
- Shughuli zinazoepuka uwezekano wa vikwazo vikubwa vya ushiriki, kwa mfano umbali mkubwa wa kusafiri hadi pale shughuli inapofanyikia, mazingira yasiyofikika kwa urahisi na huduma, uelewa wa lugha, huduma ya kumwangalia mtoto, upatikanaji wa muda, kiwango cha elimu, na uhuru wa mtu binafsi na kutembea
- Baadhi ya shughuli zinalenga makundi maalumu yanayokandamizwa ili kuweza kutatua mahitaji yao maalumu
- Shughuli zinazolenga kushughulikia masuala ya kijinsia, ulemavu, vikwazo vingine na fursa ili wanawake, wanaume, wavulana, wasichana, watu wenye ulemavu na makundi yaliyotengwa yashiriki, yafikie na yanufaike na mradi kwa usawa

**Jedwali 21 | Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Shughuli**

| Sekta ya Uwezeshaji wa Kiuchumi | | Kikoa cha GESI |
|---|---|---|
| Shughuli 1 | Mwezeshaji wa shirika la World Vision anawaongoza wanawake kwenye vikundi vya biashara na kuweka akiba | Ushiriki<br>Upataji na Ufikiaji |
| Shughuli 2 | Wanakikundi wanachagua viongozi wao na kuamua kuhusu mbinu za uwajibikaji wa kikundi zitakazowafanya wawe na nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu maslahi na sheria zao | Ufanyaji Maamuzi<br>Ustawi |
| Shughuli 3 | Shirika la World Vision linafundisha wanawake kupata ujuzi wa kuandaa bajeti, uhasibu na kuweka akiba | Upataji na Ufikiaji<br>Ushiriki |
| Shughuli 4 | Viongozi wa kikundi wanaendesha kipindi cha mpango wa biashara | Ushiriki |

## UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE MIKAKATI YA KUDHIBITI ATHARI

Kwa bahati mbaya, hata programu iliyokuwa na nia njema kabisa inaweza ikasababisha athari au matokeo hasi bila kukusudia kwa wafanyakazi na washiriki wa programu.Ili kuepuka madhara na matokeo hasi kwa makundi maalumu na kuhimiza usawa kwenye upataji na ufikiaji,ushiriki,uongozi na ufanyaji maamuzi miongoni mwa makundi ya kijamii kwenye mradi au programu, ni muhimu kuweka mikakati ambayo italenga kupunguza hatari na madhara ambayo watu waliokandamizwa wanaweza kukumbana nayo zaidi. Ingawa baadhi ya madhara yanaweza kuwa yalishabainishwa kwenye zoezi la uchanganuzi wa GESI, bado ni vema kuangalia madhara mengine ya ziada ambayo hayakukusudiwa tangu pale programu ilipokuwa inasanifiwa. Hii itasaida kudhibiti madhara ya GESI kadiri yatakavyojitokeza wakati wa mijadala inayohusiana na shughuli. Zingatia endapo shughuli za programu zinaweza kusababisha jambo lolote kati ya haya yaliyo orodheshwa kwenye Kielelezo 5.

**Kielelezo 5 | Athari Zinazoweza Kusababishwa na Shughuli za Programu**

| ATHARI | UKOSEFU WA MUDA | KUTOKUJALI MIGOGORO |
|---|---|---|
| • Kuongezeka kwa ubaguzi au unyanyapaa wa kundi la kijamii<br>• Kuendelea, kuongezeka au kutengeneza mila kandamizi kama vile ukatili wa kijinsia<br>• Wafanyakazi wa programu na/ au washiriki wa programu hawaheshimiwi au wanabaguliwa<br>• Wafanyakazi wa programu na/ au washiriki wa programu wako katika mazingira ya hatari na/au sehemu zisizofikika<br>• Ushiriki una gharama | • Kuongezeka kwa muda, kazi au majukumu kwa watu au kundi fulani<br>• Baadhi ya watu kushindwa kushiriki kutokana na kukosa muda kama vile kulea watoto na muda usiofaa kwa ajili ya kufanya mikutano na wanawake | • Pembejeo,huduma au rasilimali zinazotolewa kuleta mgawanyiko katika familia au mvutano kwenye jamii<br>• Pembejeo,huduma au rasilimali zinazotolewa zinatumika kwenye madhumuni yenye madhara yasiyotarajiwa<br>• Pembejeo,huduma au rasilimali zinazotolewa zinatumika kwa watu wasiokusudiwa |

Baada ya kubainisha hatari na madhara yasiyokusudiwa, andaa mbinu za ziada zinazoweza kutumiwa kupunguza madhara na athari kwenye programu. Angalia jedwali hapa chini la mikakati ya kupunguza madhara. Kama mkakati unahitaji rasilimali na shughuli zaidi, ongeza hio mikakati kwenye mipango ya shughuli na bajeti

**Jedwali 22 | Mfano wa Ujumuishaji wa GESI kwenye Mkakati wa Kudhibiti Athari**

| Mfano wa Sekta ya Msaada wa Kibinadamu na Dharura | | |
|---|---|---|
| **Athari Mbaya Zisizokusudiwa** | **Mkakati wa Kudhibiti Athari** | **Kikoa cha GESI** |
| 1. Wanawake wanakumbana na upinzani kutoka kwa wenza wao pale wanapopata msaada wa ziada | Fanya mikutano na wanaume na wanawake ili kujadili kwa uwazi kuhusu madhumuni ya programu na manufaa yanayokusudiwa kwa makundi lengwa | Ushiriki<br>Mifumo |
| 2. Watu wasiokusudiwa ndio wanaopatiwa mgao wa chakula | Fuatilia usambazaji wa chakula unaoshughulikiwa na kila mfanyakazi na mtendaji wa soko kupitia mfumo wa uwajibikaji | Upataji na Ufikiaji |
| 3. Wanufaika wenye ulemavu wanapata msaada ambao hauzingatii hali zao maalumu | Tengeneza tathmini ya mwanzo ya mahitaji maalumu | Upataji na Ufikiaji |
| 4. Wanufaika hawana uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu rasilimali na huduma wanazopata kutoka kwenye misaada ya kibinadamu | Bainisha njia za kuwawezesha washiriki katika kufanya maamuzi haya | Ufanyaji Maamuzi |
| 5. Msaada wa kibinadamu unatolewa kwa baadhi ya washiriki | Hakikisha kuna usawa na usalama kwenye upataji na ufikiaji wa rasilimali na huduma zinazotolewa na misaada ya kibinadamu ili kushughulikia mahitaji ya wanawake, wanaume,wasichana, wavulana, na watu wenye ulemavu. Husisha makundi yanayotengwa katika maamuzi yanayohusiana na huduma | Upataji na Ufikiaji<br>Ufanyaji Maamuzi<br>Mifumo<br>Ustawi |

## UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE MPANGO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Mpango wa ufuatiliaji na tathmini unatakiwa kujumuisha mbinu za kukusanya data, viashiria na matokeo yanayotarajiwa yenye muitikio wa GESI. Unapochagua mbinu za kukusanya na kuchanganua data zitakazoingizwa katika mpango wa ufuatiliaji na tathmini, (rejea zana zilizoko kwenye sehemu 2 na 3) na hakikisha wafanyakazi wote watakaohusika kukusanya data wanasoma hiyo miongozo. Unapochagua viashiria kwa ajili ya programu, huna budi kurejea ZANA 3.3. Ifuatayo ni mfano ya orodha ambazo unaweza kutumia kuhakikisha kuwa kila kipengele cha mpango wa ufuatiliaji natathmini kina muitikio wa GESI.

**Jedwali 23 | Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini**

| Orodha kwa ajili ya Ujumuishaji wa GESI kwenye Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini |
|---|
| **1. Mpango wa Ukusanyaji Data** |
| 1.1. Data zitagawanywa kwa jinsi, umri, hali ya ulemavu na sifa zingine. |
| 1.2 Mapungufu katika data za GESI yanashughulikiwa na kuwekwa. Kwa mfano, kama dini imebainishwa kama chanzo cha ubaguzi wakati wa uchanganuzi wa GESI, chagua kukusanya na kuchanganua data kwa aina ya dini. |
| 1.3. Mbinu za kukusanya data ni za kitakwimu na kitaamuli na zinatumia zaidi ya mbinu moja au mbili. |
| 1.4. Je, mbinu za kukusanya data ni shirikishi na zinahusisha makundi mbalimbali ya kijamii kwa usahihi? Kwa mfano kama kukusanya data kwa watoto kumelenga kwenye kiwango chao cha uelewa na kuhimiza ushiriki mzuri. |
| 1.5. Ukusanyaji data unapangwa kufanywa na mwezeshaji na wakusanya data walioshiriki kwenye mafunzo ya GESI ya shirika la World Vision. |
| 1.6. Mbinu za kukusanya data zimepangwa kupima ushiriki sawa wa wanaume na wanawake pamoja na watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Pia ukusanyaji data hupima ufanisi na athari za mradi kwa watu walio katika mazingira hatarishi. |
| 1.7. Mpango wa kukusanya data huruhusu kupima mabadiliko na mienendo katika mahusiano ya kijinsia na kijamii baada ya kipindi fulani. |
| **2. Viashiria na Mpango wa Uchanganuzi wa Data** |
| 2.1. Viashiria mtambuka na mahususi vya kisekta vya GESI vinachaguliwa kulingana na lengo na madhumuni ya programu. |
| 2.2. Viashiria vilivyochaguliwa ni angalau vikoa vitatu kati ya vitano vya GESI vya shirika la World Vision — Upataji na ufikiaji,ufanyaji maamuzi,ushiriki,mifumo, na ustawi. |
| 2.3. Viashiria vilivyochaguliwa ni vya kitakwimu na kitaamuli. |
| 2.4. Matriki za uchanganuzi wa data zinalinganisha majibu ya wanaume,wanawake,wasichana na wavulana wakiwemo watu wenye ulemavu na makundi mengine yasiyohusishwa. |
| 2.5. Uchanganuzi wa data na tafsiri zinabainisha masuala ya GESI yenye umuhimu zaidi kwa makundi mbalimbali ya kijamii, na mazingira hatarishi kwa wanaume,wanawake,wasichana, wavulana na watu wenye ulemavu na makundi mengine yasiyohusishwa. |
| **3. Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini** |
| 3.1. Je, viashiria vya GESI vimebainishwa na kuingizwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wakati wa usanifu na upangaji wa programu? |
| 3.2. Je, viashiria vya GESI vilivyowekwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji na tathmini vitasaidia kupima matokeo ya GESI, kama vile viwango vya ushiriki vya wanawake, wanaume na/au watu wenye ulemavu katika utekelezaji wa program? |
| 3.3. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaruhusu kukusanya data zinazofuatilia tofauti za faida za programu kwa wanawake, wanaume, na makundi mengine yanayokandamizwa? |
| 3.4. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini umeundwa kukusanya data za GESI ziliyogawanywa? |

| |
|---|
| 3.5. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unawezesha kulinganisha matokeo kwa muda fulani? |
| 3.6. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unawezesha ukusanyaji wa data zinazoonyesha kama malengo, matokeo, and ufanisi umefikiwa kwa wanawake, wanaume, na makundi mengine yanayokandamizwa? |
| 3.7. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unasaidia kupima mabadiliko na mwenendo kwenye upatikanaji na ufikiaji,ufanyaji maamuzi,ushiriki,mifumo, na ustawi? mienendo kati ya makundi yanayotengwa na yasiyotengwa kwa kipindi cha muda fulani, na pia kutambua sababu za mabadiliko hayo? |
| 3.8. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaruhusu ukusanyaji wa taarifa juu ya vigezo ambavyo vinaweza kuelezea kama malengo ya programu na mradi yamefikiwa kwa ajili ya wanawake,wanaume,wasichana,wavulana na makundi mengine yanayokandamizwa? |
| 3.9. Je, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaruhusu ukusanyaji wa taarifa juu ya vigezo ambavyo vinaweza kufuatilia kama kuna tofauti kubwa katika faida za programu kwa wanawake,wanaume,wasichana,wavulana na makundi mengine yanayokandamizwa? |
| 3.10. Tathmini inayopendekezwa inahusisha maswali mbalimbali ya tathmini yanayohusu namna ambavyo programu inashughulikia usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kwa kulenga vikoa vya GESI vya shirika la World Vision. |
| 3.11. Mipango ya tathmini inayopendekezwa inawakilisha kwa usawa makundi ya kijamii yaliyo katika mazingira hatarishi kwenye mchakato wote wa tathmini na kushirikisha na kuweka kumbukumbu za uzoefu juu wa usawa wa kijinsia, ushirikishaji wa watu wenye walemavu, kama vile mambo ya kujifunza na hadithi za mafanikio. |

## ZANA 3.3 VIASHIRIA VYA GESI

Zana hii hujumuisha safu yenye mifano ya viashiria vya GESI ambayo vinakusudia kupima mabadiliko ya programu. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya viashiria vya GESI kunaweza kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Hii inawezesha ukusanyaji na uchanganuzi wa data iliyogawanywa kwa jinsi, hali ya ulemavu na sifa zingine. Kutumia viashiria mbalimbali vya kitakwimu na kitaamuli husaidia timu za programu kutathmini na kufuatilia jinsi programu zinavyoshughulikia mahitaji na changamoto za makundi mbalimbali ya watu wanaokandamizwa, na kuwezesha uwepo wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.

### MALENGO YA VIASHIRIA VYA GESI

- Kuongoza timu ya ufuatiliaji na tathmini kwenye upimaji wa maendeleo ya programu katika kufikia matokeo ya programu yenye muitikio wa GESI
- Kusaidia kukusanya ushahidi wa mchango sahihi na wa kina kuhusu namna ambavyo makundi ya watu wanaokandamizwa yanazichukulia na kufaidika na programu za shirika la World Vision

### MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA VIASHIRIA VYA GESI

Kuna njia mbili za kutofautisha viashiria vya GESI: Viashiria vinavyohusiana na GESI na viashiria vinavyolenga GESI.

**Viashiria vinavyohusiana na GESI**

Viashiria vinavyogawanya data za matokeo ya programu kwa sifa za GESI kama vile jinsi au hali ya ulemavu.

- Kugawanya kiashiria kwa jinsi inamaanisha kuwa data inagawanywa kwa wanawake, wanaume na hali ya ulemavu. Kwa mfano:
- Idadi ya watoto wanaopata na kufikia sehemu rafiki kwa watoto, kwa jinsi na hali ya ulemavu
- Asilimia ya watoto wa darasa la 3 wanaopata japo kiwango cha chini cha uwezo wa kujua kusoma, kwa jinsi na hali ya ulemavu

**Viashiria vinavyolenga GESI**

Viashiria vinavyokusanya data zinazohusu matokeo ya programu kwa kundi au sifa maalumu ya GESI. Mara nyingi, viashiria hivi huonyesha kama kuna ukosefu wa usawa wa GESI miongoni mwa wanawake,wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Viashiria hivi pia huonyesha nini kifanyike ili kushughulikia mapungufu ya GESI, kufuatilia mabadiliko katika utekelezaji wa programu yenye muitikio wa GESI, na kuongeza uelewa wa masuala ya kipekee yanayoathiri kundi maalumu la kijamii. Mfano wa viashiria vinavyolenga GESI ni:

- Asilimia ya wanawake, wanaume na watu wenye ulemavu ambao ni washiriki wa programu iliyosanifiwa kwa ajili ya kuongeza upataji na ufikiaji wa rasilimali za uzalishaji kiuchumi (mali, mikopo, kipato au ajira)
- Asilimia ya wanaume na wanawake wanaoishi kama wanandoa na walio na kipato cha fedha na wanaofanya maamuzi kwa pamoja na wenza wao kuhusu matumizi ya fedha walizopata (self-earned cash)
- Timu za programu zinapaswa kuchagua kundi moja au yote mawili ya viashiria vya GESI kulingana na nadharia ya mabadiliko ya programu yao, malengo ya kukusanya data,kiwango cha afua, na namna data zitakavyotumika kuhimiza GESI.

**Viashiria vya Kitakwimu na Kitaamuli**

Viashiria vya GESI vyaweza kuwa vya kitakwimu au vya kitaamuli. Chagua aina ya viashiria vyote viwili yaani vya kitakwimu na kitaamuli ili kuhakikisha unapata uelewa kamili na wa kina juu ya namna ambavyo desturi na mienendo ya kijinsia na kijamii hubadilika.

**Kielelezo 6 | Mambo Muhimu ya Kuzingatia Katika Kuchagua Viashiria**

**Viashiria vya Kitakwimu**

- Hukusanya data za takwimu zlizogawanywa za GESI na hutoa mbinu tofauti kwa wanawake na wanaume kwa ulemavu na sifa zingine za kijamii
- Hulenga kwenye masuala yanayoweza kuhesabika kama vile asilimia ya wanawake na wanaume walio na upataji na ufikiaji wa maji salama, au kiwango cha mahudhurio ya shule kwa wasichana, wavulana, na watoto wenye ulemavu
- Huonyesha kiwango cha mabadiliko kwenye masuala ya GESI kwa kipindi fulani – kama vile idadi ya makundi ya wakulima yanayoongozwa na wanawake kulinganisha na yale ya wanaume
- Data hukusanywa kupitia njia za kawaida kama tafiti za kaya, hufafanuliwa kupitia uchanganuzi wa kitakwimu, na ufafanuzi hutofautishwa kutoka kwenye matukio yaliyoelezwa. Mfano, hali ya kipato haielezi jitahada zinazofanywa na wanawake au wanaume kujipatia kipato.
- Inaweza kuelezewa kama namba ya watu walioripoti au walioeleza jambo fulani, au asilimia ya mabadiliko, hii inaruhusu kutumia takwimu.

**Viashiria vya Kitaamuli**

- Hujumuisha viashiria vinavyohusiana na maoni ya washiriki, hisia, uzoefu, mitazamo, ujuzi, na kiwango cha ufahamu
- Mara nyingi hufikiriwa kama "wale wanaoripoti x," au "mitazamo ya x" au "kiwango cha x"
- Ni muhimu kwenye upimaji wa mabadiliko katika usawa wa kijinsia na ushirikishaji wa kijamii kwa sababu husaidia kufichua vyanzo vya kutengwa na ubaguzi

## KUGAWANYA VIASHIRIA VYA GESI

Viashiria ambavyo hurejelea "watu" au "watoto"wakati wote vinapaswa kugawanywa kwa sifa mbalimbali. Ikiwa kiashiria kinarejelea maamuzi ya pamoja kwenye kaya,basi itakuwa sahihi kukigawanywa kwa jinsi na hadhi ya kijamii na kiuchumi. Kwa viashiria vingine, inaweza kufaa kugawanya matokeo kulingana na sifa mbalimbali au zaidi za kijamii na makundi (mfano "watoto" wanaweza kugawanywa kama "wavulana,wasichana na watoto wenye ulemavu"). Kiwango na aina ya ugawaji hutegemea dhumuni la kiashia.

## VIASHIRIA VYA GESI MAALUMU KWA SEKTA NA VISIVYO NA SEKTA MAALUMU

Kwa viashiria vingi vya GESI,inawezekana kuvihusisha na sekta maalumu kama vile afya, WASH, elimu na shughuli za kujipatia riziki. Kwa mfano kiashiria kama "*asilimia ya watoto wa miaka 12-18 ambao wamekumbana na ukatili wa kimwili na kingono kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa jinsi*" mara nyingi hupimwa na programu kwenye Sekta ya Ulinzi wa Mtoto. Hata hivyo,kulingana na ujumuishaji wa programu nyingi, timu ya programu inapaswa kuzingatia pia kuchagua viashiria mtambuka ili kuboresha data zao za programu.Viashiria kama vile, *asilimia ya wanawake,wanaume, na watu wenye ulemavu walioripoti kuwa walishiriki kwenye mikutano ya kijamii au makundi mengine* " inaweza kupimwa na programu yoyote pasipo kujali muegemeo wa sekta ya programu.

**Mambo Mengine ya Kuzingatia**

- Hakikisha wabia na watekelezaji wa programu wana uwezo wa kukusanya na kuchanganua data zilizogawanywa
- Hakikisha viashiria vinaeleweka kirahisi kwa wakusanya data na timu ya ufuatiliaji na tathmini kama kufasili kila kiashiria. Pia hakikisha kwamba viashiria vimefasiliwa kwa namna ambayo haitumii maneno yenye maana hasi kama vile "kilema"
- Angalia kama viashiria vinaweza kuwaongezea wabia jukumu jipya la kuleta kuripoti na kama viashiria vinaendana na majukumu ya kuripoti yaliyopo
- Hakikisha kuwa mbinu zote za kitakwimu na kitaamuli zinatumika kukusanya taarifa za kila kiashiria kilichochaguliwa
- Hakikisha uchanganuzi wa GESI na mapendekezo yake yametumiwa katika kusaidia kuchagua viashiria sahihi na vinavyofaa vya GESI
- Hakikisha kwamba kila kiashiria kinafanikisha usimamizi wa programu

## MIFANO YA VIASHIRIA VYA SEKTA YA PROGRAMU

Jedwali hapa chini linaonyesha mifano ya viashiria vya GESI vilivyochukuliwa kutoka kwenye miundo ya ufuatiliaji na tathmini ya shirika la World Vision na mashirika mbalimbali. Viashiria hivi vimelinganishwa na vikoa vya GESI vya shirika la World Vision vya sekta ya programu na kiwango cha matokeo. Orodha ya ziada ya viashiria vya GESI vimewekwa kwenye Kiambatanisho 4. Wataalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini na wafanyakazi wengine wa programu wanapaswa kutumia orodha hizi katika kuchagua viashiria vya GESI ambavyo vinafaa zaidi kwenye programu yao. Viashiria vinapimwa zaidi na kiwango cha matokeo kama matokeo makubwa, matokeo madogo na matokeo ya ingizo na vinategemea na shughuli maalumu za programu, hivyo vinaweza kutumika kufuatana mahitaji hayo.

**Jedwali 24 | Viashiria vya GESI vya Shirika la World Vision kwa Sekta ya Programu, Kikoa cha GESI, na Kiwango cha Matokeo**

| Sekta | Kiashiria | Kikoa cha GESI | Kiwango cha Matokeo |
|---|---|---|---|
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Uwiano wa watoto wa darasa la 3 walifikia angalau kiwango cha chini cha uwezo wa kusoma, kwa jinsi na hali ya ulemavu | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Asilimia ya watoto wenye umri kati ya miaka 12-18 wanaokumbana na ukatili wa mwili au wa kingono kwenye kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa jinsi | Ustawi | Matokeo makubwa |
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Asilimia ya wasichana na wavulana wenye umri kati ya miaka 12-18 wanaofahamu sehemu wanazoweza kwenda ili kupata msaada endapo watakuwa wamekumbana na ukatili wa mwili au wa kingono | Ustawi | Matokeo makubwa |
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Asilimia ya washiriki walioripoti kuongezeka kwa kukubalika kwa dhana kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kuwa na usawa katika upataji na ufikiaji wa rasimali za kijamii,kiuchumi na kisiasa na fursa, kwa jinsi | Mifumo | Matokeo makubwa |
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Watoto waliopatiwa chanjo muhimu, kwa jinsi na umri | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Ulinzi wa Mtoto na Elimu | Asilimia ya watoto wanaopata mahitaji muhimu ya shule- sare za shule,vitabu,umeme kwa ajili ya kumalizia kazi za masomo nyumbani, kwa jinsi na ulemavu | Upataji na Ufikiaji | Matokeo madogo |
| Usalama wa Chakula na Riziki | Asilimia ya washiriki ambao ni wanawake katika programu inayolenga kuongeza upatikanaji na ufikiaji wa rasilimali za kuzalisha uchumi (mali, mikopo,kipato au ajira) | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Usalama wa Chakula na Riziki | Asilimia ya wanawake na wanaume wanaoishi kama wanandoa ambao wana kipato cha fedha na wanaofanya maamuzi kwa pamoja na wenza wao kuhusu matumizi ya fedha binafsi zilizopatikana | Ufanyaji Maamuzi | Matokeo makubwa |
| Usalama wa Chakula na Riziki | Asilimia ya wahojiwa ambao wanafikiri wanaume na wanawake wanapaswa kufanya kazi za nyumbani kwa pamoja kama vile kufanya usafi,kupika na kulea watoto, kwa jinsi | Ushiriki | Matokeo makubwa |
| Usalama wa Chakula na Riziki | Idadi ya wanaume, wanawake na watu wenye ulemavu wanaopata na kufikia taarifa na mafunzo kutoka kwa wakala wa kilimo au vituo/shule za kilimo | Upataji na Ufikiaji/ Mifumo | Matokeo madogo |
| Afya | Uwiano wa wanawake wanaopata na kufikia huduma za uzazi katika umbali wa chini ya saa moja kwa kutembea | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Afya | Idadi ya masaa yanayotumiwa na wanaume na wanawake kuhudumia wagonjwa | Ushiriki | Matokeo makubwa |
| Afya | Ushahidi kwamba vikwazo vya kisheria vinawazuia wanawake kupata huduma za uzazi vimeondolewa | Mifumo | Matokeo makubwa |
| Afya | Kiwango ambacho wanaume,wanawake, na watu wenye ulemavu wanajisikia kuwa wanahudumiwa na wahudumu wa afya kwa heshima na utu | Ustawi | Matokeo makubwa |

| Sekta | Kiashiria | Kikoa cha GESI | Kiwango cha Matokeo |
|---|---|---|---|
| Afya | Asilimia ya watoto wenye umri wa miezi 0-23 ambao walizaliwa takribani miezi 33 baada ya mtoto aliyezaliwa kabla yao ambaye yuko hai, kwa jinsi | Ustawi | Matokeo makubwa |
| Dharura ya Kibinadamu/ Ulinzi | Idadi ya watoto wanaopata na kufikia maeneo rafiki kwa watoto, kwa jinsi na hali ya ulemavu | Upataji na Ufikiaji<br>Mifumo | Matokeo madogo |
| Dharura ya Kibinadamu | Ushahidi kwamba mgawanyo wa chakula umepangwa ili kupunguza uwezekano wa athari za kiafya, muda wa kusubiri, na muda wa kusafiri kwa wanaume,wanawake na watu wenye ulemavu | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Dharura ya Kibinadamu | Ushahidi kuwa wanaume,wanawake, na watu wenye ulemavu wanapata na wanafikia maji na vyoo ambavyo vinafaa kulingana na mila zao, vina mwanga wa kutosha, na viko kwenye maeneo salama | Upataji na Ufikiaji | Matokeo makubwa |
| Dharura ya Kibinadamu | Idadi na asilimia ya wanaume,wanawake na watu wenye ulemavu wanaopata misaada ya kifedha au mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli za kujipatia riziki | Upataji na Ufikiaji | Matokeo madogo |
| Maji, usafi wa mwili na mazingira (WASH) | Idadi na asilimia ya wavulana na wasichana wanao shiriki katika shughuli za usafi wa kimwili, mazingira na vyoo shuleni na nyumbani | Upataji na Ufikiaji | Matokeo madogo |
| Maji, usafi wa mwili na mazingira (WASH) | Asilimia ya wanaume,wanawake na watu wenye ulemavu wanaoshiriki kwenye vyama vya watumiaji wa maji | Ushiriki | Matokeo makubwa |
| Maji, usafi wa mwili na mazingira (WASH) | Kiwango cha wanaume na wanawake kuridhika juu ya mgawanyo wa muda na nguvu iliyotumika kuchota maji kwa wanawake | Ustawi | Matokeo makubwa |

## ZANA 3.4 MPANGO KAZI WA UJUMUISHAJI WA GESI

Zana ya mpango kazi wa ujumuishaji wa GESI[45] inaonyesha mwelekeo wa programu katika kufanikisha ujumuishaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii katika mzunguko mzima wa mradi. Zana hii inaweza kuisaidia timu ya mradi kuhakikisha washiriki walengwa wote wanapata kwa usawa faida na fursa za mradi pasipo kujali sifa zao za kijamii na kiuchumi (jinsi,umri,hali ya ulemavu,kipato na mengine) kwa kuweka ujumuishaji na kuzingatia uhusishaji wa kijamii kwenye usanifu wa mradi na mzunguko mzima wa mradi.

### MALENGO YA MPANGO KAZI WA GESI

- Kuhakikisha mradi unazingatia mahitaji mbalimbali, vipaumbele, matakwa na uwezo wa kila kundi katika jamii (wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu n.k.) walio miongoni mwa walengwa na kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii na hasara zake
- Kueleza mikakati na hatua mahususi za GESI zitakazochukuliwa ndani ya mradi ili kuhakikisha kwamba wanaume na wanawake, wavulana, wasichana na watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki na kufaidika na afua za mradi kwa usawa
- Kuweka katika waraka mmoja vitendo na mikakati mahususi inayohusiana na GESI ili kutumika kama ramani ya mwelekeo wa GESI kwa timu ya mradi

45 Adapted from World Vision Australia Gender Mainstreaming Action Plan (GAP).

- Kuhakikisha kuwa hatua za kudhibiti athari za 'usidhuru' zitachukuliwa ili kuepuka matokeo mabaya ya mradi yanayoweza kutokea kwa makundi mbalimbali ya kijamii yaliyo katika mazingira hatarishi (kama wanawake, wasichana, watu wenye ulemavu, na watu walio na hali ya chini kiuchumi) ikiwa ni pamoja na athari kwa hadhi, mahusiano ya kijamii katika kaya, na kiwango cha majukumu ya kazi zao
- Kuhakikisha kuwa matokeo na mapendekezo kutokana na uchanganuzi wa GESI yanatumika katika usanifu na utekelezaji wa mradi
- Kuwajibisha timu ya mradi na washirika kwa kujumuisha GESI na kutekeleza afua zinazohusiana na GESI katika mzunguko wa mradi

## UNAPASWA KUFANYIKA LINI?

Mpango kazi wa ujumuishaji wa GESI unapaswa kuwa sehemu muhimu ya usanifu wa mradi, kulingana na matokeo na mapendekezo yaliyotokana na uchanganuzi wa GESI na/au tathmini zingine zenye muitikio wa GESI.[46] IMpango kazi unaweza kutengenezwa kwenye hatua ya mwisho ya mradi, kama ikibidi. Inashauriwa kujumuisha mpango kazi wa GESI kwenye Mpango wa wa Utekelezaji wa Mradi wenye Maelezo ya Kina. Maelezo ya kina yanaweza kutolewa kwenye mpango kazi na lugha ya hatua za kujumuisha GESI inaweza kuongezwa kwenye mpango wa usanifu,ufuatiliaji na tathmini.

## NANI ANAPASWA KUTUMIA ZANA HII?

Zana hii ni kwa ajili ya timu ya watendaji wote katika mradi, lakini ni muhimu zaidi kwa mameneja wa mradi na washauri wa masuala ya kijinsia na uhusishaji wa kijamii.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA[47]

1. **Fanya uchanganuzi bora wa GESI:** Tumia matokeo kutoka kwenye uchanganuzi wa GESI kutengeneza mpango kazi wa ujumuishaji wa GESI. Timu ya mradi na wabia wanahitaji kupitia matokeo na mapendekezo ya uchanganuzi wa GESI kwa ushirikiano. Kama sehemu ya mchakato huu shirikishi, tengeneza mipango na mikakati ya GESI itakayowekwa katika mpango kazi ili umilikiwe na kufahamika kwa timu yote ya mradi.

2. **Bainisha masuala ya GESI yenye kipaumbele na sababu za kuchukua hatua:** Eleza kwa kifupi vipaumbele vya masuala ya GESI vilivyobainishwa kwenye uchanganuzi wa GESI (au kutokana na tathmini zingine zenye muitikio wa GESI kama zipo) na/au ripoti za mradi na tathmini, na sababu za msingi za kuchukua hatua ili kujumisha GESI. Kwa mfano, kwa mradi wa lishe, chunguza kuenea na kukubalika kwa tabia ya wanaume kuwa wa kwanza kula na bainisha hatua za GESI ili kushughulikia tabia hii. Katika mradi wa kuwezesha watu kupata riziki, angalia kama ufanyaji maamuzi kuhusu matumizi ya fedha unaripotiwa kama kisababishi cha ugomvi au ukatili kati ya wanandoa, na kisha eleza hatua za kudhibiti athari hii.

3. **Malengo, matokeo makubwa na matokeo madogo:** Bainisha kwa uwazi, malengo mahususi yanayohusiana na matokeo makubwa na madogo ya GESI ambayo yatawezesha kushughulikia mapungufu na masuala yaliyobainishwa wakati wa uchanganuzi wa GESI.

4. **Hatua za GESI:** Bainisha hatua za GESI zinazohitajika ili kufikia malengo, matokeo makubwa na madogo. Hatua za GESI zitategemea mradi, masuala yaliyobainishwa, rasilimali zilizopo, n.k. Hakikisha hatua za GESI zinaongozwa na kuungwa mkono na timu ya wataalamu mahiri ya GESI, iliyowekewa bajeti (iwe ya kutoka ndani ya World Vision, nje, au sehemu zote mbili). Tenga rasilimali za kutosha zinazohitajika kwa utekelezaji mzuri wa shughuli za GESI. Hakikisha kuna timu ya muda mrefu ya wataalamu wa GESI ndani ya timu ya mradi ili kuongoza, kusaidia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji

46 Adapted from World Vision Australia Gender Mainstreaming Action Plan (GAP).
47 ADB (2013b). Preparing a Project's Gender Action Plan.

wa hatuza za GESI. Pale inapowezekana, jumuisha watu wawili wa kaya moja ( hasa wenzi/wanandoa) katika mafunzo ya kiufundi na matukio mengine ya kujenga uwezo yanayofanywa na mradi. Mifano wa hatua za GESI inaweza kuwa:

- Wakati wa kupanga ratiba ya mafunzo na shughuli nyingine za kujenga uwezo, wafanyakazi wa mradi huzingatia kiwango cha majukumu na ratiba za wanawake, ikiwa ni pamoja na majukumu ya malezi ya watoto, pamoja na mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu.
- Bajeti ya mradi inajumuisha fungu la fedha kwa ajili ya wafanyakazi kushiriki katika mafunzo, pamoja na fedha za usafiri ili kuwawezesha wanawake wenye watoto wadogo na watu wenye ulemavu kuhudhuria mikutano na mafunzo muhimu ya mradi husika.
- Kutoa motisha utakao hamasisha washiriki kutoka katika makundi yaliyotengwa kuhudhuria katika shughuli za mradi, kwa mfano kuwapa huduma/manufaa yanayogusa maslahi na mahitaji yao.

5. **Shughuli za mradi:** Kama sehemu ya maandalizi ya mpango kazi wa GESI, ni muhimu kuorodhesha shughuli zote za mradi au baadhi ya shughuli kutoka katika usanifu wa mradi zinazohitaji kujumuisha GESI. Baada ya mpango kazi wa GESI kukamilika, timu ya wafanyakazi wa mradi inaweza kuamua kufuta safu-wima, au kurekebisha jedwali la mpango kazi wa GESI kadiri itakavyotakiwa, au kuziacha shughuli za mradi kama safu-wima ya kwanza.

6. **Tumia viashiria na malengo ya GESI:** Weka viashiria vya GESI katika matokeo makubwa na/au katika matokeo madogo kwenye mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa jedwali la shughuli za mradi (log-frame), kama itafaa.Vinginevyo kuwa huru kuondoa safu-wima hii. Wafanyakazi wengine wanaweza kuongeza viashiria vya ziada na malengo ya GESI kwa ajili ya hatua za GESI zilizobainishwa, ingawa hizi zitakuwa nje ya jedwali la shughuli za mradi.

7. **Majukumu:** Ainisha majukumu yatakayofanikisha hatua za GESI. Orodhesha wafanyakazi wa mradi/wabia ambao wanahusika na kila jukumu na andika msaada unaotakiwa au unaohitajika kutoka katika ngazi za ofisi kuu za World Vision katika nchi (National Office), ofisi za kikanda (Regional Office), na makao makuu (Global Center), n.k.

8. **Muda wa utekelezaji:** Bainisha muda(mwaka/miaka) ambao majukumu yote yatatekelezwa.

Kidokezo!

Jumuisha jumbe na maudhui ya GESI katika nyenzo zote za mafunzo ya mradi, matukio ya kujenga uwezo na ya kukuza ufahamu yanayoendeshwa na wabia na jamii ili ujumbe wa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii uwasilishwe kwa washiriki mara kwa mara na kutoka vyanzo mbalimbali.

Hakikisha kwamba hatua za usawa wa kijinsia zinaongozwa na mtaalamu na mshauri mahiri aliyewekwa kwenye bajeti (iwe wa ndani ya World Vision, wa nje, au zote mbili).

**Jedwali 25 | Mpango Kazi wa Ujumuishaji wa GESI**

| Shughuli za Mradi | Masuala ya GESI yenye kipaumbele na sababu za kuchukua hatua | Hatua za GESI | Viashiria na malengo ya GESI | Majukumu | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| Nini? | Kwa nini? | Kwa namna gani ? | Yapi? | Nani? | Lini? |
| Lengo: | | | | | |
| Matokeo makubwa #: | | | | | |
| Matokeo madogo #: | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| Matokeo makubwa #: | | | | | |
| Matokeo madogo #: | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| Matokeo makubwa #: | | | | | |
| Matokeo madogo #: | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

## ZANA 3.5 UANDAAJI WA BAJETI YENYE MUITIKIO WA GESI

Uandaaji wa bajeti yenye muitikio wa GESI ni zana yenye lengo la kujumuisha masuala ya GESI katika mchakato wa kuandaa bajeti ambayo imegundulika kuwa mojawapo ya mbinu madhubuti za kufikia matokeo ya GESI. Utumiaji wa lenzi ya GESI kwenye bajeti husaidia kuhakikisha kuwa bajeti, mapato na matumizi yanazingatia mahitaji tofauti tofauti ya kila mtu (wanawake na wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na vikundi vingine vya kijamii). Hii ni pamoja na kuchanganua jinsi bajeti itakavyoathiri makundi mbalimbali ya kijamii katika hatua zote za mchakato wa bajeti. Pia inahusisha kubadilisha bajeti ili kuhakikisha kuwa jitihada za usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii zinatekelezwa na kuonekana.[48]

Kushindwa kutenga rasilimali watu na rasilimali fedha kwenye shughuli za GESI zinaweza kupunguza ufanisi na uthabiti wa programu.[49] Ili GESI iweze kuonekana ipasavyo katika maamuzi ya bajeti, ni muhimu kwanza kufanya uchanganuzi wa GESI ili kuelewa mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii.[50] Ikiwa wanawake au makundi mengine yaliyotengwa hayafahamiki, na mahitaji yao hayajapangiwa bajeti pale mwanzoni wakati wa usanifu wa programu, ni ngumu sana baadaye kurudi nyuma na 'kuweka upya' matumizi ya rasilimali na kuongezea bajeti baadaye. Zana hii inakusaidia kupima namna ambayo umetenga rasilimali za kifedha na watu zinazofaa kwa ajili ya kukuza GESI.

48 Oxfam (2018). A Guide to Gender-Responsive Budgeting.
49 Sharp and Elson (2012). Improving Budgets.
50 Oxfam (2018). A Guide to Gender-Responsive Budgeting.

## MALENGO YA BAJETI YENYE MUITIKIO WA GESI

- Husaidia kuhakikisha kuwa mgao wa bajeti ni wa haki, usawa na unajumuisha washiriki wote wa mradi
- Husaidia wafanyakazi katika kukadiria vyema gharama na rasilimali zinazohitajika kushughulikia vipaumbele mbalimbali, mahitaji, vikwazo, na fursa kwa makundi yaliyotengwa na yaliyo katika mazingira hatarishi (kama watoto, wanawake, watu wenye ulemavu)
- Inatenga fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya programu unajumuisha ufanisi na matokeo ya GESI
- Huongeza ubora wa programu na huduma kwa watu walio katika mazingira hatarishi

Zingatia vigezo vifuatavyo unapokuwa unatenga/tayarisha bajeti wakati wa usanifu wa programu ili kuhakikisha mpango wa GESI unaotakiwa utatekelezwa:

- Bajeti imetengwa kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na kuongeza ufanisi wa programu katika kutekeleza programu zenye muitikio wa GESI
- Bajeti imetengwa kwa ajili ya kuongeza ufikiaji na uhusishaji wa watu wenye ulemavu, kutoa msaada na teknolojia saidizi kwa watu wenye ulemavu ili kuboresha uwezo wao wa kushiriki na kufaidika na mradi
- Bajeti imetengwa ili kushughulikia usawa wa kijinsia kulingana na idadi ya wafanyikazi wakike na wakiume

## KUTENGENEZA BAJETI YENYE MUITIKIO WA GESI

Wakati wa mapitio ya andiko la mradi yenye muitikio wa GESI,jibu maswali kwenye Jedwali 24. Katika safu wima ya kulia, weka alama kwa kila kipengele kulingana na mizani ya Likert ya pointi 5. Baada ya maswali yote kujibiwa, jumlisha alama zote ili kupata jumla ya alama. Weka jumla ya alama chini ya jedwali. Kiwango cha juu ni alama 50. Ikiwa alama ni pungufu ya 45, basi kuna haja ya kuipitia tena bajeti ili kuhakikisha kuwa ina muitikio wa GESI.

**Jedwali 26 | Kutengeneza Bajeti yenye Muitikio wa GESI**

| Maswali | ALAMA<br>1=Hakuna 2=Mbaya<br>3=Wastani 4=Nzuri<br>5=Nzuri sana |
|---|---|
| 1. Je, kwenye bajeti kuna kipengele kwa ajili ya kufanya uchanganuzi au tathmini ya GESI? Au je, tayari mojawapo lilifanyika na matokeo yalitumika kuandaa bajeti hii? | |
| 2. Je, shughuli zinazolenga GESI zimetengewa fungu maalumu kwenye bajeti? | |
| 3. Je, uundaji wa nyaraka za kuongeza maarifa ya GESI (kama muhtasari wa mafanikio, nyaraka zilizotafsiriwa, maandishi makubwa kwa wale walio na ulemavu wa kuona, masomo waliyojifunza, muhtasari wa mwongozo bora wa utendaji, na njia mbadala za mawasiliano) zimewekwa kwenye bajeti? | |
| 4. Je, bajeti imetenga fungu bayana kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi kuhusu GESI? | |
| 5. Je, mradi una mpango wa kuajiri mtu kutoka miongoni mwa makundi ya watu waliokandamizwa kijamii (kama vile watu wenye ulemavu) na kwamba rasilimali zimetengwa kwa ajili hiyo? | |
| 6. Je, kuna ahadi yoyote katika andiko na muundo wa programu inayosisitiza kwamba hairuhusiwi kwa wafanyakazi wa jinsi ya kiume au ya kike kuzidi 60% ya wafanyakazi wote? | |

| Maswali | ALAMA<br>1=Hakuna 2=Mbaya<br>3=Wastani 4=Nzuri<br>5=Nzuri sana |
|---|---|
| 7. Je, kuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mtaalamu wa GESI atakayetoa msaada wa kitaalamu kwa ajili ya mradi (mfano nafasi ya mtaalamu wa GESI, mtaalamu wa muda mfupi kuhusu GESI, au % ya muda wa mshauri kutoka ofisi inayotoa misaada/ofisi kuu nchini /Kanda) | |
| 8. Je, kuna rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya mfuko wa uhusishaji ili kukidhi gharama za ziada za programu pale inapobidi mshiriki alipiwe gharama za kuangalia mtoto, usafiri, gharama za msaidizi, mkalimani wa lugha za ishara au gharama nyinginezo za lazima katika kuwezesha ushiriki wake? | |
| 9. Je, kuna shughuli zinazoshughulikia mahitaji maalum ya vikundi vya watu - kama vile mafundisho ya kusoma na kuandika, utoaji wa vifaa vya usaidizi, n.k. ambazo zimewekewa bajeti | |
| 10. Je, bajeti inajumuisha shughuli za kudhibiti athari za GESI na matokeo yasiyokusudiwa kwa washiriki wa mradi au wafanyikazi? | |
| **JUMLA YA ALAMA KATI YA 50** | |

## UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE MPANGO WA USIMAMIZI WA WAFANYAKAZI/TIMU

Wakati wa kuunda programu yenye muitikio wa GESI, ni muhimu kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa programu hiyo wamewekewa bajeti, wameajiriwa/wamepewa majukumu na wana sifa za kuweza kutekeleza mpango unaotakiwa kwa kutumia lenzi ya GESI. Viongozi wa programu wanapaswa kukagua matokeo na shughuli za programu na kuchagua wafanyakazi wanaofaa.

Zingatia mambo yafuatayo wakati unaunda timu ya wafanyakazi wa programu:

- Wafanyakazi wana uzoefu wa kufanya kazi na makundi maalum yanayokandamizwa na wanaelewa mahitaji na changamoto zao za kipekee
- Wafanyakazi wana uwezo na ari ya kusanifu miradi inayohusisha jamii (yenye mwitikio wa GESI). Ikiwa sivyo, hakikisha kuna mpango wa kuwajengea wafanyakazi uwezo
- Wafanyakazi katika ngazi zote ni pamoja na wanawake na wanaume, hasa wale walio kwenye maeneo ya mradi na wafanyakazi wabia
- Wafanyakazi ni wawakilishi wa vikundi lengwa vya programu, kadri iwezekanavyo,na hii inaweza kuchangia kukuza uhusiano wa World Vision na jamii husika
- Wafanyakazi wameshawahi kushiriki angalau katika mafunzo ya GESI ya World Vision, au kuhudumu kama wawakilishi wa GESI
- Wafanyakazi wanaweza kuwasiliana na vikundi lengwa vya programu kwa lugha yao na pia kupitia njia mbadala za mawasiliano (kama lugha ya ishara, nukta nundu)


World Vision
CardinalHealth

# Sehemu 4

# Ujumuishaji wa GESI kwenye Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu

Sehemu hii inatoa mwongozo wa jinsi ya kujumuisha GESI katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mradi. Sehemu hii ina zana tatu:

| | |
|---|---|
| **ZANA 4.1** | Ujumuishaji wa GESI kwenye Ufuatiliaji wa Programu |
| **ZANA 4.2** | Tathmini ya Programu yenye Muitikio wa GESI |
| **ZANA 4.3** | Kuchanganua na Kuripoti Data kwa Muitikio wa GESI |

Ujumuishaji wa GESI kwenye utekelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya mradi ni muhimu ili kuelewa kama shughuli za mradi zilizopangwa zinafikia malengo ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii kwa kushughulikia mahitaji na vipaumbele vya wanawake,wanaume,wasichana,watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.[51] Pia inasaidia kutathmini mchango wa programu kwa makundi mbalimbali ya kijamii na kuangalia mapungufu kulingana na vipengele vya GESI ambavyo vinatakiwa kujumuishwa kwenye mifumo ya tathmini. Ufuatiliaji na tathmini ulio thabiti na wenye muitikio wa GESI unapaswa kutumia data za kitaamuli na kitakwimu zilizogawanywa kwa jinsi, umri, hali ya ulemavu na sifa zingine za kijamii ili kupima mchango wa programu kwa makundi mbalimbali. World Vision ina mbinu kadhaa za kitaalamu zinazowezesha ufanisi wa programu zenye muitikio wa GESI. Mbinu hizi zimeainishwa katika Mkabala wa GESI na Nadharia ya Mabadiliko.

## MALENGO YA UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE UFUATILIAJI NA

- Kuwasaidia wafanyakazi wa shirika la World Vision kujumuisha GESI kwenye michakato ya ufuatiliaji na tathmini
- Kuhakikisha kuwa programu imeshughulikia mahitaji mbalimbali ya wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi
- Kuhakikisha kuwa programu ina matokeo chanya katika kuimarisha upataji na ufikiaji, ufanyaji maamuzi, ustawi na mifumo kwa ajili ya watu walio kwenye mazingira hatarishi
- Kuboresha utekelezaji na ufanisi wa programu. Pia inaruhusu uhusishaji katika kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyobainika kwenye baada ya tathmini ya awamu ya kati[52]
- Kuboresha ujifunzaji kwa ajili ya ufanisi na mabadiliko ya miradi ya GESI inayofuata[53]

51 FAO (2014). Gender-Sensitive Monitoring and Evaluation for FNS.
52 The World Bank (2001). Integrating a Gender Dimension into Monitoring & Evaluation.
53 The World Bank (2001). Integrating a Gender Dimension into Monitoring & Evaluation.

# ZANA 4.1 UJUMUISHAJI WA GESI KWENYE UFUATILIAJI WA PROGRAMU

Ujumuishaji bora wa GESI katika ufuatiliaji wa programu ni shughuli endelevu ya kutathmini michakato na shughuli za utekelezaji wa programu na jinsi mipango hiyo inavyowasaidia wanawake, wanaume, wasichana, wavulana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Ufuatiliaji pia hujumuisha ufanyaji maboresho yenye tija katika utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha kuwa data iliyokusanywa, iliyochanganuliwa, na kuwasilishwa, inatumiwa kuonyesha maendeleo yanayolenga kufikia malengo ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Ufuatiliaji pia hutoa taarifa juu ya maendeleo kuelekea kwenye usawa wa kijinsia na malengo ya ujumuishi wa kijamii (ufuatiliaji wa utendaji). Hii inafanywa kupitia ukusanyaji wa kawaida na maalumu wa data, uchanganuzi, na uwekaji kumbukumbu, na kuripoti.

## MALENGO YA UFUATILIAJI WA PROGRAMU NI:[54]

- Kutathmini na kufuatilia maendeleo ya shughuli za utekelezaji wa programu zilizopangwa
- Kujifunza kuhusu mafanikio muhimu na kipi kimefanikiwa na kipi kinatakiwa kuboreshwa, na kipi hakikufanikiwa ili kufanya maamuzi ya kiutawala
- Kubainisha mienendo na ruwaza za mradi na kuhakikisha kuwa shughuli za mradi zimewekwa kwenye ratiba
- Kubainisha mahitaji,changamoto na matatizo na kuchukua hatua sahihi za kurekebisha
- Kuhakikisha uwajibikaji wa utendaji na rasilimali za mradi kwa wafadhili na washirika
- Kutoa msingi wa tathmini na ujifunzaji

## MWONGOZO WA HATUA KWA HATUA

### Fanya uchanganuzi wa GESI

Fanya uchanganuzi wa GESI kukusanya taarifa za awali. Taarifa za awali zinapaswa kukusanywa mwanzoni mwa programu na zinapaswa ziwe na data za GESI zilizogawanywa. Uchanganuzi wa GESI hutoa taarifa zinazohusu masuala maalumu ya GESI, changamoto, athari na namna ambavyo mradi unaweza kusaidia kuendeleza GESI. Hii itatoa mwelekeo wa kutathmini matokeo na mchango wa programu. Pia itasaidia kuamua kama mabadiliko yanapatikana au hapana na kiwango cha mchango wa programu katika kufikia malengo ya GESI.

### Tumia Viashiria vyenye Muitikio wa GESI

Viashiria vinapaswa kupima vikoa vyote vya GESI vya upataji na ufikiaji,ushiriki,ufanyaji maamuzi,ustawi na mifumo. Viashiria vyenye muitikio wa GESI vitakusaidia kuamua kama kuna maendeleo kuelekea usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii au hapana.

### Tengeneza Mpango wa Ufuatiliaji wa GESI

Mpango wa ufuatiliaji unapaswa kubainisha yafuatayo:[55]

- Angalau mtu mmoja katika timu ya ufuatiliaji anapaswa kuwa na ujuzi na umahiri wa kutosha wa GESI
- Iwapo wabia wa mradi wamepewa mafunzo au kuhamasishwa kuhusu masuala ya GESI
- Mbinu za kukusanya data (kama tafiti, data ya pili, majadiliano ya vikundi lengwa, n.k.)
- Jinsi data itakavyochanganuliwa
- Ni mara ngapi data mbalimbali zitakusanywa ili kufuatilia viashiria
- Mahali ambapo ufuatiliaji utafanyika
- Jinsi data itakavyoripotiwa na kuwasilishwa

54 WHO (2006). Communicable Disease Surveillance and Response Systems; UNICEF (2003). Programme Policy and Procedures.
55 GIZ (2014). Guidelines on Designing a Gender Sensitive Results-Based Monitoring System.

### Ziara za Ufuatiliaji

Ziara za ufuatiliaji ni muhimu katika kuhakikisha kuwa shughuli za mradi zinatekelezwa kama zilivyoelezwa kwenye mpango wa mradi. Ziara hizi kwa kawaida huhusisha kukutana na timu ya wasimamizi wa mradi na/au washiriki wa programu.[56] Ziara za maeneo ya mradi zinaweza kutoa taarifa ambazo zinaweza zisiwe kwenye ripoti za mradi, au mikutano ya simu na mtandao. Uchunguzi wa ana kwa ana wakati wa ziara za maeneo ya mradi unatoa uelewa mzuri kuhusu eneo la mradi, shughuli, taratibu, matokeo, na ushiriki.[57] Ufuatiliaji unapaswa kuwa jumuishi na shirikishi ili kuhakikisha mahitaji ya makundi yaliyo katika mazingira hatarishi yanafahamika na kushughulikiwa. Wakati wa ziara ya ufuatiliaji, kusanya taarifa za GESI zinazojumuisha: maendeleo kuelekea malengo na madhumunin ya mabadiliko ya GESI; kama bajeti na rasilimali zinazingatia GESI; changamoto na fursa za kuboresha; na msaada wowote unaohitajika.

### Ukusanyaji wa Data

Masuala ya GESI yanahusiana sana na maadili ya kitamaduni, mitazamo ya kijamii na maoni. Kwa hiyo, inashauriwa kutumia viashiria vyenye muitikio wa GESI ambavyo vinaweza kukusanya taarifa zote za kitakwimu na kitaamuli zinazohusiana na vikoa vya GESI. Data lazima zigawanywe kwa jinsi, umri, hali ya ulemavu, na sifa zingine za kijamii. Timu zinazohusika na ukusanyaji wa data zinapaswa kuwa na uwakilishi katika jinsi, kabila au dini. Pia, zinatakiwa kuwa na ujuzi kamili wa lugha inayotumika.[58] Hii itasaidia kupunguza upendeleo na athari za mitazamo ya kitamaduni inayohusiana na GESI.[59]

### Fanya Uchanganuzi wa Data

Hakikisha kuwa timu inayohusika na uchanganuzi wa data ina umahiri wa GESI. Uchanganuzi wa data unapaswa kuzingatia hali ya sasa ya viashiria na kusisitiza matokeo ya GESI Pamoja na kufuatilia matokeo ya GESI na athari zake.[60] Kubainisha jinsi mpango huu unavyoathiri wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Pia kubainisha maendeleo juu ya mafanikio ya matokeo ya GESI.

### Andaa Ripoti za Maendeleo ya Kiutendaji

Baada ya uchanganuzi wa data, andaa ripoti ya maendeleo. Ripoti hizo zinaweza kuwasilishwa kwa wabia wa programu. Katika ripoti hizo, hakikisha umegawanya taarifa kwa kigezo cha jinsi, umri, hali ya ulemavu au sifa zingine za kijamii. Jadili ripoti za maendeleo ya kiutendaji na wafanyakazi wanosimami utekelezaji wa shughuli, washiriki, na wadau wengine na utafute maoni yao juu ya jinsi ya kuboresha utekelezaji wa programu.

Ripoti za maendeleo ya kiutendaji zinapaswa kuwa na taarifa zifuatazo:[61]

- Jinsi mradi unavyoathiri wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi
- Matokeo yoyote ya programu yasiyokusudiwa
- Jinsi programu inavyoonyesha maendeleo katika kuendeleza GESI na kubadilisha maisha
- Mapendekezo kuhusu jitihada zinazohitajika kuimarisha utekelezaji wa programu na kuhakikisha malengo ya GESI yanafikiwa

### Fanya Marekebisho Yanayohitajika

Amua kama kuna marekebisho yoyote ambayo unatakiwa kuyafanya ili kufikia malengo ya programu hususani shughuli au michakato ambayo gharama zake si nafuu, hazina ufanisi, hazifanyi kazi, haiendelezi GESI, haichangii kufikia kwenye malengo ya programu na inasababisha madhara ambayo hayakukusudiwa kwa washiriki. Imarisha michakato na shughuli ambazo zinasababisha maendeleo yaende taratibu.[62]

56 WFP(Undated). Gender and Monitoring.
57 UNICEF (1990). Guide for Monitoring and Evaluation.
58 USAID (2014a). Toolkit for Monitoring and Evaluating Gender-Based Violence Interventions.
59 Brambilla (2001). Gender and Monitoring: A Review of Practical Experiences.
60 The World Bank (2005). Gender Issues in Monitoring and Evaluation.
61 WFP(Undated). Gender and Monitoring.
62 WFP(Undated). Gender and Monitoring.

## ZANA 4.2 TATHMINI YA PROGRAMU YENYE MUITIKIO WA GESI

Tathmini zenye muitikio wa GESI ni muhimu katika kuimarisha usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa kijamii katika programu zetu. Tathmini hupima umuhimu, ufanisi, matokeo na uendelevu (uliokusudiwa na usiokusudiwa) wa mradi kwa wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.[63] Tathmini hujumuisha vikoa vya GESI katika mikabala, mbinu na michakato. Tathmini ya programu inaweza kufanywa kabla au mwanzoni, katikati na mwishoni mwa programu au muda mrefu baada ya programu kwisha.[64]

### MALENGO[65]

- Kupima athari za programu yote zilizokusudiwa na ambazo hazikukusudiwa kwa wanawake,wanaume,watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo kwenye mazingira hatarishi
- Kubainisha vipengele vya programu ambavyo vimefanikiwa katika kushughulikia masuala ya usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii. Tathmini ya programu ya GESI hutumia data ili kuangalia maendeleo na mchango wa programu kwenye utekelezaji kwa makundi mbalimbali ya kijamii
- Kubainisha mapungufu na mienendo iliyofanikiwa kwenye usanifu,utekelezaji wa programu na kuweka rasilimali. Taarifa hii ni ya muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi baadaye ambayo yataboresha matokeo chanya ya GESI
- Kutoa taarifa na maarifa mapya ya kile kilichofanikiwa, ambacho hakijafanikiwa na namna ya kushughulikia changamoto mbalimbali katika kutekeleza programu za GESI
- Kuhakikisha uwajibikaji wa wadau kuhusiana na michakato na mchango wa programu?

### TATHMINI YA PROGRAMU HUULIZA MASWALI YAFUATAYO[66]

- Je, programu ilitumia shughuli sahihi kwa wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi? Je, shughuli zilifanywa ipasavyo?
- Je, programu hii inafanya kazi? Imeleta mabadiliko?
- Je, athari za shughuli za programu kwa wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo kwenye mazingira hatarishi ni zipi?
- Je, nini sababu kubwa ya matokeo yaliyoonekana? Je, matokeo unayoona yamesababishwa na programu?
- Je, kuna kitu kingine nje ya programu kilichochangia mabadiliko yaliyojitokeza?
- Je, programu inastahili gharama hii?

### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Hakikisha uchanganuzi wa GESI umeonyeshwa katika mawanda yote ya kazi (*Scope of Work*) au hadidu za rejea (*Terms of Reference*) kwa ajili ya mikataba ya tathmini ya programu [67]
- Tumia viashiria vyote vya kitaamuli na kitakwimu vyenye muitikio wa GESI.Tumia viashiria hivi katika tafiti zako za awali na uzifuatilie tangu mwanzoni mwa mzunguko wa programu [68]
- Timu ya tathmini inahitaji kuwa na angalau mtaalamu mmoja wa GESI. Mtu huyo anapaswa kuwa na uzoefu katika kusanifu au kuongoza tathmini au programu zenye muitikio wa GESI, na katika kufanya uchanganuzi wa GESI Mtu huyo anapaswa pia kuonyesha uelewa wa masuala ya GESI.[69] Kwa kuongezea, washiriki wote wa timu ya tathmini wanatakiwa kuwa na maarifa madhubuti ya utamaduni na desturi za

63 The World Bank (2001). Integrating a Gender Dimension into Monitoring & Evaluation.
64 Fehringer, et.al. (2017). Monitoring and Evaluation of Health Programs. UN Women (2015). How to Manage Gender-responsive Evaluation.
65 UN Women (2015). How to Manage Gender-responsive Evaluation.
66 Fehringer, et.al. (2017). Monitoring and Evaluation of Health Programs.
67 Save the Children (2014). Engendering Transformational Change.
68 Save the Children (2014). Engendering Transformational Change.
69 USAID (2014b). Gender-Sensitive Evaluation.

kijamii, mazoea ya kitamaduni na mitazamo, na masuala muhimu ya GESI kwenye eneo husika.

- Hali kadhalika, timu ya tathmini inapaswa kujumuisha wanawake na wanaume ambao wana utaalamu na uzoefu katika mbinu zote za utafiti yaani wa kitaamuli na kitakwimu na angalau mtu mmoja aliye na ujuzi au uzoefu wa sekta husika.[70] Kwa mfano, ikiwa unafanya tathmini katika sekta ya maji, usafi wa kimwili na usafi wa kimazingira (WASH), unahitaji angalau mtu mmoja katika timu ya tathmini ambaye ana utaalamu wa WASH.
- Kusanya na changanua data za GESI ili kubaini mapungufu yoyote kwa wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira ya hatarishi katika upataji na ufikiaji, ushiriki, ufanyaji maamuzi, mifumo, na ustawi. Angalia sababu kuu za mapungufu haya, ikiwa yapo. Pia, bainisha athari chanya na hasi za programu kwenye makundi tofauti tofauti ya kijamii.
- Chukua hatua za kurekebisha ili mapungufu haya na kushughulikia athari hasi na ambazo hazikukusudiwa za shughuli za programu.

Jedwali hapa chini ni muhtasari wa mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandaa hadidu za rejea na kusanifu tathmini.

**Jedwali 27 | Uandaaji wa Hadidu za Rejea na Kusanifu Tathmini**

| **Hadidu za Rejea** |
|---|
| 1. Je hadidu za rejea zinahitaji usawa wa kijinsia na ushirikishaji wa kijamii kwenye wasaidizi wa watafiti na wahojiwa? |
| 2. Je, maswali yanayohusiana na jinsia na uhusishaji wa kijamii yameingizwa kwenye hadidu za rejea? |
| 3. Je, imebainishwa kuwa sampuli za tathmini ni lazima zihusishe uwakilishi sawa wa wanawake, wanaume na makundi mengine ya watu waliokandamizwa? |
| 4. Je, inafahamika ni mbinu gani za kitakwimu na kitaaluma zinatakiwa zitumike, na je, mbinu husishi zimehitajika pia? |
| 5. Je, inafahamika kwamba uwezeshaji wa wanawake na makundi mengine yanayokandamizwa unapaswa kupimwa? |
| 6. Je, umeeleza kwa uwazi na kina kuhusu ukusanyaji wa data juu ya mahusiano ya kijinsia na utofauti wa matokeo ya mradi kwa wanaume na wanawake? |
| 7. Je, umeeleza kwa uwazi na kina kuhusu ukusanyaji wa data za makundi yanayokandamizwa kwenye mradi na utofauti wa matokeo ya mradi kwa makundi hayo yanayokandamizwa? |
| 8. Je, uliweka maswali yanayohusu jinsia na uhusishaji wa kijamii ambao unaendana na dhumuni la mradi la Nadharia ya Mabadiliko? |
| 9. Je, jinsia na uhusishaji wa kijamii unapaswa kuzingatiwa kwenye kila swali la tathmini za kitaalamu na siyo tu kwenye 'kipengele cha jinsia' |
| **Usanifu wa Tathmini** |
| 10. Je,timu ya tathmini imehusisha asilimia 50 ya wanawake? |
| 11. Je, kigeu cha uchanganuzi ni mtu mmojammoja au kaya? Je, kaya inafasiliwaje na ni nani anaweza au anapaswa kuzungumza kwa niaba ya kaya? |
| 12. Je, tathmini inajumuisha kufanya mapitio ya bajeti na kufuatilia matumizi ya fedha ili kubaini uchepukaji wowote wa matumizi? |
| 13. Je, tathmini itaonyesha namna mradi ulivyotengeneza ubunifu wa GESI? |
| 14. Je, tathmini itaandika jinsi mradi ulivyoshirikisha mbinu zenye mafanikio na ubadilishanaji wa maarifa kuhusu GESI. |
| 15. Je, kuna maswali yamewekwa ili kupima mahusiano ya kijinsia na kijamii kwenye ngazi ya kaya, jamii na mtu mmoja mmoja? |
| 16. Je, mbinu zinazopendekezwa zitaruhusu ukusanyaji wa data zilizotenganishwa kuhusu jinsi,umri, na ulemavu kwa ajili ya viashiria vinavyohusika? |

70 USAID (2014b). Gender-Sensitive Evaluation.

| |
|---|
| 17. Je, kuna mpango wowote wa kupima matokeo ya muda mrefu na mchango wa afua za GESI? |
| 18. Je, muhtasari mkuu unajumuisha matokeo yanayohusiana na jinsia na ujumuishaji wa kijamii (mafanikio na/au kushindwa)? |
| 19. Je, mradi ulishindwa kuwa na uhusishi kutokana na ushawishi wa desturi za kijinsia na kijamii? Kama ndiyo, je, ulihakikisha kwamba mtafiti anajua kwamba mafunzo haya yanapaswa kuandikwa na kupendekezwa kwa miradi ya siku zijazo ili kushughulikia uhusishi kupitia programu? |
| 20. Je, muundo wa mkakati wa kuchagua sampuli umegawanywa kwa jinsia au aina ya kaya? Tafadhali kumbuka kwa kawaida matokeo huwa yanaegemea zaidia kwenye mtazamo wa wanaume ikiwa ni mkuu wa kaya pekee atahojiwa. |

## KUANDAA RIPOTI YA GESI YA TATHMINI YA PROGRAMU

Ni muhimu kutumia uchanganuzi yakinifu wa GESI wakati wa kuandaa ripoti ya tathmini. Usizingatie tu viashiria vya maingizo na matokeo. Upimaji mzuri wa matokeo madogo unapaswa kuendelea hadi kwenye matokeo makubwa na kuzingatia muktadha zaidi ya mradi ili kuelewa vema mienendo ya GESI na mabadiliko ya hali ya kijamii ya wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na vikundi vingine vilivyo kwenye mazingira hatarishi. Miradi ambayo hupima viashiria vya pato tu itashindwa kutoa tarifa za jinsia na mabadiliko mengine ya desturi za kijamii, na upataji na ufikiaji, ushiriki, ufanyaji maamuzi, mifumo, na ustawi ulio bora, na hii husababisha ukosefu wa taarifa juu ya kipi kinaleta ufanisi au kipi hakileti.

**Jedwali 28 | Uandaaji wa Ripoti za Tathmini za Programu wenye Mwitikio wa GESI**

| Orodha ya Uandaaji wa Ripoti za Tathmini ya Programu wenye Muitikio wa GESI |
|---|
| 1. Vikwazo kwa ajili ya ushiriki vinapaswa kuandikwa kama wanawake, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi hayakuwakilishwa vema. |
| 2. Ripoti inapaswa kujadili kama mradi ulibadilika,ulipunguza au uliondoa unyanyapaa, chuki, na desturi zinazowatenga wanawake, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. |
| 3. Ripoti inapaswa kujadili kama mradi uliboresha upataji na ufikiaji wa rasilimali, fursa, na huduma kwa wanawake na makundi mengine yaliyotengwa. |
| 4. Ripoti inapaswa kujadili kama mradi uliwawezesha wanawake na makundi mengine ya kijamii yaliyotengwa kutoa maoni yao wakati wa mikutano na matukio ya mradi. |
| 5. Ripoti inapaswa kujadili kama mradi uliwawezesha wanawake na makundi mengine ya kijamii yaliyotengwa kushiriki kwenye mradi. |
| 6. Je, wanawake na makundi mengine ya kijamii yaliyotengwa yalionekana kwenye nafasi za uongozi wa jamii? |
| 7. Je, ripoti inajadili vipimo vya ukosefu wa uhusishaji ambavyo havikushughulikiwa kwenye mradi lakini vilisababisha vikwazo vya uhusishaji? |
| 8. Lugha maalumu inapaswa kutumika. Kwa mfano kufasili na kuelezea 'wakulima wadogo ni wakina nani' na hakikisha wakati wote tathmini inaonyesha 'wakulima' au 'washiriki' kuwa ni wote wanaume na wanawake. |
| 9. Panapaswa kuwa na kipengele maalumu cha masuala ya GESI. Hata hivyo masuala hayo yanapaswa kuhusishwa na kuoanishwa kwenye ripoti nzima-na siyo kujadiliwa tu kwenye kipengele cha GESI peke yake. Ripoti inatakiwa kuonyesha kuwa GESI imetumika kama lenzi ya kufanyia tathmini na sio kutaja tu na kutenga kipengele kizima cha GESI halafu baadae kukipuuzia. |
| 10. Masuala yanayohusiana na jinsia na uhusishaji wa kijamii yanapaswa kuchukuliwa na kuandikwa kwenye 'sehemu ya mapendekezo' ili kuhakikisha kuwa ujifunzaji unaendelea. |

| Orodha ya Uandaaji wa Ripoti za Tathmini ya Programu wenye Muitikio wa GESI |
|---|
| 11. Mawazo ya makundi ya wanawake waliokandamizwa yanapaswa kuwekwa kwenye kauli ya uwakilishi. Visa vya 'masimulizi' havipaswi tu kulenga kwenye viashiria ambavyo mradi ulikuwa unaviangalia, lakini pia vinapaswa kushughulikia muktadha. |
| 12. Ripoti ya tathmini inapaswa kuhusisha taarifa za kiprogramu na kubainisha mbinu zilizofanikiwa kuleta mabadiliko yanayohusiana na GESI, na inahusisha data na afua za programu. |
| 13. Matokeo ya tathmini yanapaswa kuzungumzia ufanisi wa programu kwa washiriki wanawake na makundi yaliyotengwa, na si uwajibikaji kwa wafadhili tu kuhusu ufanisi wa malengo. |

## ZANA 4.3 KUCHANGANUA NA KURIPOTI DATA KWA MUITIKIO WA GESI

Data zenye muitikio wa GESI zinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia mkabala wa mbinu changamani ambayo huhusisha mbinu zote za uchanganuzi  yaani za kitakwimu na kitaamuli. Uchanganuzi wa kitakwimu huruhusu kulinganisha data za nambari ziliyogawanywa kufuatana na jinsi, hali ya ulemavu na sifa nyingine za kijamii kama kabila, umri, tabaka au kundi. Ulinganishaji huonyesha mapungufu na fursa. Ulinganishi huu unasaidia kuonyesha mapungufu na ukosefu wa usawa na kuhimiza uchanganuzi wa kitaamuli (usio wa nambari) ili kubainisha kwa nini mapungufu haya na ukosefu wa usawa upo. Ni muhimu kwamba data ichanganuliwe mara kwa mara na katika hatua zote wakati wa mchakato wa usanifu, ufuatiliaji, na tathmini ili:

- Kubainisha vikwazo na fursa ambazo hukwamisha au kuwezesha ufanisi wa malengo ya GESI[71]
- Kutathmini mabadiliko ya desturi za kijinsia na kijamii, wajibu na majukumu
- Kutathmini kama mahitaji halisi, maslahi ya mkakati na vipaumbele vya makundi mbalimbali ya jamii yameshughulikiwa
- Kupima na kutathmini athari mbalimbali za programu kwa makundi mbalimbali ya kijamii
- Kutoa taarifa zitakazo saidia kufanikisha mabadiliko katika utekelezaji wa programu ili kuboresha matokeo kwa makundi ya kijamii

### MAPENDEKEZO YA MANDALIZI KWA AJILI YA UCHANGANUZI WA DATA WENYE MUITIKIO WA GESI

- Weka pamoja data zote zilizokusanywa, hii ni pamoja na madokezo na tafakari za mwezeshaji, matokeo ya utafiti, rekodi za mahojiano,vitini au picha
- Bainisha data ya kipaumbele ambayo imegawanywa kwa jinsi, hali ya ulemavu, umri na sifa zingine za kijamii kwa uchanganuzi
- Iwapo data yoyote inakosekana au inahitaji ufafanuzi, wasiliana na wenzako wa ufuatiliaji na tathmini, wakusanyaji wa data au wanaojaza hojaji
- Hakikisha kuwa una programu ya takwimu (SPSS, STATA, R), programu ya manukuu, au programu ya uchanganuzi wa kitaamuli (NVivo, ATLAS.ti)

71 JHPIEGO (2019). Gender Analysis Toolkit for Health Systems.

## UCHANGANUZI WA GESI WA DATA ZA KITAKWIMU

Uchanganuzi wa kitakwimu wenye muitikio wa GESI unahusika na uchanganuzi wa data za namba zenye mgawanyiko wa GESI (data zinazoweza kuhesabika) kama vile umri,ukubwa wa familia na kipato.Husaidia kujibu swali la "nini." Kwa mfano, Je, ni nini wastani wa wanawake,wanaume na watu wenye ulemavu ambao wanaweza kupata maji salama ya kunywa? Je, ni nini asilimia ya wanawake, wanaume,wavulana na wasichana wanaojisikia kuwa wamewezeshwa? Kielelezo 7 kinawasilisha hatua muhimu kwa ajili ya uchanganuzi wa data za kitakwimu.

**Kielelezo 7 | Hatua za Uchanganuzi wa GESI kwenye Data za Kitakwimu**




### Mwongozo wa Hatua kwa Hatua

#### Kusafisha Data

Kusafisha data kunabaini, sahihisha na kuondoa makosa na kukosekana kwa ushikamani wa data ambako kunaweza kusababishwa na ukusanyaji na uingizaji mbovu wa data. Programu nyingi za kitakwimu zina mfumo wa kuthibitisha ambao umeundwa kusaidia kuondoa au kusahihisha data ambazo zingeweza kusababisha hitimisho lisilosahihi.

## Uchanganuzi Fafanuzi wa GESI

Huonyesha tofauti za data kati ya vikundi mbalimbali vilivyogawanywa: jinsi, hali ya ulemavu, umri na sifa zingine za kijamii. Kwa mfano, kama unataka kujua namna ambayo jinsia na hali ya ulemavu inavyoathiri kuridhika na na ubora wa vyanzo vya maji ya kunywa, utatenganisha data ulizonazo na kuziweka kwenye jedwali kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**Jedwali 29 | Mfano wa Jedwali la Mzunguko la GESI**

Asilimia ya watu wanaojisikia wanaridhika na ubora wa chanzo cha maji ya kunywa kwa jinsi na hali ya ulemavu.

| Jinsi na Hali ya Ulemavu | Junla ya Idadi | Idadi ya Walioridhika | Asilimia ya Walioridhika | Idadi ya ambao Hawajaridhika | Asilimia ya ambao Hawajaridhika |
|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake wasio na ulemavu | 625 | 226 | 36.2% | 399 | 63.8% |
| Wanawake wenye ulemavu | 112 | 7 | 6.2% | 105 | 93.8% |
| Wanaume wasio na ulemavu | 859 | 343 | 39.9% | 516 | 60.1% |
| Wanaume wenye ulemavu | 130 | 10 | 7.7% | 120 | 92.3% |

Data hii inaweza kuonyeshwa kwa kutumia miundo mingine ikiwemo mhimili wa wima hapo chini. Pia waweza kutumia chati ya pai. Kisha unatakiwa kuyaelezea matokeo yako.

**Kielelezo 8 | Mfano wa Grafu ya Mhimili wa GESI**

Asilimia ya watu wanaoridhika na kiwango cha ubora wa chanzo cha maji kwa kigezo cha jinsi na ulemavu.




Baada ya kuwasilisha matokeo yako kwa kutumia majedwali ya masafa, mihimili au chati, unatakiwa kuandika maelezo ili kufafanua matokeo yako.

**Jedwali 30 | Mfano wa Kuelezea Matokeo yenye Kuonyesha GESI**

| Matokeo | Tafsiri |
|---|---|
| Matokeo yanaonyesha kuwa watu wengi hawakuridhika na ubora wa vyanzo vya maji, ila wanaume na wanawake wenye ulemavu hawakuridhika zaidi na ubora wa vyanzo vya maji ukilinganisha na wale wasio na ulemavu (wastani wa 93% ukilinganisha na wastani wa 62%).<br><br>Palikuwa na tofauti ndogo katika viwango vya kuridhika kati ya wanaume na wanawake (chini ya 4%). | Hii inamaanisha kuwa juhudi zinapaswa kufanywa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanalengwa ili kuboresha upataji na ufikiaji wao na kuridhika na ubora wa vyanzo vya maji.<br><br>Kumbuka: Basi utahitaji kutumia taarifa ya kitaamuli ili iwe kuelewa kwanini hali iko hivyo. |

Data zilizogawanywa zinapaswa kuchanganuliwa kwa kila robo ya mwaka kwa kutumia uchanganuzi wa data zilizokusanywa kwa mfululizo wa muda (*Time Series Analysis*) au uchanganuzi wa mwenendo ili kuelewa matokeo ya mradi kwenye makundi mbalimbali. Katika hali hii, utahitaji kuona kama kiwango cha kuridhika kwa watu wenye ulemavu kimekuwa bora zaidi baada ya kufanya tathmini ya kitaamuli ili kuelewa kwa nini hawaridhiki na kisha kuchukua hatua za kushughulikia sababu hizo.

**Jedwali 31 | Mfano wa Jedwali la GESI Linaloonyesha Mzunguko wa Data Zilizokusanywa kwa Mfululizo wa Muda**

Wastani wa asilimia ya watu ambao hawaridhiki na ubora wa chanzo cha maji ya kunywa.

| Jinsia na Hali ya Ulemavu | Wastani wa Watu ambao Hawajaridhika | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Robo 1 | Robo 2 | Robo 3 | Robo 4 |
| Wanawake wasio na ulemavu | 63.8 | 60 | 55 | 46 |
| Wanawake wenye ulemavu | 93.8 | 80 | 54 | 42 |
| Wanaume wasio na ulemavu | 60.1 | 58 | 40 | 22 |
| Wanaume wenye ulemavu | 92.3 | 78 | 52 | 43 |

Data hii inakufanya uhitimishe kuwa jitihada zako zimekuwa na mafanikio kwenye kuongeza kuridhika kwa wanaume na wanawake wenye ulemavu. Hata hivyo,wanawake wasio na ulemavu hawakuridhika zaidi kuliko wanaume wasio na uleamavu. Utatumia taarifa za kitaamuli ili kupata sababu kwa nini hili limetokea.

## Uchanganuzi wa GESI wa sampuli ya data ili kufanya mahitimisho kuhusu kundi kubwa la watu

Uchanganuzi wa GESi wa sampuli ya data ili kufanya mahitimisho kuhusu kundi kubwa la watu huchunguza uhusiano kati ya sifa fulani za kikundi kidogo cha watu (kama vile jumuiya chache tofauti) ili kufanya hitimisho kuhusu idadi kubwa zaidi ya watu. Kuna aina nyingi za uchanganuzi wa sampuli ya data ili kufanya mahitimisho kuhusu kundi kubwa la watu ambazo unaweza kutumia kuzielewa data zako. Kijitabu hiki kinatoa mifano miwili: uchanganuzi wa uwiano na jaribio la tofauti muhimu kitakwimu au jaribio la T (T-test).

### Uchanganuzi wa Uwiano

Uchanganuzi wa uwiano unachunguza kama vigeu viwili vinahusiana au vimeoana. Kwa mfano, unaweza kutaka kujua ikiwa uwezo wa mtu binafsi kufanya maamuzi kuhusu ushiriki wa shughuli za kujipatia kipato inahusiana na jinsi na ulemavu ( angalia Jedwali 16). Uchanganuzi wa uhusiano unaweza pia kubaini nguvu ya uhusiano (hakuna uhusiano, uhusiano wenye nguvu au dhaifu) na ikiwa uhusiano huo ni chanya au hasi. Kujua ni vigeu vipi vinahusiana na kwa namna gani vinahusiana husaidia sana katika kuelewa jinsi shughuli za mradi zinavyoweza kuathiri makundi mbalimbali ya kijamii kwa namna chanya au hasi. Uwiano unachanganuliwa kwa kutumia programu za kitakwimu kama vile STATA au SPSS. Kadri mgawanyo wa uwiano unakuwa karibu na namba moja ndio kadri nguvu ya uhusiano hunaongezeka (0.5 au zaidi, iwe chanya au hasi). Ikiwa mgawanyo wa uwiano ni 0, inamaanisha hakuna uwiano, + 1 inamaanisha uwiano kamili chanya, -1 inamaanisha uwiano kamili hasi.

Kwa mfano, ikiwa umechanganua uwiano kati ya uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu ushiriki wa shughuli za kujipatia kipato na hali ya ulemavu, na uwiano ni -0.8, basi utaripoti kuwa kuna uhusiano hasi kati ya uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu ushiriki wa shughuli binafsi za kujipatia kipato na hali ya ulemavu. Hii inamaanisha kuwa watu wenye ulemavu hawana maamuzi kuhusu ushiriki wao katika shughuli binafsi za kujipatia kipato ikilinganishwa na watu wasio na ulemavu. Unaweza kutumia data za kitaamuli zilizokusanywa kuelewa sababu za uwiano huu hasi na kutafuta njia za kuwawezesha watu wenye ulemavu kufanya maamuzi kuhusu kushiriki katika shughuli za kujipatia kipato.

### Jaribio la Tofauti Muhimu Kitakwimu (Jaribio la T) la GESI

Jaribio la T (t-test) ni jaribio rahisi katika uchanganuzi wa GESI wa sampuli ya data ili kufanya mahitimisho juu ya kundi kubwa la watu. Umuhimu kitakwimu unamaanisha uwezekano kwamba matokeo ya uhusiano kati ya vigeu viwili hayana uwezekano wa kutokea kwa bahati tu. Hii inamaanisha kuna sababu ambazo zinachangia uhusiano huu. Jaribio la T hutumiwa kulinganisha wastani wa makundi mawili na kuelewa kama yana tofauti muhimu kitakwimu, ukubwa wa umuhimu wa hiyo tofauti (inapimwa kwa kutumia wastani) na kama tofauti hizo zimetokea kwa bahati tu. Jaribio la T linakokotolewa kwa kutumia programu za kitakwimu kama vile STATA au SPSS. Kwa mfano, unaweza kukokotoa takwimu za T za data zilizokusanywa kwenye Jedwali 17 zinazouliza swali lifuatalo:

| Swali | Jibu |
|---|---|
| Je, unashiriki mara kwa mara katika usafi wa mazingira na usafi wa kimwili? | 1=Hapana 2=Wakati mwingine<br>3=Mara nyingi 4=Wakati wote |

Utahitaji kuweka madai ili kuona kama kuna uhusiano. Kwa mfano: "hakuna tofauti muhimu kitakwimu kati ya asilimia ya wanawake na wanaume walioshiriki katika usafi wa mazingira na na usafi wa kimwili." Hili linaitwa bunio batili. Kuna bunio mbadala ambalo linadhani bunio batili si sahihi. Linasema kuwa kuna tofauti muhimu ya kitakwimu katika asilimia ya wanawake na wanaume ambao walishiriki katika shughuli za usafi wa mazingira na usafi wa kimwili. Unatakiwa kupima bunio batili ili kujua uwezekano wa hii kuwa kweli.

Weka kigezo (kiwango cha uhakika) ambacho utakitumia kuamua kukubali au kukataa bunio batili. Kokotoa takwimu "t" kwa kutumia programu ya uchanganuzi wa takwimu ili kupata thamani ya "p" ambayo utatumia kufanya uamuzi. Thamani ya "p" ni uwezekano ulioonyeshwa ambao ni kati ya 0 na 1 na hauwezi kuwa hasi. Kama thamani ya "p" ni 5% au chini ($p < .05$), utakataa bunio batili kwani hii inaonyesha kiwango cha uhakika cha 95% kwamba bunio batili si la kweli. Utajua kuna tofauti muhimu kitakwimu katika ushiriki wa wanaume na wanawake. Kama thamani ya "p" ni ni kubwa kuliko 5% ($p > .05$), utakubali bunio batili na kuwa na uhakika wa 95% kwamba hakuna tofauti muhimu kitakwimu katika asilimia ya wanawake na wanaume walioshiriki katika usafi wa mazingira na usafi wa kimwili.

**Jedwali 32 | Mfano wa Matokeo ya GESI ya Jaribio la T**

Kushiriki kwenye tabia za mara kwa mara za usafi wa kimwili na usafi wa mazingira kulingana na jinsi. Unaweza kufanya hivyo hivyo kwa jaribio hilohilo kwa watu wenye ulemavu.

| **Kiwango cha Ushiriki** | **Asilimia** | | |
|---|---|---|---|
| | **Wanawake** | **Wanaume** | **Thamani ya "p"** |
| Haijawahi kutokea | 15 | 30 | 0.05 |
| Wakati mwingine | 30 | 45 | 0.25 |
| Mara nyingi | 50 | 23 | 0.01 |
| Wakati wote | 5 | 2 | 0.05 |
| **Jumla** | **100** | **100** | |

Hapa utasoma thamani za "p" na kuzitumia kulinganisha asilimia zilizoonyeshwa kwenye jedwali kwa ajili ya wanawake na wanaume. Utahitimisha kuwa asilimia ya wanawake ambao hawakuwahi kuwa na tabia za mara kwa mara za usafi wa mazingira na usafi wa mwili ilikuwa na tofauti muhimu kitakwimu iliyo chini sana kuliko wanaume (p = 0.05). Vilevile, asilimia ya wanawake ambao wengi mara nyingi au wakati wote walishiriki katika tabia za usafi wa mazingira na usafi wa kimwili zilikuwa za juu sana kuliko wanaume (thamani ya p ni .01 na 0.5 kama ihusikavyo). Hata hivyo, asilimia ya wanawake na wanaume ambao wakati mwingine walishiriki katika usafi wa mazingira na usafi wa kimwili hauna tofauti muhimu kitakwimu (kwa sababu thamani ya p ni kubwa kuliko 0.05). Hii inamaanisha kwamba ingawa asilimia ya wanawake ambao wakati mwingine hushiriki katika usafi wa mazingira na usafi wa kimwili ni ndogo kuliko wanaume, tofauti ni kwa bahati tu (haina tofauti muhimu kitakwimu). Hitimisho ni kwamba wanawake hushiriki zaidi kuliko wanaume katika tabia za usafi wa mazingira na usafi wa kimwili. Kuna haja ya kushawishi au kuhamasisha wanaume kushiriki zaidi. Unaweza kutumia data za kitaamuli ili kuelewa kwa nini hii iko hivi. Kwa kuongezea, unaweza kutumia wanawake kama mawakala wa mabadiliko kuwashawishi wanaume.

## Linganisha Matokeo

Baada ya kuchanganua, ni muhimu kuoanisha data ili kuelezea baadhi ya matokeo ya kitakwimu. Unaweza kutumia majadiliano ya vikundi lengwa au data za upili kutafiti kitu kilekile.[72]

72 O'Connor and Gibson (2003). A Step-by-Step Guide to Qualitative Data Analysis.

## UCHANGANUZI WA GESI WA DATA ZA KITAAMULI

Uchanganuzi wa kitaamuli huchanganua data ambazo si namba zenye mgawanyo wa GESI kama vile hisia, fikara na mitazamo.

**Kielelezo 9 | Hatua za Uchanganuzi wa GESI kwenye Data za Kitaamuli**[73]

**BADILISHA SAUTI KUWA MANENO**
Badilisha data zote zilizokusanywa kutoka kwa washiriki

**PANGA NA PITIA**
Weka alama na zipange data kulingana na chanzo na/au mbinu. Pitia vyanzo vyote vya data

**KUSIMBA**
Tengeneza mti wa kusimba na ongezea maudhui yanayojitokeza

**CHANGANUA**
Changanua maudhui makuu, mienendo, na tengeneza viunzi vinavyoshahibiana

**HOJI**
Jenga uelewa wa kina kutoka kwenye matokeo

**THIBITISHA MATOKEO**
Thibitisha kwa kuliinganisha matokeo ya kitaamuli na kitakwimu

### Mwongozo wa Hatua kwa Hatua

### Badili sauti kuwa maneno

Anza kwa kubadili sauti kuwa maneno kwa vitini, majibu, na maoni. Kwenye kila faili, hakikisha umeandika mtu aliyekuwa anazungumza na sifa zingine bainishi ambazo unaweza kuwa umeziandika kwenye vitini vyako. Maelezo haya ni muhimu kwa sababu ikiwa wahojiwa walieleza taarifa zinazohusiana na kikoa kimojawapo kati ya vikoa vitano vya GESI, ni muhimu kufahamu sifa za kijamii na mahusiano ya kimamlaka yanayoweza kuchangia namna ambavyo wanakandamizwa au kutohusishwa. Vilevile, ni muhimu kuhusisha yale yaliyoshuhudiwa au kuakisiwa kwenye mchakato huu kwa kuwa hii inaweza pia kukupatia taarifa muhimu kuhusiana na desturi, wajibu na majukumu ya kijamii na kijinsia. Kwa mfano, kama baadhi ya watu wanashiriki kutoa maoni mara chache au walikuwa hawaangalii watu machoni wakati wa ukusanyaji data.

### Panga na Pitia

Baada ya kubadili sauti kuwa maneno, weka alama na panga data zako kulingana na chanzo na/au mbinu. Unaweza kufanya hili kwa kutumia vitini vyako au programu za uchanganuzi wa kielektroniki. Kwa mfano, unaweza kupanga data kwa aina ya mhojiwa, kama vile wanaume,wanawake,wasichana na wavulana. Unaweza pia kuchagua kupanga data kwa kutumia mbinu za ukusanyaji data, hususani ikiwa kila mbinu inalenga mada maalumu. Njia bora zaidi ya kupanga data zako ni kurudi nyuma na kusoma mwongozo wako wa usaili/majadiliano na kujaribu kubainisha maswali ambayo bado hayana majibu .[74] Kisha soma tena maelezo yote ili uelewe yaliyomo.

73 Adapted from EAR. (undated).Ethnographic Action Research Training Handbook.
74 O'Connor and Gibson (2003). A Step-by-Step Guide to Qualitative Data Analysis.

## Simba

Baada ya kumaliza kupanga na kupitia data, unaweza kusimba au kupangilia mawazo, maudhui, dhana au kikundi cha maneno. Unaweza kuanza kwa upana na kisha kubainisha makundi ya maudhui na misimbo maalumu zaidi. Maudhui yanaweza kuhusisha mawazo mbalimbali. Bainisha nukuu zilizotolewa ambazo zinatoa muhtasari wa kila maudhui. Unaweza kutumia vikoa vya GESI kusaidia kupangilia maudhui. Tumia programu ya kompyuta ya Excel au vitini vya kugundisha ukutani au programu za uchanganuzi wa kielektroniki wa kitaamuli kama vile NVivo na ATLAS ti katika kusimba. Kama utatengeneza misimbo kabla ya ukusanyaji wa data kulingana na maudhui yaliyobainishwa kwenye upitiaji wa maandiko, tumia hio misimbo kwenye data zako. Ufuatao ni mfano wa jinsi ya kusimba data iliyokuswanya kutoka kwenye majadiliano na kikundi cha wanawake t peke yao. Unaweza kufanya hivyo hivyo kwa wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine.

**Jedwali 33 | Mfano wa Data Zilizosimbwa**

| Mada | Majibu | Misimbo |
|---|---|---|
| Upataji na ufikiaji, umiliki na udhibiti wa ardhi kwa wanawake | Kati ya wanawake 15 waliohudhuria mahojiano ya vikundi lengwa, 10 kati yao hawana elimu ya darasani na wengine wamemaliza shule ya msingi. Niliwauliza kama wana haki ya kumiliki ardhi wote walisema hapana. Walisema wanaweza kupata ardhi ya familia na wanaweza kuitumia, lakini hawawezi kudai umiliki chini ya sheria za kimila. Pia walisema hawana udhibiti wa ardhi kwa sababu kijadi wanawake wanachukuliwa kama mali inayomilikiwa hivyo mali haiwezi kumiliki mali. Wanaume wanamiliki ardhi yote katika jamii, lakini wanawake ndio wanaofanya kazi zaidi kwenye ardhi kuliko wanaume. Niliuliza jinsi wanavyojisikia kuhusu hilo, walisema wanakubaliana nalo kwa sababu mwanamke anapoolewa, kimsingi anahamia familia nyingine, hivyo kuruhusu wanawake wamiliki ardhi inaweza kusababisha ardhi ya familia kuhamishiwa familia nyingine. | Elimu<br>Elimu kwa wanawake<br>Kupata ardhi<br>Kumiliki na kuwa na udhibiti wa ardhi<br>Mitazamo kuhusu upataji na ufikiaji na udhibiti wa ardhi<br>Desturi za kijamii |

## Changanua

Baada ya data kuwa zimesimbwa, bainisha maudhui, miundo, au mienendo inayojitokeza zaidi. Bainisha utofauti na tafuta maelezo.

## Hoji

Baada ya kufanya uchanganuzi wako wa jumla, jiulize jinsi gani/kama majibu yanatofautiana kulingana na aina ya watu – wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Ifuatayo ni orodha ya maswali muhimu unayoweza kuyazingatia. Maswali yanapaswa kuzingatia vikoa vya GESI na yanaweza kutumika katika aina zote za programu:[75]

1. Je, kuna desturi za kijinsia na kijamii ambazo zinachangia katika malengo ya maisha, matarajio, na ustawi wa makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi?
2. Je, ni kwa namna gani shughuli, majukumu, matumizi na muda hutumika kwenye kazi ya kulipwa na kazi zisizo za kulipwa zinazoathiri makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi katika kaya zao au jamii?
3. Je, makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi yana upataji na ufikiaji wa fursa ya kutumia rasilimali za uzalishaji, kama vile mali, mapato, huduma za umma (afya, elimu, maji), teknolojia na taarifa?
4. Je, makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi yana uwezo wa kuamua, kushawishi na kuwa na udhibiti wa nyenzo, rasilimali watu, ujuzi, na rasilimali fedha, katika familia zao na /au jamii?
5. Je, makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi yana uwakilishi katika nafasi za kufanya uamuzi, na je, mawazo yao husikika katika katika mashirika ya kijamii?
6. Je,desturi za kijinsia na kijamii zinaathiri jinsi makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi yanavyoshiriki katika shughuli na kufaidika na miradi?
7. Je, jamii inawahusisha watu wenye ulemavu kwa kuondoa vikwazo vya kimwili na kimtazamo?

75 Adapted from UNDP (2013). Gender Mainstreaming Made Easy, and USAID (2017). Integrating Gender Equality and Female Empowerment.

## Thibitisha matokeo

Jaribu kuthibitisha hitimisho lako kwa kutumia data za ziada za kitakwimu au kitaamuli.

### Kuripoti Matokeo ya Kitaamuli

Anza na hitimisho lako na liimarishe kwa kutumia data zako na vyanzo vyovyote vya taarifa ya upili. Ikiwezekana, onyesha tofauti za data kati ya aina mbalimbali ya watu, kwa mfano wanawake, wanaume, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Unaweza kutumia nukuu za maneno kutoka kwenye makundi mbalimbali ya kijamii iwapo unahitaji kuboresha hoja zako au kutoa mifano.[76] Jadili maana ya matokeo hayo kwa kila kundi la kijamii, toa mapendekezo, na mikakati ambayo itafanikisha mabadiliko na mipango ya usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa kijamii.

## KUWASILISHA NA KURIPOTI MATOKEO YA GESI

Matokeo ya GESI na mapendekezo yanapaswa kuwasilishwa kwa wafanyakazi wa World Vision na wabia wengine kwa njia ambayo inaongeza ufahamu kuhusu usanifu na utekelezaji wa programu na kupinga desturi za kijamii zenye ubaguzi. Zana hii inatoa orodha itakayosaidia kuhakikisha kuwa ripoti yoyote inafanikisha hili.

### Jedwali 34 | Orodha ya Kuwasilisha na Kuripoti Matokeo ya GESI

| Je, ripoti/chapisho la taarifa: | 1=Ndiyo<br>0=Hapana |
|---|---|
| 1. Imetumia taswira au picha chanya za wanawake na wanaume, watu wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu na makundi mengine yanayokandamizwa? | |
| 2. Imetumia picha zinazochochea mawazo ya kibaguzi? kwa mfano, Je, kuna picha za wanaume wakiwa wanalea watoto au ni wanawake tu? Je, kuna picha zinazoonyesha watoto wenye ulemavu wakiwa kwenye shule za kawaida na si shule maalumu? | |
| 3. Imegawanya mafanikio kwa jinsi, umri, hali ya ulemavu, n.k? | |
| 4. Imeweka kipengele maalumu kuhusu GESI ambacho kinazungumzia mambo yakujifunza kuhusu GESI? | |
| 5. Imejumuisha GESI kwenye vipengele vyote? | |
| 6. Inatumia lugha bora? Mfano, "nguvukazi" badala ya "rasilimaliwatu" "mtu" badala ya "binadamu" au "watu wenye ulemavu" badala ya "vilema"? | |
| 7. Inawaelezea wanawake na watu wenye ulemavu kama wako katika mazingira hatarishi tu, au ushupavu na mafanikio yao pia yanaripotiwa? | |
| 8. Inatoa ripoti kuhusu viashiria vya GESI na matokeo sambamba na viashiria na matokeo mengine? | |
| 9. Inajadili tofauti kati ya makundi ya kijamii na mambo yanayosababisha tofauti hizo? au inatumia maneno ya jumla kama vile "mkulima"? | |
| 10. Inabainisha vilkwazo vinavyohusiana na kufanya sampuli ya data? Kwa mfano, kama kundi fulani (wanawake wenye ulemavu n.k.) hawakuhusishwa kwenye mchakato na hii inamaanisha nini kwenye matokeo. | |
| 11. Ikiwa wanawake na makundi yanayokandamizwa hawakuwakilishwa kwa usawa kwenye sampuli ya watafitiwa, je, hili limeelezwa kwenye kipengele cha mapungufu ya methodolojia? | |
| 12. Imenukuu na kuomba ushauri kwa makundi yanayowakilisha makundi ya kijamii yanayokandamizwa? | |
| 13. Imenukuu maandiko yenye muitikio wa GESI (mfano je, inawanukuu waandishi kutoka dunia ya kusini)?[77] | |
| 14. Inajadili namna ambavyo matokeo chanya ya GESI yanahimizwa na namna ambavyo matokeo hasi yanapunguzwa au kuondolewa? | |
| 15. Inatoa maoni kuhusu mchango wa shughuli za mradi katika uwezeshaji wa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi (kujiamini,uwezo wa kuongoza na kujiongoza wenyewe)? | |
| 16. Inatoa ripoti kuhusu uwiano wa wanawake na wanaume wanaoshiriki kwenye shughuli za mradi (kama washiriki,wafanya maamuzi au mawakala wa mabadiliko) wakati wa kipindi cha kutoa ripoti? | |
| **JUMLA YA ALAMA** | |

KUMBUKA: **Kama jumla ya alama ni** 13 au zaidi, basi umeripoti vizuri matokeo ya GESI, kwa njia sahihi na umeepuka upendeleo na mitazamo kuhusu GESI.

76 O'Connor and Gibson (2003). A Step-by-Step Guide to Qualitative Data Analysis.
77 The term 'Global South' refers, broadly, to Latin American, Asia, Africa and Oceania. The term signals a departure from a central focus on state of development (such as the term 'low-income countries') or cultural differences (such as the term 'Third World') focusing instead on geopolitical relations of power.

# VIAMBATANISHO



# **KIAMBATANISHO 1** FAHARASA YA DHANA ZA GESI

Ifuatayo si orodha yote ya dhana za msingi za GESI, imechukuliwa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

| Dhana | Fasili ya Dhana |
|---|---|
| 1. Uwezo wa kufanya mambo | Uwezo wa kufanya mambo unapatikana pale watu (na makundi) walio kwenye mazingira hatarishi ambao awali walikuwa na uwezo/nguvu kidogo, wanakuza uwezo wa kujitambua na kueleza mawazo yao, na kuwa na udhibiti juu ya maisha yao, rasilimali, imani, maadili, na mitazamo.[78] Uwezo wa kufanya mambo hupelekea kujiwezesha—**nguvu ya** kufanya mambo na **nguvu ya ndani**—kupitia ufahamu binafsi na mabadiliko ya mitazamo binafsi, jinsi mtu anavyojitazama na mahusiano ya kimamlaka. |
| 2. Data zilizogawanywa | Data imegawanywa kulingana na kundi dogo. Data iliyogawanywa inaweza kuonyesha kukosa, kutohusishwa, kutengwa na ukosefu wa usawa ambao hauwezi kuonekana kikamilifu katika data iliyojumlishwa. Data iliyokusanywa kuhusu watu inaweza kuainishwa kulingana na jinsi, umri, hali ya ulemavu, kabila, kiwango cha elimu, na tofauti za vijijini na mijini, n.k. |
| 3. Mkabala wa usidhuru | Mkabala wa 'usidhuru' katika miradi na programu inahitaji uchanganuzi endelevu ili kuhakikisha madhara yanayoweza kutokea ya kuchochea au kuimarisha ukosefu wa usawa wa kijinsia na uhusishaji kijamii bila kukusudia katika muktadha wa afua yanatathminiwa kila wakati na kufuatiliwa kwa uangalifu, na kwamba hatua za kurekebisha/fidia zinachukuliwa, ikiwezekana.[79] |
| 4. Uwezeshaji | Unatofautiana kulingana na mahali na muktadha. Ni pamoja na kukuza uelewa, kujenga uwezo wa kujiamini, kuongeza uwezo wa kuchagua, kuwa na udhibiti juu ya rasilimali na itikadi na inahusiana na na uwezo wa kufanya maamuzi. Inahusiana na mambo ya kisiasa kwa kuwa ni mchakato unaohusu kubadili mahusiano ya kimamlaka. Mahusiano jumuisni ni muhimu katika kuchochea mabadiliko chanya ya kijamii kwa kubadilisha miundo na taasisi zinazosababisha ubaguzi na kukosekana kwa usawa.[80] |
| 5. Usawa | Hali inayosababisha watu wote kufurahia kwa usawa haki za kibinadamu, mambo yanayothaminiwa na jamii, fursa, na rasilimali. Zaidi ya usawa au sheria, usawa wa kweli wa kijamii ni kupanuka kwa uhuru na kuboreshwa kwa kiwango cha maisha kwa ujumla. |
| 6. Uwiano | Ni mchakato wa kutenda haki kwa watu wote. Ili kuhakikisha haki inakuwepo, hatua zinahitajika kufidia ukosefu wa usawa kiuchumi,kijamii na kisiasa ambao umekuwa ukifanyika kwa miaka mingi na ambao unaendelea kuyazuia makundi yanayokandamizwa kupata usawa. |
| 7. Ujumuishaji wa GESI | Humaanisha mikakati inayotumika kwenye uchanganuzi, usanifu, utekelezaji na tathmini ya programu ili kuzingatia mtazamo wa GESI na kushughulikia kukosekana kwa usawa wa kijinsia na uhusishaji wa kijamii.[81] |
